**YOANNE KOLICHARAS**
**THEOLOGIEN**

# UZIMA YA MARTIN LUTHER NA FUNDISHO YA UONGO YAKE

## MKUBWA WA WAPROTESTANTS

**MUFASIRI**
**MUTAWA DAMASKINOS GRIGORIATIS**

**CENTRE MISSION ORTHODOXE**
**KOLWEZI**
**R.D.CONGO**

# MARTIN LUTHER

(1483-1546)

## Mkubwa wa Kundi la Waprotestants

Martin Luther alizaliwa mu muji Aislemben kule Allemagne mu mwaka 1483. Alifunza masomo yake ya kwanza ku muji yake. Wakati alikomea alifunza philosophie ku muji Erfurti. Wakati alikuwa kijana hakukusudia kufunza théologie. Lakini mambo moja ya ajabu, mu tarehe 2 ya mwezi ya saba mwaka 1505 akaanza kufwata mafundisho ya théologie na uzima ya upadri. Mambo gani ilimufikia? Siku moja mbingu ilijaa na mawingu, umeme na mungurumo ya radi yalifanyika katika anga, kuliwa tetemeko na woga. Basi, Martin kijana, juu ya woga yake, wakati alikuwa fasi moja akichunga kondoo za wazazi wake, akanguka chini na alizania ya kama Mungu alisirika juu yake na ya kama kisha muda kidogo mashetani watamubamba na watamutupa ndani ya gehena. Akamuita na kumuomba Mtakatifu Anna, mama wa Mzazi Mungu Maria, aliyekuwa Mulinzi wa baba yake, akasema : “ Mtakatifu Anna unisaidie. Nakuahidi ya kama nitakuwa mutawa“.

Hakupate hatari mbaya juu ya umeme, akajihakikishia ya kama amefungwa na hii ahadi yake na anapashwa kuitimiza. Na kwa sababu mama yake alimupipiga sana nyumbani bila kosa kubwa, hii yote yalimusukuma kuingia mu kundi la watawa waliyoitwa wa “Congrégration ya Mtakatifu Augustin “ kwa umro wa miaka 22. Yeye mwenyewe alisema : “ Siku moja mama yangu alinipiga mpaka kunitosha damu, kwa sababu niliiba tunda moja. Makali ya wazazi yangu ilinisukuma kuingia mu Monasteri“. Ku mwaka 1507 alipata Fumbo ya upadirisho, akawa padri. Kisha alianza kufwata mafundisho ya théologie, bila kupenda kwake na mwito kimungu kwa hii uzima ya utawa na upadirisho. Lakini, kama tulivyosema, sababu ya woga wake ya kama atakufa mu ile fasi alikuwajuu ya umeme, hii woga ilimufuata mpaka mwisho ya uzima yake. Ku mwaka 1512 akawa mwalimu wa kufafanusha Agano Jipya ku Université ya muji Bitembergi kule Allemagne. Aliishi na woga juu ya wokovu wake na alijikaza kusikia maana ya haki ya Mungu katika mafundisho ya Mtume Paulo : „Kwa sababu haki ya Mungu inaonekana ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa: Mwenye haki ataishi kwa imani“ (Waroma 1,17). Ku mwanzo yeye alifafanusha hii neno „haki“ sawa apizo na fitina ya Mungu kwa mutu. Hivi, polepole woga iliingia ndani yake. Moyo wake ilimuhamakia tena sababu ya ile mambo aliwaza mu akili yake. Tena mashaka, kutokutii na zambi ya uzini yalimuletea woga na mawazo ya kwamba amekwisha kuhukumiwa. Siku zote mu mawazo yake aliona paka Hadeze na ya kama alikuwa tayari kutupwa katika gehena. Huyu Martin alisema tena : “ Nilitubu, lakini hakuna namna ya kuishi na kitumaini mbele ya Mungu“. Peke yake alishindana katika roho na mashindano ya kipekee kwa kutaka kwake, kuliko ile mashindano kundi ya watawa ilimwaambia kushindana nayo. Tena alifanya mafungo ya chakula kupita watawa wengine wengi. Kwa mufano: Hakule katika siku tatu. Alitosha matelas pa kitanda chake juu ya kusikia baridi mpaka kuwa sawa mufu. Alikesha na alisali mingi kuliko watawa wengine. Tena aliungama mara mingi kila siku na alionyesha makosa yake ile aliwaza mu mawazo akili yake kwa sababu aliogopa ya kama ataenda mu gehena. Pa siku moja aliungama mara sita juu ya kupata maondoleo ya zambi zake, zaidi zambi za mawazo. Lakini hakuna namna ya kusikia amani katika roho yake, ao alizania ya kwamba atamufurahisha Mungu. Wakati alisikia jina la Yesu Kristu mu Kanisa ao katika mazungumuzo na watu wengine aliogopa kwa sababu alizania ya kama Mungu eko na kasirani juu yake. Tena alimuona Mungu kuwa sawa adui ya watu, mubaya, mwenye chuki, mwenye hasira na mwenye makali juu ya zambi za watu hata kama ni kidogo. Alimuona Mungu kuwa tayari kumulipiza mutu mwenye zambi hata juu ya zambi yake kidogo sana. Wakati alifanya ibada ya Liturgia mara ya kwanza, alitetemeka mwili wake muzima. Hii woga na tetemeko

yalimuharabisha misipa yake ya kichwa. Aliwaomba sana na kivukutu rohoni mwake Watakatifu wengi juu ya kumuombea kwa Mungu Yesu Kristu wokovu yake. Amekwisha kuchagua watakatifu makumi mbili na moja sawa walinzi wake na alifanya sala kwa watakaitfu tatu kila juma. Lakini, hakuna namna ya kupata utulivu rohoni mwake. Kujikaza kwake kulikuwa kwa bure. Polepole alisadiki ya kama matendo ya mutu haina na mafaa hata kidogo, hata kama ni matendo mazuri. Alichunga wazo ndani yake ya kwamba kila mutu, kisha kuanguka kwa Adamu na Eva, hawezi kufanya tendo zuri hata moja, tena na ya kwamba mutu alipoteza kabisa zawadi yote ya Mungu. Kwa hivi wokovu ilikuwa paka kazi ya Mungu : kuleta ao kukatalia neema na usamehe wa zambi.Tena alisadiki ya kama wokovu ni kazi ya Mungu, anayeokoa ao na kuhukumu kila mutu kwa hukumu yake bila mutu kuweza kubisha hata kidogo. Kwa hivi, mutu ataweza kufanya nini juu ya kuokoka ao juu ya kuepuka mbali malipizi ya gehena? Hakuna kitu kingine ila tu imani, hivi alisema martin,Luther. Lakini na hii imani Mungu anaileta kwa mutu. Kwa hivi, Martin Luther alifika na kwa kusadiki ku Ukomo kamili (Destination absolue) na kwa hii ukomo mapenzi ya kila mutu inaharibika, paka Mungu anakamata mpango ya kuchagua wanani wataenda mu Paradizo na wanani wataenda mu Gehena. Martin Luther alihuzunika sana juu ya mwili wake na juu ya roho yake, kwani hakujua kama ataokolewa ao atateswa pamoja na wenye zambi mu gehena.

Hii mawazo ya roho yake ilimuteswa sana, mpaka wakati alitajwa kuwa mwalimu ku Université ya Bitembergi. Tangu ile wakati alisikia ya kama neno “haki” maana yake ni “neema takatifu na mapendo ya Mungu kwa wanadamu”. Alisikia ya kama kweli Mtume Paulo anasema hivi : „Kwa maana sioni haya kwa Habari Njema, kwa sababu ni uwezo wa Mungu unaoleta wokovu kwa kila mutu anayeamini; kwa Muyuda kwanza, na kwa Muyunani vilevile” (Waroma 1,16). Mustari ingine 17 ilimujaza na kitumaini kwa sababu alisadiki ya kama mutu ataokolewa paka kwa imani. “Mwenye haki ataishi kwa imani” (Waroma 1, 17). Tangu ile wakati alichunga ndani yake hii wazo : ya kwamba paka imani inaweza kumuokoa mutu, kwa sababu namna gani matendo yake maskini yataweza kumuokoa?

Hii haiko ya mafaa?.Matendo yake maskini yataweza kumusaidia?

Ku mwanzo ya ujana wake alimuona Mungu kuwa sawa mwenyi kuazibu watu, lakini sasa anamuona kuwa mwema kamili na ya kama haazibu mutu hata mumoja. Nikusema alisadiki kabisa ku mapendo ya Mungu kwa watu na alikataa kabisa haki yake Mungu. Kwa hivi, alisikia ndani yake ya kama aliokolewa kwa tetemeko na shaka ya wokovu wake. Alisikia ya kama aliangaziwa kwa mapendo kimungu na iliondoka mbali yake uzito ya zambi zake zilizomuteswa kabisa. Ku mwaka 1517 aliandika hivi : “Mutu hawezi kusimama peke yake mbele ya Mungu na zambi yoyote, hata ni kidogo“.

Ilipita wakati, Martin alisadiki ya kama mapendo ya Mungu ni kubwa na alisema mara mengi: “Mimi siwezi… Mungu anayelipiza mutu na anamuhukumu...Mungu wa Wakristu ni Mungu wa mapendo“. Hii imani ilimufurahisha sana, lakini mara moja mafundisho ya walimu wa Kanisa katholika ya Roma ilimuletea woga juu ya ile malipizi Mungu anawapa watu wenye zambi katika hii uzima, tena na ku Purgatori na ku uzima wa milele ndani ya gehena. Kwa hivi aliondoa mu akili yake wazo la haki ya Mungu na alichunga ndani yake mafundisho ya wema kubwa wa Mungu. Tena alizarau na alitosha mu akili yake wazo ya kwamba mutu ataokolewa kwa matendo mema. Alizoea kusema ya kama kila mtu hawezi kufanya kitu juu ya wokovu wake, kwa sababu amekwisha kuanguka sana. Juu ya wokovu wake paka neema takatifu ya Mungu inatenda“. Lakini, kwa hii mawazo yeye bado kupata amani na utulivu rohoni mwake. Mara mingi alisema hivi : “Kama, kwa mufano, mafundisho yangu juu ya wokovu itakuwa ya uwongo, hii kazi yote ya kutayarisha mafundisho ya wokovu ya watu itabomolewa...“.

Ni kweli, Martin Luther hakusadiki kabisa na utaratibu hii mafundisho yeye alifundisha wafwasi wake. Alisemaka hivi: „Mimi siwezi kusadiki na imara hii maneno ninasema kwa watu na ninaandika katika vitabu vyangu...Ni kweli, watu wanaamini ya kama mimi ninasadiki, bila

shaka kwa Evangelio na kwa ile ufafanusho mimi ninafanya kwa Evangelio ya Kristu. Tena alitafuta kutosha katika Agano Jipya mafundisho fulani yale hayakumupendeza. Aliwaza ya kama Maandiko Takatifu ni kitabu kilichoandikwa na maongozi ya Roho Mtakatifu, lakini hapana Kitabu muzima. Yeye alisemaka: „Neno la Mungu ni ndani ya Maandiko Takatifu, lakini Maandiko Takatifu haiko Neno la Mungu".

Katika hii maneno inaonekana ya kama Martin hakuimarishe mafundisho yake pa Evangelio. Haiko ya kweli hii mambo wanasema wafwasi wake (waprotestant) ya kwamba Martin Luther na walimu wengine walikuwa na imara na utaratibu mu uzima yao juu ya Maandiko Takatifu. Kwa mfano Barua za Mitume Petro na Yakobo, kwa sababu yanafanana. Luther anayazarau. Havumilie hii mustari ya barua ya Mtume Yakobo : " Imani pasipo matendo haizai" (Barua ya Yakobo 2,20). Kwa sababu Mtume Yakobo alileta mafaa kubwa kwa matendo mazuri; pa hii fasi Luther alisema ya kwamba hii barua ni ya mayani. Tena alikataa kitabu cha Ufunuo cha Yoane na hasadiki ya kama ni Mtume Yoane alikiandika kwa sababu alifundisha sana mafaa ya matendo mazuri. Hakuna namuna kwa Luther kusikia hii mustari ya Ufunuo : " Heri wale wanaosafisha nguo zao, maana watakuwa na haki ya kula matunda ya muti wa uzima na kuingia katika milango ya muji wake..." (Ufunuo 22,14-15). Hii maneno ya Mtume Yoane yalimutetemesha. Ku ile Monasteri aliingia sababu ya kupata utulivu na ukimya rohoni mwake haikufurahisha mapenzi yake. Ku mwaka 1518 alisema juu ya mwili wake : " Ninafahamu mutu mumoja aliyepita katika woga kubwa na hata lugha moja haiwezi kuisema…Ule mutu hakujuwa mwili na woga, hakuna namna ya kunisadiki. Kama ilipashwa kuvumilia hii woga na tetemeko hata nusu ya saa, ilipashwa kupoteza yote, tena na mifupa yake yalipashwa kuwa sawa maivi". Na kama alivyosema rafiki yake Melakthon, tetemeko na woga ya Luther ilikuwa ya hatari sana, na sababu ya hii woga hakuweza kuokolewa katika uzima yake sawa mutawa ku monasteri yake.

## UGOMVI YAKE YA KUKOMBANISHA KANISA YA PAPA (KATHOLIKA YA ROMA)

Mambo yalimusukuma Martin Luther kukombanisha na kutengeneza mambo ya Kanisa yalikuwa ku mwanzo ni makosa ya Kanisa ya Papa wa Roma. Luther, kwa sababu alikuwa na mafundisho mingi, alikuwa na namna ya kujua makosa ya Kanisa ya Papa. Kwa sababu Luther alikuwa huru, hakuweza kuvumilia uharibifu wa mafundisho ya Kanisa. Ku mwanzo ya uzima yake ya utawa alimuheshimu papa, lakini, wakati alimufahamu muzuri, aliona ya kama papa ni sura ya majeshi ya hadeze na ya kama anataka kuepusha wakristu mbali ya Kristu.. Huyu papa eko Anti-kristu, na ananyanganya uwezo wa Kristu na anaonekana kuwa sawa Kristu. Aliandika ndani ya vitabu na ya barua zake ya kama papa anafanana na anti-kristu. Na hii mustari ya Mtume Paulo ( 2 Wathesaloniki 2,3-8) pahali anasema juu ya mutu wa zambi na ya muharibifu, anasema ya kama huyu muharibifu ni papa.

Tena na mapadri wengine wakubwa wa kanisa ya papa wamekwisha kumuchukiza sababu ya tabia yao mubaya. Ku mwaka 1510 alienda mara ya kwanza ku muji wa Roma sawa padri . Kule alishangaa juu ya mapadri wa inchi ya Italie ambao waliisha ibada ya Liturgia sita ao saba ile wakati yeye aliweza kufanya Liturgia paka moja. Siku moja, alikuja kwa mukutano mumoja wa maaskofu wote ku muji wa Roma. Alishangaa na alisirika sana kwa sababu maaskofu wengine walisema na majivuno na walitukana na kuchekelea Fumbo ya Komunyo takatifu. Maaskofu hawa walisema, walichekelea, ile saa ya Matoleo ya mwili na ya vinyo katika Liturgia, walisoma hii sala na walisema: " Uko mukate na utabaki mukate; Uko vinyo na utabaki vinyo ". Lakini, waaminifu wale hawakujua lugha ya kilatini walipokea sala yao na heshima na walisema ku mwisho: Amina. Mara moja mapadri hawa walicheka sana.

Martin Luther akasema : Ee Mungu wangu, ni nani huyu papa na mapadri wake wakubwa?”

Zaidi alihuzunika sababu ya tabia mbaya ya mapadri na watawa wao. Uzarau yao mbele ya waaminifu wao hakuna namna ya kuisema, ni mbaya sana. Luther aliandika hivi : “Inchi inajaa na mapadri na maaskofu na makardinali, wenye kujitenga mbali ya waaminifu wao, sawa vile mbingu iko mbali ya dunia na wanamuzarau Kristu na majivuno yao. Martin Luther aliiita Ma Monasteri kuwa fasi ya zambi ya mwili na fasi ya miungu ya wapagano ambapo panafanyika mambo mengi mbaya. Alisemaka tena : “Uzima safi ndani ya Monasteri ni ya bure. Inapashwa kijana mumoja kati ya wale waliingia mu ya tanuru moto ku Babiloni awe ndani ya ile Monasteri na atabaki safi na bikira. Wakubwa wa ma Monasteri ingine waliwasukumu watawa wafanye mafungo ya chakula siku nyingi na sala ya usiku juu ya kuwapeleka ku lufu.

Mapadri wengi sana waliwadanganya waaminifu kwa kuwafanyia ibada mbalimbali ao kuwapa mifupa ya watakatifu juu ya kuibusu sababu ya kupata feza. Walizunguuka katika muji na walionyesha kwa waaminifu wao mifupa ya bure wakiwaambia ya kwamba ni mifupa ya watakatifu fulani, hii yote ni kusudi wapate feza mingi. Wathéologiens waprotestants ku mwanzo walisema ya kama mapadri ya Kanisa ya Papa waliwawekea waaminifu wao vitu vya uwongo sababu ya kuvisujudu, kwa mufano bawa ya Malaika Mikaeli ile ilianguka wakati huyu Malaika alimukombanisha shetani ku mulima Nabab. Tena walifanya kilauri moja na walisema ya kwamba na hii kilauri ni nabii Musa alinywiyamo maji mu jangwa. Tena waliwapa nyota moja waisujudu wakiwaambia ya kama hii ni ile nyota iliwaongoza wenye akili tatu ku Betlehemu sababu ya kumuabudu Bwana Yesu Kristu. Tena walisema ya kama walichunga na machozi ya Bwana Yesu ile alilia wakati alikufa rafiki yake Lazare! Juu ya kuongezea feza yao ikuwe mingi, Mapadri walifundisha ya kama ibada ya Liturgia inaleta feza mingi kama kila mwaminifu analipa juu ya kumufanyishia liturgia yake. Tena inaleta faida kubwa ya kiroho kama anaiomba paka mtu moja. Walisema hivi juu ya kupata feza mingi kwa wale watu walipenda kufanyishisha Liturgia mingi. Mapadri ya kanisa ya papa walisema: „Kama watu wakufanyishisha Liturgia weko mingi, neema ya liturgia itakuwa kidogokidogo kwa wale watu wanaifanyishisha. Kama weko watu wachache watapokea neema mingi”. Tena walisema: “Kama mwaminifu mumoja analipa kwa padri feza mingi neema ya ile liturgia itakuwa mingi ”. Na mafundisho ingine sawa hii yalimuhuzunisha Martin Luther na yalitayarisha roho yake juu ya kutoka inje na mbali ya kanisa yao.

Lakini ile fundisho ilimusirikisha kabisa na ilimusukuma kukamata mpango juu ya kukombanisha hii Kanisa ya papa ilikuwa fundisho ya Purgatori, nikusema ni fasi kisha lufu ya mutu inapita moto ya Roho Mtakatifu na inasafisha roho za wale watu hawajatayarisha roho zao juu ya kuingia mu paradizo. Ilimusirikisha tena ni fundisho ya wapapa juu ya kuuzisha makaratasi ya Kusamehe zambi. Mutawa Yoane Checheli alizunguuka fasi ya Saksonia kule inchi ya Ingreza (Angleterre) na aliuzisha makartasi ya usamehe namna moja mbaya na bila haya. Alihubiri juu ya makartasi ya usamehe sawa vile wenye kuuzisha biashara wanatumika pa soko. Huyu Mutawa hakuwa mutu wa imani na hakusopoke mu uzima yake kwa mambo ya uzima safi. Papa Léon wa Kumi aliyemupa baraka ya kuuzisha makartasi ya usamehe alimuita ule mutawa “imbwa mchafu”. Huyu Checheli aliuzisha makartasi ya usamehe sawa mutumishi wa mkubwa wa Kanisa ya jimbo Moguntia, jina lake Albertos, alikuwa amekwisha kununua haki kwa papa Leon wa Kumi kusudi auzishe katika majimbo yake makartasi ya usamehe katika miaka minane. Lakini watumishi wa banki ya Fuggeri walimunyanganya ule mutawa nusu ya ile feza alipata.

Ni kweli, matendo haya yamekwisha kuleta machukizo kwa waaminifu wengi na yalikuwa ni sababu kwa Martin Luther kukamata mpango ya kukombanisha kanisa ya papa, kuondoka inje yake na kisha kufungula kanisa yake. Ile ugomvi alikombanisha Papa na matusi mbaya yasiyo na heshima inatuonyesha ya kama huyu Luther hakukuwa paka kafiri na mutoaji wa

kanisa yake, lakini yalionyesha chuki kubwa na kasirani ile alikuwa nayo juu ya papa na kanisa ya Katholika ya Roma. Aliandika ya kama cheo cha papa wa Roma kilitoka kwa shetani. Shetani alimukokota papa toka kinywa cha Hadeze. Alifatula papa na kichwa chake kilikuwa sawa kichwa cha punda. Pa picha ingine alimufatula papa mwenye kukaa juu ya bega ya nguruwe moja mwanamuke. Alisemaka: " Mpaka mwisho wa uzima yangu mimi sitaacha kumuomba Mungu kukombanisha papa na Waturki".

Fasi ingine aliandika : "Kweli, Kanisa ya papa iko na uwongo na hii uwongo ni uwezo wa shetani sababu ya kuharabisha kila mwaaminifu, sawa vile mafundisho ya kweli ya Mungu ni uwezo wa wokovu wa kila mwaaminifu". Mu Kitabu chake "*Kupinganisha kanisa ya papa*" anaandika namuna mbaya kabisa ya kumukombanisha papa. Anamuita: "*Mtu mbaya, mkubwa wa watu wabaya*". Pa fasi moja ya hii kitabu chake anaandika: "*Kuja hapa, ee papa, punda na masikio yako murefu na kinywa chako chenyi kulaaniwa sababu ya mafundisho yako ya uwongo*". Martin alisema mara mingi ya kama papa ni musaidizi wa shetani. Ni anti-kristu. Kadiri ya miaka ya maisha yake na chuki ndani ya roho yake ilizidi. Alimuita „*nguruwe ya shetani*", mwenye kuweka pa kichwa ya mapadri alama ya nyama".

Wakati Martin Luther alikuwa ku mwisho ya uzima yake, alisema: „*Kwa maana Mungu alivyopenda ulimwengu, hata kutoa Mwana wake wa pekee, ili kila mutu akimwamini asipotee, lakini apate uzima wa milele*" (Yoane 3,16). Tena na mukono wake wa kupooza na wenyi kutetemeka aliandika hivi ku ukuta : „ *Wakati niliishi nilikuwa laana kwako; kama mitakufa, ee papa, nitakuwa lufu yako*". Hii maneno yake inatuonyesha hii chuki na roho mbaya alikuwa nayo Martin Luther kwa kumukombanisha Papa. Mambo yake ni magumu sana sababu ya maneno haya alisema mbele ya kufa kwake. Nikusema hatubu juu ya chuki yake mbele ya papa na Kanisa yake. Tunaona ya kama mkubwa wa Waprotestants alikuwa mu hali mbaya mbele ya kufa kwake na alionyesha majivuno na chuki mbele ya papa na kanisa yake.

## <u>SABABU KUBWA YA MARTIN LUTHER KUTOKA KU KANISA YA KATHOLIKA YA ROMA</u>

Makosa haya ya kanisa ya papa yalikuwa sababu ya inje ya Martin kutoka ku kanisa yake. Lakini kulikuwa na sababu ingine ile ilikuwa ndani ya roho na uzima ya Luther, ile ilimuletea fujo mu roho yake na ilimusukuma kumuchukia papa. Luther, sawa tulisema, alikuwa mutawa juu ya ahadi yake, wakati aliogopa ya kama umeme itamuuwa ku fasi moja ya muji wake. Lakini roho yake haikuitwa bado ku hii uzima ya utawa wala kupata amani ndani ya hii uzima. Katika roho yake alitaka kuishi na ndoa . Na kwa sababu alikuwa mutawa, hakuna namna ya kuowa. Kama, kwa mufano, aliowa, mara moja kanisa yake ilipashwa kumuhukumu, lakini hii mambo yake hakuna namna ya yeye kuivumilia. Tena hakuwa na nguvu rohoni mwake juu ya kuvumilia mashimango ya watu kama alivula manguo yake ya utawa na kuowa mwanamuke. Tena ndani ya roho yake alikuwa na chuki juu ya mapadri na juu ya kanisa ya papa, kwa sababu papa amekwisha kukamata mpango ya kukataza mapadri wake wasiowe. Aliwaza namna gani atatupa ile muzigo muzito ya utawa wake sababu ya kuwa huru juu ya kuowa na kufanya jamaa yake. Namuna ilikuwa paka moja : Kuleta fujo na kukombanisha Kanisa na sheria za kanisa ya papa. Kwa kuimarisha hii ugomvi ilipashwa mwili wake na ndugu zake waitike ya kama uzima ya watawa haifwate mapenzi ya Mungu.

Kweli, alitumika na alifanya nguvu namuna yote juu ya hii mambo. Kila wakati alishitaki na kuchukia uzima ya watawa na amekwisha kukusudia kuvula manguo yake mweushi, kwani aliizarau na kuichukia. Lakini hakupenda kukamilisha mara moja hii mpango yake. Aliongojea wakati muzuri. Alihubiri sana juu ya kukombanisha uzima ya watawa pasipo kusema ya kama anafanya hivi jjuu ya uzima yake, lakini ilionekana sawa anapenda kusaidia watawa wengine,

kwani aliwaza ya kama mu uzima yao watawa waliteswa na yeye alitaka kuwaokoa. Siku moja mutu mumoja mkubwa, mufwasi wake, jina lake Karlstad, alisema ya kama mapadri na watawa wanapashwa kuowa. Luther alijibu ya kwamba kama kweli ni fundisho ya imani juu ya wokovu, monasteri yote yanapashwa kuwa wazi, maana watawa, wanaume na wanawake, wanapashwa kurudi mu dunia kusudi waowe na kuolewa. Kwa sababu alipenda kufuchika mawazo yake kwa ule mutu alimwaambia: " Mimi lakini nataka kuchunga uhuru yangu, sipende kuowa".

Ugomvi yake ya kukombanisha uzima ya utawa ilizaa matunda mengi, kwani Monasteri mingi yalianza moja kwa ingine kuwa wazi. Watawa, wanaume na wanawake, walirudia mu dunia. Ku mwaka 1523 mutawa mwanamuke Ekaterini Mbora, ambaye kisha wakati kidogo aliolewa kwa Luther, alitoka mu monasteri yake pamoja na watawa wanawake munane. Lakini, kwa sababu wazazi wao walikataa kuwachunga nyumbani mwao, hawa wanawake watawa walirudia kwa Luther na walimuomba ulinzi na saidio yake. Martin Luther aliwapokea na aliwachunga mu monasteri yake. Hii mapatano yake na watawa wanawake iliharibisha mawazo yake. Zaidi kupatana kwake na mutawa mwanamuke Ekaterini Mbora. Mpango yake juu ya kuowa sasa likuwa nguvu ndani ya roho yake. Lakini, mbele ya miezi chache alimwaambia rafiki yake, jina lake Spalatino, ya kama hana hata na mapendo ya kuoa. Wakati alipata habari ya kama rafiki na musaidizi wake Karlstad na watawa wanaume wengine wanaowa, alishangaa na alisema hii maneno : " Kwa jina la Mungu, ni kweli wakaaji wa muji Bitemberg watawapa watawa wanaume mabinti wao juu ya kuwaowa?" Tena alisema na maneno mengine ya kuchekelea : "Lakini, hakuna namna kunipa mimi binti hata moja?"

Basi, aliendelea kukombanisha uzima ya watawa na aliwaambia watawa wanaume wote watoke mu monasteri yao na warudi mudunia. Na yeye kisha wakati kidogo alizunguuka ndani ya monasteri yake, kwani kwa shauri yake, watawa wote walitoka na walikimbia, alisikitika rohoni mwake, kwani alibaki kule peke yake. Mu mwezi wa Decemba mwaka 1524 na yeye alitoka ku monasteri yake, na alituma funguo ya monasteri kwa jemadari mkubwa wa police wa muji Bitembergi, na alimwaambia ya kama hakuna mutawa hata moja ndani ya monasteri yake. Basi, Luther alivula kanzu yake mweushi na manguo yake ingine, alivaa manguo sawa laike na alianza kusema kusema mambo ya kuowa bila kuogopa.

Hii tabia yake ilileta makelele mingi na watu walianza kumuchekelea na kumuchokoza. Waaminifu walimwaambia ya kama sababu ya hii tabia yake ulimwengu muzima itacheka na shetani naye atacheka kule chini ya gehena. Lakini Luther aliwajibu: "Ndiyo, nitaowa na ulimwengu itanichekelea". Ni kweli, mu tarehe 11 mwezi ya sita mwaka 1525 aliowa ule mutawa mwanamuke Ekaterini Mbora. Luther alikuwa na umri wa miaka 42 na "bibi" yake na umri wa miaka 27. Luther akasema : " *Niliowa sababu ya kumuchekelea shetani*".

Tangu ile wakati tabia yake iligeuka. Na mafundisho yake ilikuwa ingine. Alihubiri mafundisho ingine juu ya zambi ya mutu na usamehe yake kwa Mungu, watu walishituka. Kwa mufano alisema: *"Kuwa mwenye zambi, tenda zambi zote, lakini umwamini sana Kristu na utafurahi karibu ya Kristu"*. Mbele ya rafiki yake Melakthon alisema: " *Tenda zambi wakati mwili wako ungali na nguvu . Mungu anasamehe paka mutu mwenye zambi kabisa"*. Na alimwaambia mutu mumoja hivi : *kama haufanye zambi, majivuno itazaliwa ndani yako*. Mufwasi moja alimuuliza kama itawezekana kwa mutu kushika amri hizi zote zinaandikwa katika Evangelio ya Kristu, yeye alimujibu: *"Mungu anaamuru, lakini ni kufwatana na nguvu ya mutu*". Lakini ndani kabisa mu roho yake Luther alihuzunika sana juu ya zambi zake zote na aliona ya kama watu wote wanamuzarau. Tena Luther, aliandika hivi mu kitabu chake : " *Juu ya ndoa yangu nasikia ya kama nilianguka chini kabisa na nilipoteza heshima mbele ya watu wote"*.

## UZIMA YAKE NDANI YA JAMAA YAKE

Alipitisha uzima yake pamoja na bibi yake na watoto yake katika furaha na sikitiko mingi. Matunda ya hii hali ya roho yake yalikuwa hii maneno alisema kila wakati mara ingine ya kutukuza ndoa, na wakati ingine ya kuizarau, wakati ingine ya kuihukumu, wakati ingine ya kuleta haki mu mwili wake. Alisema: *"Ndoa ni musingi wa jamii, musingi wa uzima na wa dini"*. Tena aliongeza na uchungu rohoni yake: *"Ni mapashwa ya kila mutu; sawa vile kila mutu anakula, anakunywa, anatema mate na hivi hivi"*. Ilikuwa wakati na ilisika sababu ya sheria ya ndoa, alipaza sauti na kulalamika ya kwamba *"sheria inaleta fujo", kwa hivi wanaume "wanapenda vijana wanawake na hapana wa wake wao"*. Hii maneno yake yalikuwa mabaya sana kwa sababu yeye mutu aliyeonekana kati ya watu sawa mkubwa anayeweza kutengeneza mambo ya jamii. Tena ubaya yake ilizidi sana sababu ya matusi yake mbaya. Ku mahubiri yake moja alisema hivi : " *Kama muke wako hakupendeze, umuache, chukua mujakazi wako awe muke wako"*.

Hii maneno na ingine ingine yanaonyesha, sawa vile anasema Daniel Rops, hii fujo ilikuwa ndani ya roho yake na ya zamiri yake. Alifika mpaka kusema maneno mbaya ya kukombanisha Fumbo ya ndoa. Mara mingi alisema: " *Mimi siwezi kusikia namna gani ndoa ni Fumbo ya Mungu. Mapatano gani iko kati ya ndoa na imani yangu juu ya wokovu wa roho yangu?"* Wakati aliowa, huyu mutawa mwenye nguvu ya kutumika alinenepa sana na alikuwa sawa kijana. Macho yake siku moja yalikuwa na ngiza, siku ingine yalikuwa na nuru, saa ingine yalikuwa ya makali.

Mbele ya bibi yake (mutawa Ekaterini) alikuwa mara ingine mwema, mara ingine mukali na mugumu, mara ingine alimuchekelea ao ya kumuumiza zamiri kwa maneno yake mbaya. Saa ingine alimuita Katerine, saa ingine Keta, lakini mara mingi alimuita Lutheriene toka jina lake. Akimuomba mashauria alimuhakikishia ya kama atayatimiza. Mara ingine alimuita fundi wa vinyo. Wakati ingine alimuita mupenda-feza, tabia yake ilikuwa mbaya sana. Mu barua moja kwa bibi yake , ile aliandikaka mu tarehe 1-2-1546, aliandika ku mwanzo hivi: *„Kwa mupendwa kamili mukubwa wa nyumba yangu Katerina, Lutheriene, muganga, mtoto wa Zulsdorf, mkubwa wa kununua nguruwe na kufanya kila kazi yenye kuwezekana kufanyika"*. Maneno na majina mengi alisema na kumupanga muke wake. Tunapata mambo haya katika barua zake kwa muke wake.

Kisha kuunga ndoa yao bila fumbo ya kanisa, walizaa watoto sita. Katika hii jamaa yao walipata furaha na sikitiko. Wakati ilifika saa ya muke wake kuzaa mtoto yao wa kwanza, aliandika mu tarehe 26-5-1526 barua kwa rafiki yake akasema : "*Kisha wakati kidogo atazaliwa mtoto moja kwa wazazi mutawa moja mwanaume na mutawa moja mwanamuke*". Lufu ya mtoto yake mwanamuke jina lake Magdalena, ilimupa sikitiko mingi mu roho yake. Tunapashwa kusema ya kama Luther mara mingi mu uzima yake alikuwa na roho mwema na teketeke kwa watoto na jamaa yake. Lakini roho yake ilianguka na alikuwa mukali na mugumu na mwenye mawazo mbaya.

## MAKOSA NA MANENO YAKE YA AJABU

Sisi tunashangaa kwa sababu kila wakati Luther alianguka katika mawazo mbaya na alikuwa karibu ya kusadiki ya kama majivuno na zamiri yake juu ya kujibu hii mambo ya kuacha kanisa na utawa na upadirisho yake yalikuwa sababu kubwa ya kuwaza na kusema ubaya juu ya kukombanisha sheria na amri za Mungu. Alisikia ni lazima kabisa kupata ukimya ndani ya roho yake na alikataa kujuwa ya kama yeye alikuwa kisa ya matendo yake yote. Ni hivi alifika pa fasi ya kukataa uhuru na mapenzi ya kila mutu, na ya kwamba kila mutu hana sababu ya matendo

yake yote. Hii fundisho yake ya uwongo iliharibu zima ya wafwasi wake, kwa sababu walikataa ya kama hawako huru na kwa hivi wao si sababu ya matendo yao yote. Mu Kitabu chake kimoja kile aliandika mu mwezi wa Dekemba mwaka 1525 na titre : „De servo arbitrio“ aliandika maneno yale yalishitusha watu. Aliandika hivi *: " Kila mutu eko na mapenz yake,, lakini hapana mapenzi ya uhuru. Kwa mufano, mutu anaomba kitu moja, anakipenda, lakini bila uhuru, ni kwa lazima.* Akaongeza : "Uhuru wa mapenzi ni uwongo sana. Paka Mungu eko na uhuru ya mapenzi yake, apana kwa mtu mwingine“. Huyu anaona ku mbele, anatangulia kusema mbele ya wakati na anamaliza kila tendo na mapenzi yake isiyokuwa na kosa, ni ya milele na isiyoharibika“. Hii maneno yake inafanana na umeme ile inaanguka chini udongoni, inabomoa udongo na inaharibu musingi ya uhuru na ya mapenzi ya mutu.

Tena Luther alizaa mu akili yake mawazo ya hatari. aliondoa, alikata, alichanga, ao aliharabisha mistari ya Maandiko Takatifu kwa kila kazi alitaka kufanya. Ku mwisho alisadiki na kusema ya kama kila kitu inatufuata, hata kama inakuja mara moja, inakuja katika lazima, bila mapenzi ya mutu. Tena pa hii fasi alisema : „ Mapenzi ya mutu ni katika vitu viwili, sawa vile nyama na vitu pa mabeka yake. Kama Mungu atakaa juu ya ribeka yake, huyu nyama ataenda ku hii fasi Mungu anapenda. Lakini, kama shetani atakamata fasi ya Mungu na atakaa pa ribeka yake, huyu nyama ataenda ku hii njia shetani anataka. Haiko mapenzi yake ya furaha ya kwenda wapi anataka, lakini ni mapenzi ya ule mwongozi atakaa juu yaa ribeka yake na huyu nyama atatii mikono ya mwongozi wake...Kwa hivi, basi inaonekana ya kama mapenzi ya uhuru ni haki paka ya Mungu, na hakuna namna wala uwezekano kwa mutu mwingine kupata hii zawadi ya uhuru. Kwa sababu paka Mungu anaweza kutenda kila tendo anataka kufanya mbinguni na duniani.

Pa hii mawazo na mafundisho yake Martin Luther hasopoke na hasikie nini inasema Maandiko Takatifu. Tena anakanyanga akili ya mutu na anamuona Mungu sawa muzulumu asiye na wema, mwenye kutuma watu wamoja mu gehena bila daraka ya matendo yao na wengine katika Paradizo bila kuwafanya kuwa watu wazuri. Tena aliingiza ndani ya mwili wake na ya wafwasi wake hii shaka ya kama Mungu atamutuma mu gehena ao mu paradizo. Tena aliwaongoza wafwasi wake mu njia yasipo na kitumaini na wale watu kutenda zambi zote za mwili, kwa sababu, katika hii mafundisho ya Luther, walisema ao waliwaza hivi: "*Kama iliandikwa na Mungu ya kwamba nitaokolewa, nitaokolewa. Nikusema, kama Mungu amekwisha kukamata mpango juu ya kuniingiza mu gehena, mimi sitaweza kufanya kitu, kwa sababu ni mapenzi yake“.*

Luther alifundisha watu ya kama kila mutu atafwata ukomo yake, katika mapenzi ya Mungu, bila mapenzi yao. Juu ya kusimamisha nguvu mahii fundisho yake alikimbilia kupata musingi kwa waandishi wapagano, kwa sababu alikataa kupata mafundisho ya Maandiko Takatifu. Kwa hivi, alikimbilia kufwata maneno ya Virgilius. Hii mafundisho yake Daniel Rops anaiita "*ya kuoza na yenyi kuzarauliwa*", na eko na haki.

Tena Luther amekwisha kushikwa na mawazo ya dini mbaya na aliteswa sana mu uzima yake. Aliteswa sababu ya woga yake ya upumbafu na alizani ya kama shetani alimufuata nyuma yake. Alisema ya kama alimusikia shetani anamufwata mu mukongo yake siku zote za uzima yake. Alisema ya kama, aliona matunda fulani yalikuwa ndani ya sanduku moja yalitetemeka kwa nguvu ya shetani. Alisema tena ya kwamba siku moja alisirika sana kwa hii tendo la matunda ndani ya ile sanduku na alitupa chini chupa na wino lakini chupa ilipasu ku ukuta ya nyumba yake. Mkubwa Bainton anasema ya kama Luther alikuwa na mawazo haya ya kutetemeka woga na kuwaza mubaya tangu kwa wazazi wake. Ni kweli, wazazi wa Luther walikuwa watu wa mugini, bila kujifunza mingi na walikuwa na imani moja yenye kuchangana na mambo ya shetani, waliamini dini ya wapagano katika inchi ya Allemagne. Kwa mufano, walisadiki ya kama pepo, maji, fasi ya pori ni yenye kujaa na walozi na pepo wachafu ya shetani. Waliamini ya kwamba kila ugonjwa na uharibifu juu ya mvua mingi ni matendo ya roho mchafu ambao wanapenda kuangush watu ndani ya zambi, ni hivi watu waliishi ndani ya giza. Mama yake ya Luther alisadiki ya kama

mashetani wanaweza kuiba mayayi, maziwa, manteka na ingine…Inaonekana, basi, ya kama mawazo haya yamekwisha kuingia mu uzima yake tangu utoto wake na yalibaki ndani yake siku zote za maisha yake.

Tena mu maisha Luther alikuwa na majivuno mingi na imani paka ya mwili wake na ya akili yake. Alisadiki ya kama paka yeye peke yake anaweza kufafanusha maana ya Maandiko Takatifu kupita Watakatifu wakubwa wa Kanisa ya Kristu, tena kupita Mikutano mikubwa ya Kanisa. Juu na watu wengine wasadiki ya kama paka yeye peke yake anaweza kufafanusha Maandiko Takatifu, alipata maarifa moja.

Alisemaka ya kama katika Maandiko Takatifu kuna vipande mbili. Kipande moja cha inje na kipande kingine cha ndani. Maana, ile iko ndani ya Biblia mtu hata mumoja hawezi kuyasikia, wala neno moja, hata kama eko na nuru ya Roho wa Mungu. Kwa sababu watu wote weko na roho ya giza na hawawezi kusikia ao kujua ni nini mafundisho ya kweli. Hawasikie Mungu ni nani, wala sheria zake ni nini, wala kitu kingine. Roho wa Mungu anapashwa kumusaidia mutu kwa kusikia maana ya Biblia na ya mafundisho yake yote.

Sababu ya hii mawazo yake mbaya alitangulia kusema ya kama Mapadri wakubwa wa Kanisa ya Kristu na Mikutano mikubwa hawana na nuru ya Roho Mtakatifu, na kwa hivi Mapokeo Takatifu (Les SaintesTraditions) ni matungo ya bure, hakuna namna mtu kusadiki hii Mapokeo na kitumaini. Halafu, juu ya mwili wake alisema ya kama yaya alipokea Roho Mtakatifu na kwa hivi, paka yeye anaweza kusikia na kufundisha maana ya mafundisho ya Biblia. Lakini, hakusia ya kama hii maneno yake inajaa na majivuno mingi na ya kama kuiko namna watu wengine watakataa hii imani yake ao kuiko namna watu wengine watapokea hii mafundisho yake, sawa vile alifanya kisha miaka ingine mkubwa wa Témoins de Jéhovah, Karol Roseli aliyetoka na makundi ya Waprotestants. Kwa hivi, hii ilikuwa ni sababu ya Luther kupoteza mafundisho ya Kanisa ya Kristu, ni majivuno yake kubwa na imani ya akili yake na ya mwili yake.

## <u>TABIA YAKE MBELE YA KANISA ORTHODOKSE</u>

Halafu, kulikuwa namna ya yeye kutoka ku hii njia ya upotevu alikuwa kama alikimbilia na unyenyekevu na utii ku Kanisa Orthodokse, kwa sababu marafiki na wasaidizi wake wote walihakikisha ya kama paka Kanisa Orthodokse inachunga mafundisho yote toka Mitume bila kuharibika. Rafiki yake mupendwa na musaidizi Filipo Melakthon, théologien mkubwa, alisema hivi juu ya kanisa Orthodokse *: „Mungu, kwa namna ya ajabu, anachunga Kanisa yake kubwa, na hii ni Kanisa Orthodokse, kule Grèce, katika Azia ndogo,* Thraki...sawa vile aliokoa wale vijana tatu ndani ya tanuru ile wakati wa mufalme Nebukadneza. Mu mwezi wa saba ya mwaka 1519, wakati alizungumuza na théolgien Eck wa Katholika ya Roma, Luther aliyechukia wa Waortodoksi ya kwamba weko wakosefu kwa imani kwa sababu walikataa ukubwa ya papa, katika maneno yake ingine alisema : *„Wakati Eck anasema ya kwamba umoja ya maaskofu mwanzo yake ni muji wa Roma, ninaitika na mimi, lakini kama tunasema juu ya Kanisa ya Mangaribi (ya Roma), tunapashwa kusema ya kama na hii Kanisa ya Roma ilitokea ku Kanisa ya Yerusalema iliyo Mama ya makanisa yote. Kwa hivi, ni kosa ya kusema ya kama umoja ya maaskofu wote mwanzo ni Kanisa ya Roma na ya kama hii Kanisa ya Roma ni mwanzo na mukubwa wa Makanisa yote. Kwa sababu, bila shaka, tunaweza kusema ya kama Yerusalema ni mama na mkubwa wa Makanisa yote...Kama waaminifu wa ulimwengu wote wanaitika ya kama askofu mkubwa wa Roma ao, kwa mufano wa Paris, ao wa muji ingine, ni wa kwanza na mkubwa kati ya maaskofu wengine wote, mimi sikatae kumufahamia na mimi, kama waaminifu wote wa dunia wanaitika na wanamufwata. Lakini hii mambo haionekane ndani ya Kanisa, wala zamani, wala leo, wala ku mbele, kwa sababu mpaka leo Kanisa Orthodokse haitike hii fundisho ya ukubwa wa papa wa Roma, bila kusema ya kama hii Kanisa orthodokse iko na kosa kwa imani“.*

Kwa sababu ya hii mafundisho na ya makosa yake wale watu walimufuata walianguka katika zambi yote, kwani mwalimu wao mukubwa Luther aliwaambia ya kama inaenea imani ya kuokolowa. Rafiki yake mumoja aliyeishi ile wakati anatuhakikisha ya kama ile wakati Allemagne " ilikuwa chini ya zambi zote, sawa kula mingi, kulewa, kupenda feza, uzini na usharati". Tena waaminifu wa Luther walizarau mafundisho na mashauri ya Evangelio ya Kristu. Tena na rafiki yake mwingine, Filipo Melakthon alisema : " *Tazameni sasa wafwasi wa Luther mutaona namuna walivyo washarati, walevi, wasiyo na heshima, na wapotevu!... Oneni hali ya jamaa zao.* Mutaona ya kama hawa watu wanaishi sawa wapagano, pasipo kumuogopa Mungu. Hata maji yote ya mutoni Elva haitaenea kulilia ile mateso na ile zambi ilileta „uadibisho" ya Luther".

Na kila siku Luther aliona ya kama upotevu ya watu ilikuwa mubaya sana. Watu walizarau amri za Mungu na walitenda zambi zote. Na Luther alisikia ya kama alikuwa mukosefu kwa Mungu kwa sababu kwa ajili yake watu walipoteza njia ya Mungu. Tena Luther aliona ya kama wale watu walimuchukiza na walimuzarau walikuwa na haki kwa sababu hii mafundisho yake alifundisha watu wanakuwa bila haya, bila heshima na bila kumwogopa Mungu. Wakati alitaka kuwafundisha waaminifu wake, wao walimujibu: *" Wewe haukutufundisha ya kwamba mutu hawezi kufanya tendo nzuri na hawezi kuokolewa sababu ya matendo yake mema?"* Kisha Luthrro akasirika. Wakati ingine alipiga mikono yake sawa mwenye mazimu na alisema na udanganyifu*: "Salamu, uzima ya usharati".* Tena alisema: *„Wanawake ya wanaume wa inchi ya Allemagne ni nguruwe wasipo na haya*"! Juu ya wanafunzi wake, alisema : *Hakuna namna ya kupata katikati ya vijna maelfu mbili ao tatu, hata wanafunzi mbili ao tatu wenye kumuogopa Mungu".* Juu ya watu ya mugini na muji alisema : *"Wanaanguka siku zote ndani ya zambi ya ulevi na zambi ya mwili".* Kwa hivi muji wake Bitembergi ilikuwa sawa Sodoma na Gomora juu ya zambi za watu. Martin Luther aliandika ya kwamba *: "watu wa hii muji weko sawa nyama, wivi, wanyanganyi, wapenda feza na wenye zambi ya usharati".*

Hii mambo yake iliharibisha na usingizi yake. Alipoteza amani roho mwake. Wakati ingine alianguka katika sikitiko mingi na wakati ingine alikuwa na kasirani. Kutoka mwaka 1520 alipoteza usingizi yake. Alibaki bila kulala usingizi siku ine ao tano, bila kutikisika pa kitanda chake sawa kufa. Muganga wake alijikaza kumurudishia amani na ukimya rohoni, lakini hakuna namna.

Ile kitu ilimuletea kabisa sikitiko kubwa ilikuwa hii mambo ya kama aliona matengano, makelele, na wafwasi wake walianguka kabisa mu zambi. Siku moja Melakthon alisemaka hivi : *"Walimu ngapi wataleta hii milele ya sasa! Fujo itafika ku mwisho. Hata mtu moja hapendi kufwata mwingine. Hapendi kufwata wazo yake ao kutii mamlaka yake. Kila mutu atapenda kuwa mwalimu na mkubwa*".Hii maneno yanatimizika hata sasa na yalikuwa sawa unabii.

Iko vile. Tangu ile wakati alihukumu Kanisa ya papa, alikataa kutafuta na kufwata musingi wa kanisa orthodokse, alijivuna, akafungula kanisa yake. Kwa hivi, na wasaidizi, na wafwasi wake walimufwata mwalimu yao. Nao walifungula makanisa yao. Nani kweli, ataweza kusimamisha majivuno na mapenzi yao ya kufungula kila mtu kanisa yake? Na iko kweli ya kwamba ile wakati aliishi Luther mwalimu yao, kulitokea walimu wengi ambao zamani walikuwa wafwasi na wanafunzi wake. Lakini, ku mwisho walimukataa, walimuzarau sawa mutu mukosefu na mwenye mazimu, na kila mumoja alisadiki paka mwili wake kuwa mwalimu wa kweli. Kwa hivi katikati ya makundi ya Waprotestants kulitokea funjo na matengano mengi. Wasaidizi wake wa zamani walimuzarau sasa mwalimu yao Luther na walimuita *„Mwalimu wa kiti, mwalimu wa bure, mwalimu muwongo, papa mupya ya Bitembergi, muzaifu na mwenye kushitaki".* Tena na huyu rafiki yeka mupendwa Filipo Melakthon alianza kuhukumu mafundisho mengi ya rafiki yake Luther. Mwalimu mumoja mkubwa, jina lake Karlail anasema : Mu mugini ya Luther Uadibisho yake iliharibika wepesi. Basi, haiko dini ya imani, lakini ni ya makelele juu ya mambo ya Mungu, neema ya Mungu haiingie ndani ya roho ya watu. Ni paka malalamiko na ndani ya hii malalamiko ni mawazo mbalimbali".

Mwanafunzi wa zamani wa Luther alikuwa mutu mumoja jina lake Thoma Minster. Huyu alikuwa mwongozi wa ile fujo ilianza kisha Uadibisho wa Luther. Luther alimuandikia barua. Sisi tunashangaa kwa hii maneno alimwandikia. Aliandika hivi *: "Mupigeni, muuweni, muchinjeni..."* Kwa mazungumuzo yake fulani alisema *: " Kama mtu mumoja ataweza kumupiga mwingine, kumuuwa na kumuchinja ao kwa siri ao kwa kuonekana, haifai kusahau ya kama hakuna kitu kinapita sumu ila kabisa mwenye kuletesha fujo ". Ni namna moja na ule mutu atapiga na atauwa imbwa moja; kama atamupiga, ya kwanza ataluma huyu alimupiga na ataluma dunia muzima".* Maneno haya ya Luther yanatuonyesha woga na fujo ya roho yake. Aliogopa ya kama hii uadibisho yake itaharabika, ndio vile alikuwa sawa mazimu sababu ya kisilani yake. Hii woga ya kuharibika kazi yake ilifukuza kumuogopa Mungu.

Luther alikuwa mugonjwa na huzuni mingi rohoni mwake wakati alianza kuandika juu ya kukombanisha papa na wasaidizi yake.Ile kitabu aliandika inatushangaza kwa ile matusi aliandika. Tena hii ugomvi yake ilizambalisha na kupiganisha walimu ya masomo. Juu ya walimu aliandika maneno haya *: " Walimu yao walikuwa wanguruwe ya uchafu, potopo ya kuoza, na uchafu ya gehena* "! Hakuweza kupata ukimya kwa mapatano na mazungumuzo na watu wengine wote, hata na bibi yake, wala rafiki zake, wala wale watu waliishi karibu naye. Kwa maneno ya rafiki yake Melakthon, *"Uzima ya Luther ilikuwa sawa kifungo moja kisichovumilia".*

Tena kwa kasirani yake ilimusukuma Luther na kukombanisha Waebrania ambao aliwaita *" wanyama weushi".* Ndani ya maneno yake ya mwisho alishauria Waturki wawafukuze Waebrania mbali ya majimbo yao. Na ule rafiki yake, alimusifu, jina lake Karlail., aliandika hivi: *" Ndani ya vitabu na matendo ya Luther munaingia kasirani ya milele, upofu, tamaa mingi Tunamutakia aondoshe tamaa hizi".*

Usiku ya tarehe 17 na 18 ya mwezi ya mbili ya mwaka 1546 ilimupiga magonjwa pa kichwa. Waganga walikwenda wepesi, lakini hakukukuwe namna ya kumutunza. Asubui, alikufa pa saa ya tatu. Maneno yake ya mwisho yalikuwa hii : "*Kwa maana Mungu alivyopenda ulimwengu, hata kutoa Mwana wake wa pekee, ili kila mutu akimwamini asipotee, lakini apate uzima wa milele" (Yoane 3,16).*

Luther alikuwa na zawadi mingi za Mungu. Alikuwa na haki juu ya kusimamisha makosa mengi na uzulumu wa Kanisa ya papa. Ndani ya vitabu vyake tunaweza kupata maneno yake mazuri Lakini juu ya majivuno na imani yake kwa mwili na akili yake, alianguka na alizama ndani ya potopoto ya mawazo mbaya na ya fujo ya roho yake. Alikombana mingi mu uzima yake kwa kukombanisha Kanisa ya papa, lakini ku mwisho alishindwa, moyo wake ilimuuma sana. Papa alimutosha na barua inje ya kanisa yake na Luther aliuliza mwili wake kila wakati : "*Roho yangu inashituka na ninauliza mwili wangu : Paka wewe uko na haki? Watu wengine wote ni wakosefu? Halafu, kama ni wewe ulikokota watu wengi mu imani ya kosa na uliwapeleka kwa uhukumu ya Mungu?"*

Wakati maulizo haya yalikuwa ndani ya mawazo yake, alitetemeka na alijikaza kwambia mwili wake ya kama yeye eko na haki.

Lakini vitu vyote vinatuonyesha ya kama yeye hakuwa na haki, kwa sababu alifwata mafundisho mengi ya uwongo. Ni lazima sisi kusema mara ya pili ya kwamba kulikuwa namna ya Luther kuwa mutu mkubwa kwa sababu alitaka kusimamisha makosa na zoezo mbaya ya mapadri na ya maaskofu wa Kanisa ya papa kama alirudi ku Kanisa Orthodoksi, kwani hii ni Kanisa ya kwanza na ya kweli. Matunda ya mashindano yake ya kukombanisha Kanisa ya papa ilikuwa ya kutenganisha watu katika makundi mengine mbalimbali. Hapa sasa makundi ya Waprotestants mu dunia nzima yanapita yulu ya 23.000. Kama Luther alirudi ku Kanisa ya kwanza, kulikuwa namna ya kutoa matendo makubwa duniani, kwa sababu kulikuwa namna ya kuunganisha watu chini ya muchungaji mumoja, Bwana Yesu Kristu, na ndani ya Kanisa moja, lakini majivuno yake, zambi zake na tamaa zake zingine yaliharabisha imani ya mataifa yote ya Ulaya na ya dunia muzima.

# MAFUNDISHO YA WAPROTESTANTS NA YA WAORTHODOKSE

## MAFUNDISHO YA KANISA

Waprotestants wanasema ya kama maana ya kanisa ni mukusanyiko, kundi ya watu wenye kumwaamini Kristu.

Sisi Waorthodoksi tunawajibu hivi: Kanisa haiko paka mukusanyiko, kundi ya watu wenye kufwata imani moja ya Kristu. Tena ni jamii kamilifu, na iko na Mitume, Maaskofu, Mapadri, mashemasi na waaminifu. Tena ni shirika kimungu na kimutu, Kichwa chake ni Bwana Yesu Kristu, na viungo vyake ni wale wanaamini mafundisho yake na wanabatizwa kwa Jina la Utatu Mutakatifu. Tazama anasema nini Mtume Paulo : " *Mujiangalie wenyewe, na kundi lote Roho Mtakatifu aliwaweka ninyi kuwa wasimamizi wao, kusudi mupate kulisha kanisa la Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe" (Matendo 20,28).* Cheo ya Upadirisho ikwako tangu ile wakati wa Mitume, lakini Waprotestants wanaikataa. Mtume Paulo mu barua yake kwa Wafilipi 1,1 anaandika *: "… na kwa wasimamizi wa kanisa na kwa wasaidizi ",* hawa ni wachungaji wa waaminifu. Mu Barua ya kwanza kwa Timotheo (3,2) anaandika namna gani mutu mumoja ataweza kuwa muchungaji wa waaminifu. Paka pa hii barua (5,22) na mu barua ya Tito 1,6 anasema kwa wanafunzi wake namna gani watachagua mapadri wapya na ya kama ni lazima kusopoka sana. *"Usiwekee mutu mikono kwa haraka, wala usishiriki kwa zambi za watu wengine"* Na kwa Tito anaandika: *"na kuweka wazee katika kila muji…"*Wazee ni mapadri. Sisi waorthodoksi tuko na cheo tatu tangu wakati ya Mitume na tunayatumia mpaka leo, kwani tuko kanisa ya kutengeneza mambo yake yote tangu mwanzo wake.

Makundi ya Waprotestants yalifanyika duniani mara ya kwanza mu mwaka 1520. Mbele ya hii tarehe, hakukukuwe Kanisa ya Kristu? Namna gani hawa watu wanasema ya kama wanafwata kanisa ya Kristu? Kama watasema ya kwamba kanisa ya kwanza ilipotea, sisi tunawauliza : Kuiko namna ya kupotea kanisa ya Kristu? Nikusema Roho Mtakatifu aliacha kanisa ya Kristu? Namna gani Kristu anawaambia Wanafunzi wake ya kama atawatumia Roho Mtakatifu na atabakia kwao milele? Tena, kama Kanisa ya Kristu iliharibika, namna gani Yesu alisema: *„Wewe ni Petro na juu ya mwamba huu (imani yake) nitajenga Kanisa langu; wala milango ya Hadeze haitalishinda" (Matayo 16,18).*

Kila kundi ya waprotestants linapenda kusadiki ya kwamba kanisa yao ni ya kweli na hakuna ingine. Lakini sisi tunawajibu ya kwamba Bwana Yesu Kristu tangu mwanzo aliacha kanisa paka moja tu na inabakia ya milele. Mtume Paulo anaandika kwa barua yake ya kwanza kwa Timotheo 3,15 : *" iliyo kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na musingi wa kweli".* Bwana Yesu analeta mafaa kubwa ku Kanisa yake, ndio maana anasema *: „naye, kama akikataa kuwasikia, ambia Kanisa; na kama akikataa kusikia kanisa vilevile, awe kwako kama mutu wa mataifa na mutoza kodi „* (Matayo 18,17). Nikusema, kama mutu mumoja anakataa kusikia neno la Kanisa sisi tunapashwa kumuacha, sawa vile Waebrania zamani walikimbia watoza kodi wakati walikutana nao.

Basi, Kanisa yetu iko na daraja tatu, hivi : Ni shirika na jamii ya Kristu, hakuna namna ya kuharibika, na ya tatu iko na mafundisho muzima ya kweli, bila kosa.

Waprotestants wanakataa kusikia ya kama Kanisa ya Kristu iko katikati yetu na inaonekana waziwazi. Wao wanasadiki ya kama kanisa ya Kristu iko mbinguni na isiyoonekana. Juu ya nini? Wanatwaambia ya kama hawawezi kuitikia Kanisa moja, lakini waaminifu wao ni watu wenye zambi na wauuwaji. Juu ya hii uwazo yao, jibu linatoka kwa Mtume Paulo (Waefeso 5,27) *"kanisa la utukufu, lisilo na alama ya uchafu wala kikunjo, wala kitu cho chote kama hivi, lakini liwe takatifu na pasipo kilema".* Kwa hivi Waprotestants wanasema ya kwamba kanisa

lisilo na uchafu na alama mbaya ni paka kanisa ya mbinguni na waaminifu wake paka Mungu anawajuwa na kule wanashindana juu ya kusikia muzuri bila kufwata kanisa fulani pa hii dunia.

Nikusema waprotestants wanatwaambia ya kama kanisa iko paka mbinguni, viungo vyake, maana waaminifu wake, ni watakatifu, hawana na alama ya uchafu na ya zambi, na watu wanaweza kufwata hii kanisa toka makanisa yoyote.

Sisi Waorthodoksi tunawaambia hivi : Wakati Bwana Yesu Kristu anapenda kuonyesha mapendo kwa wakristu wake anawaambia: *"Ambia kanisa"*. Hii maneno inatuonyesha nini? Hii maneno inatuonyesha ya kama ni kanisa ya kuonekana katikati yetu. Wakati Bwana Yesu aliwapa Mitume wake madaraja ya Upadirisho, ni sababu ya nini, sababu ya waaminifu waliyo mbinguni? Hapana, ni sababu ya kuwa wachungaji wa watu na wafwasi wa Kristu duniani : Sisi tuliyo na roho na mwili. Basi, wapi itakaa mwili yetu kama Kanisa ya Kristu iko paka mbinguni? Kanisa ya Kristu ni katikati yetu katika dunia yetu, na ndani yake muko waaminifu ambao wanakombana juu ya kushinda nguvu ya shetani. Kisha lufu wataingia mu Paradizo, pahali wanaishi Malaika na Watakatifu. Kwa hivi, Kanisa ya Kristu ni moja na vipande vyake ni mbili: Moja ni pa hii dunia na ingine mu Paradizo. Waaminifu wa ile kanisa ya mu hii dunia ni hawa walio na uzima, waaminifu wa ile kanisa ya mu Paradizo ni wale wamekwisha kufa na waliingia mu paradizo.

Waprotestants wanatwaambia ya kama hakuna namna ya kusadiki ya kwamba wataokolewa paka wale watu wanafwata Kanisa Orthodokse kwa sababu na wao ni wenye zambi na hawatubu.

Tunawajibu : Njia ya wokovu ni paka moja tu, Kanisa yake Kristu duniani iko katikati yetu. Lakini hawataokolewa wote wanaoingiamo, paka wale wanatubu kweli, lakini wale wasiyo kutubu wataenda mu gehena, sawa vile mulimanji anatupa mayani mbaya ndani ya moto. Lakini Mungu anatwaambia sisi tuwe na uzima kamilifu *: „Basi muwe wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mukamilifu“* (Matayo 5,48). Lakini, hakuna mutu aliye mukamilifu na asiye na zambi, ila tu Mungu peke yake, *" Tumutazame Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiliza imani yetu"* (Waebrania 12,2) na tutakombana juu ya kupata fazila za Kristu na toba ya kweli. Vile, polepole tutakuwa viungo safi na vya kweli vya Kanisa yake na wenye kustahili wokovu. Kama tuko tena watu wenye zambi, hii haiseme ya kama hatustahili kuishi katika kanisa, kwa sababu namna gani tutaokolewa na namuna gani tutatakaswa kama tuko inje na mbali ya Kanisa? Bwana Yesu alichunga kati ya wanafunzi wake mutoaji wake Yudasi pasipo kumufukuza. Alimuacha atoke yeye mwenyewe peke. Ni ajabu kama watu wenye zambi wanaamini mu kanisa? Yesu hakuja duniani kuwaita watu wenye zambi watubu? Kisha, watu wenye zambi kitu gani mbaya watafanya mu Kanisa ya Kristu? Wataweza na zambi zao kuharibisha utukufu na kazi ya kanisa ya Kristu? Hapana, hata kidogo.

Mifano ya Bwana Yesu, sawa ya magugu katikati ya ngano (Matayo 13,24), ya Makila (Matayo 13,47), ya ndoa ya mwana wa mufalme (Matayo 22,11), ya mabikira kumi (Matayo 25,1-14) yanatuonyesha ya kama katika Kanisa, inayoitwa Ufalme wa mbinguni munaishi na watu wenye zambi, hakuna namna ya Kristu kuwafukuza, kwani alikuja duniani juu yao. Kwa ile wakati wa mavuno, nikusema ya hukumu ya mwisho Mungu atawatenga waaminifu na wale wenye zambi, wasiyokutubu.

Waaminifu wenye zambi walikuwako tena na ile wakati wa Mtume Paulo.Kwa mufano, ku kanisa ya Korintho kulikuwa mutu mumoja alitenda zambi ya mwili na ndugu yake. (barua ya 1 Korinto 5,3-5). Mtume Paulo anasema : *"Kutolea shetani huyu mutu, ili mwili wake iharibiwe, hata roho yake iokolewe katika siku ya Bwana Yesu"*. Huyu mwaaminifu mukosefu aliishi katika Kanisa, hapana inje. Tena, Mtume Paulo anaachanisha wale wenye zambi na wale walio safi, wale wa kwanza watubu, lakini wataishi kidogo mbali ya wale walio safi. Kwa hivi, wale wenye zambi, haipashwe kuwafukuza, kwa sababu wakifukuzwa wanaweza kupoteza kitumaini yao kwa Mungu na watapotea, wataepuka ku mapashwa yao kwa Kristu juu ya kugeuza nia yao mbaya na kutubu katika mashauri ya padri yao wa roho.

Waprotestants wanatwaambia ya kama hakuna mambo kama katika Kanisa ya Kristu munaishi na wale wasiyo na imani, kwa sababu hawa watu hawataharibu misingi ya kanisa.

Sisi tunawaajibu hivi : Bwana Yesu anakataa sisi watu kuharibu ao kugeuza amri yake hata moja, kwa sababu atakuwa chini mu ufalme wa mbinguni. “*Basi mutu yoyote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kufundisha watu hivyo, ataitwa mudogo kabisa katika ufalme wa mbinguni…”(*Matayo 5,19*).* Tena Mtume Paulo anamushauria mwana wake wa roho Tito hivi: *“ Umwonye mutu muchonganizi mara ya kwanza na mara ya pili, asipokubali maonyo, umukatae. Kwa maana unajua mutu kama huyu ameacha njia ya kweli na zambi zake zinaonyesha kama yeye amejihukumu mwenyewe”* (Tito 3,10-11). Kwa hivi anafanya zambi hapana paka ule mwenye zambi ya mwili (Galatia 5,19-20) : *“Uasherati. Uchafu, uzini, kuabudu sanamu, ulozi, uadui, ugomvi, uwivu, hasira, fitina, faraka…”* Mtume Petro anasema mu barua yake : *“Lakini wanabii wa uwongo walisimama katikati ya watu, kama katikati yenu vilevile watakavyokuwa walimu wa uwongo watakoingiza mafundisho ya imani ya uwongo kwa siri, wakikana hata Bwana aliyewanunua, wakijileta wenyewe uharibifu usiokawia”* (2 Pet. 2,1-2). Kwa hivi, hakuna namna kuokolewa ule mutu anafwata imani ya uwongo hata kama eko mu Kanisa Orthodokse. Ni lazima tena kuwa na uzima safi na kufwata mafundisho ya kweli juu ya sisi kupata wokovu wa nafsi yetu.

Na sasa, leo kuiko namna kufupisha hii mafundisho ya leo : *“ Kanisa ya Kristu iko na matayarisho yake, itabakia ya milele tena ni fasi ya kuchunga mafundisho yote ya Kristu na ya Mitume wake. Kanisa ni paka moja tu, na vipande vyake ni mbili : moja ni mbinguni na ingine ni hapa duniani. Mu Kanisa ya Kristu, hakuna namna ya kuokolewa wale watu wanafwata mafundisho ya uwongo ao wanafanya zambi ya uzini na usharati. Kanisa ya Kristu iko sawa jamaa moja ya Waortodoksi, bila kutenga wakosefu. Tafauti yao itafanyika ile siku ya uhukumu ya Mwamzi Yesu Kristu. Kanisa na matayarisho haya ni paka Orthodokse, kwa sababu makundi ya waprotestants yalifanyika duniani mara ya kwanza* <u>*mu karne ya kumi na sita. ”*</u>

## MAFUNDISHO JUU YA MAANDIKO TAKATIFU

Kama tunasema Maandiko Takatifu tunawaza kundi moja ya Vitabu Vitakaitfu vilivyoanandikwa kwa maongozi ya Roho Mtakatifu katika wakati moja ya miaka 1500, nikusema toka Nabii Musa, 1400 miaka mbele ya kuzaliwa Kristu mpaka mwandishi wa mwisho wa Kitabu cha Ufunuo, nikusema miaka 100 kisha kuzaliwa kwa Kristu.

Waprotestants wanakubali paka Maandiko Takatifu. Wanakataa Mapokeo Takatifu, wanafafanusha paka mistari ya Maandiko Takatifu, kila mutu kwa akili yake. Ni ile fujo iko katikati yao, kwa sababu mafafanusho ya mistari ya Maandiko yanakuwa mingi, bila maana. Wanashangaa na wanatuuliza juu ya nini Kanisa yetu haiache kila mwaaminifu wake kufafanusha Maandiko Takatifu ya Mungu na kuyahubiri fasi yote. Sisi, waorthodoksi tunawajibu hivi: Kila mukristu anapashwa kusoma Maandiko Takatifu, lakini hana na uwezo ya kuyafafanusha. Kanisa yetu inaleta hii uwezo paka kwa mapadri na wathéologiens wake. Uwezo wa kufundisha watu iko kapa kwa maaskofu na mapadri na wathéologiens, hapana kila mwaaminifu, kwa sababu huyu eko pa fasi ya mwanafunzi na hapana pa fasi ya mwalimu (Matayo 28,20). Mtume Paulo anasema: *“Wote ni Mitume? Wote ni manabii? Wote ni walimu? Wote wanatenda matendo ya uwezo?* ( l Korinto 12,29). Walimu na wachungaji wanafundisha hii mafundisho Kanisa inachunga, hapana ile mafundisho inatoka kwa akili yao. Wanafundisha watu kwa jina la Kristu na la Kanisa yake.

Lakini Waprotestants wanasema ya kama kila mukristu“*anajua kufasiri Maandiko Takatifu“ (*1 Yoane 2,20 na 27*).*

Sisi tunawajibu ya kwamba Maandiko Takatifu inafanana na kisima kirefu. Huyu mutu anayesikia kiu hataingia ndani juu ya kunywa maji, lakini ataishota na beketi na kisha ataikunywa na kopo. Kama ataingia ndani ya kisima juu ya kunywa maji, atakufa. Ni vile iko mambo na ya

kusikia Maandiko Takatifu. Kila mutu hawezi kusikia na kufafanusha hekima ya Mungu. Karibu "*makanisa*" ingine misingi yao ni Mandiko Takatifu. Kwa maana wanafafanusha mistari ya Biblia na akili yao, ndio maana waongozi wao wanafungula "*makanisa*" mingi na wakuwa <u>sababu</u> ya kupotea kwa wokovu wa roho za watu wengi. Mutumishi wa Kandake, Malkia wa Ethiopia, wakati alimukaribia Mtume Filipo, alimujibu safi akasema : " *Nitayafahamu namna gani pasipo mutu kuniongoza?* (Matendo 8,31). Hii mustari ya 1 Yoane 2,20 na 27 : "*Munajua yote*" inatuonyesha ya kwamba kila kitu iko na Mupinga Kristu na wafwasi wake kwani juu yake kunaendelea maneno mengine kisha mistari ingine ya hii barua.

Maandiko Takatifu yanasikilika kwa namna tatu: 1. katika wazo la neno lake, nikusema maana ya inje. 2. Katika maana ya kiroho na ya ndani, wanaisikia paka wale watu weko na hekima ya Roho Mtakatifu. 3. Maneno ni ingine na maana yao ni ingine.

Waprotestants wengine wanasema ya kwamba Mungu anafunua mara mingi mafumbo ya mafundisho ya Maandiko kwa wenye akili, na anayafunua paka kwa watoto wadogo (Matayo 11,25).

Sisi tunawajibu: " Mungu anafunua mapenzi yake kwa wale weko watoto wadogo kwa roho na ubikira yao, hapana kwa wale weko na akili na mawazo sawa watoto wadogo. Mtume Paulo anawaambia waaminifu wa ku Korinto: " *Ndugu zangu, musiwe kama watoto kwa mafikiri; ila muwe kama watoto kwa maneno mbaya, lakini muwe watu wazima katika mafikiri yenu* (1 Kor. 14,20).

Waprotestants wanaendelea kusadiki ya kwamba paka kwa Kitabu kimoja watapata wokovu yao, lakini sisi tunawajibu na upole : " Mutu hakule kila siku paka chakula moja, *kwa hivi hawezi kusoma paka kitabu kimoja kila siku. Nyuki anazunguluka juu ya maua mengi sababu ya kubeba vitu vya kufanya navyo sali yake.* Na sisi kwa vitabu nyingi tunapata uzuri wa Neema takatifu. Roho Mtakatifu hakuangazie paka Waandishi wa Maandiko Takatifu, lakini anaendelea kuangaza Kanisa ya Kristu na waaminifu wake wenye kuishi rohoni mwao na mafundisho ya Kristu na wanaweza kuandika hii ufahamu yao sababu ya kusaidia wandugu wengine.

## <u>MAFUNDISHO JUU YA MAPOKEO TAKATIFU</u>

Kwa sisi waorthodoksi Mapokeo takatifu ni chemchem ya pili ya Ufunuo Takatifu na yanaheshimiwa pamoja na Maandiko Takatifu. Ni mafundisho muzima yenye kutoka kwa watu wa Mungu tangu milele yote ya Kanisa ya Mungu. Kipande chake kimoja kinaitwa Mandiko Takatifu.

Kutoka Adamu mpaka Abrahamu, kama walivyoandika Waandishi wa zamani, kulipita miaka 3678. Kama tutaongezako miaka 430 ile walikaa Wayuda mu Msiri, tunakuwa na miaka 4108. Katika hii wakati hakukukuwe wala Maandiko Takatifu, wala Sabato, lakini kulikuwa paka siku kubwa ya taifa la Waebrania. Hii wakati yote murefu watu wapenzi wa Mungu walifundishwa njia ya wokovu paka na Mapokeo Takatifu, nikusema hii mafundisho walisikia kwa kinywa cha watu wengine wa zamani. Ni paka tokea mwaka 1400, mbele ya Kristu, nikusema tokea nabii Musa mpaka kuja kwa Kristu duniani tuko na Kitabu cha Maandiko Takatifu (Agano la kale).

Huyu alitufundisha mafundisho ya Agano Jipya ku kinywa chake alikuwa Bwana Yesu Kristu. Katika miaka tatu na nusu alizambalisha na kinywa Habari yake Njema pasipo yeye kuandika hata kidogo wala kuwaambia wafwasi wake waandike. Aliwaambia paka waende duniani kuhubiri na kubatiza watu kwa jina la Utatu Mutakatifu. Tangu ile siku Kanisa yetu ilianza kazi yake. Kutoka siku ya Pentikosti mpaka ile siku iliandikwa Evangelio ya kwanza mafundisho ilihubiriwa paka na Mapokeo Takatifu na kinywa kwa kinywa. Kipande ψηake kidogo kiliandikwa kisha.

Waprotestants wanakataa Mapokeo Takatifu ya Kanisa, kwa sababu wanazani ya kwamba ni mafundisho na maneno tu ya watu wa bure. Tena wanaleta na hii mustari : *„Lakini wananiabudu bule, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya watu"* (Matayo 15,9). Sisi tunawajibu : Ku mustari ya Matayo 15,6 inaandikwa: *"Munazarau Neno la Mungu kuwa bule kwa sababu ya desturi zenu"*. Kwa hii mustari inaonekana ya kama mafundisho yao ni "maagizo ya watu". Na inapashwa kuyazarau, kwani iko mbali ya Mandiko Takatifu.

Kufwatana na mafundisho ya Kanisa yetu Mapokeo Takatifu ni ya mafaa pamoja na Maandiko Takatifu. Tazama kwa mufano : Mu Matayo 28,20 Bwana Yesu anawaambia Mitume yake ya kama "*atakuwa pamoja nao siku zote hata mwisho wa dunia*". Lakini, kisha miaka chache Mitume wake walikufa wote. Sasa Bwana Yesu atakuwa pamoja na watu gani hata mwisho wa dunia? Bila shaka anasema juu ya wafwasi wao. Ni wanani wafwasi hawa wa Mitume, ni sisi Waorthodoksi ao Waprotestants wenye walikuja duniani mu mwaka 1525? Ufwasi ya Mitume ilianza kisha uzima ya Mitume kwa maneno ya Bwana Yesu : "*Na tazama mimi ni pamoja nanyi siku zote hata mwisho wa dunia*". Haseme "*nitakuwa*", lakini *mimi ni* ( tangu sasa). Basi, ufwasi sawa hii paka Kanisa orthodokse iko nayo.

Mufano ingine : Sisi tunasadiki ya kama Maandiko Takatifu yaliandikwa na waandishi wale walijaa na mwangaza ya Roho Mtakatifu. Mtakatifu Paulo anasema: "*Kila andiko limepewa kwa maongozi ya Mungu..."* (2 Timotheo 3,16). Anasema kweli juu ya Agano la kale, kwa sababu ile wakati Mtume Paulo aliandika hii barua hakukukuwa vitabu vya Agano Jipya. Namna gani inaonyeshwa maongozi ya Agano Jipya? Mitume walionyesha mambo yote walisikia na waliona ile wakati walikuwa pamoja na Kristu. Ni vile tena anasema na Mtume Luka (10,16) "Yeye anayewasikia ninyi, ananisikia mimi…" Kwa hivi kila neno Mitume waliandika ni maneno na matendo ya Kristu, iliandikwa kwa mwangaza ya Mungu. Kati ya Waandishi watakatifu wa Agano Jipya kulikuwa wengine hawakuwa Mitume wa Kristu, lakini wanafunzi ya wafwasi wake, sawa Marko na Luka...Sisi tunawauliza Waprotestants : Vitabu vya Evangelio ya Marko na Luka viliandikwa kwa nuru ya Mungu ao hapana? Kama viliandikwa kwa nuru ya Mungu, namna gani watwaambie? Kama hapana, watwaambie sababu gani viliwekwa pamoja na Evangelia zingine? Nani aliziingiza ndani ya Evangelia zingine? Tena ulizo yetu ingine : Mt. Polikarpos, askofu wa muji Smirni ya Azia Kidogo na Mt. Ignati, askofu wa Antiokhia, walikuwa watoto wa roho wa Mtakatifu Mtume Yoane. Nao waliandika barua na vitabu. Juu ya nini vitabu vyao havikwingizwe katika kundi la Vitabu vya Agano Jipya, lakini Vitabu vya Evangelia ya Marko na Luka viliingizwa? Nani alifanya hii tafauti na alikubali vitabu vimoja na kukataa vingine?

Kwa sisi Waorthodoksi jibu ni paka moja yu : Ni Mapokeo Takatifu ilifanya hii kazi. Lakini, kwa sababu, Waprotesta wanakataa Mapokeo takatifu, wanasema nini? Nani alifanya hii kazi?

Mufano ingine : Bwana Yesu mu sala yake kwa Baba yake anaombea wakristu wote umoja na maneno haya : "*Ili wote wakae mumoja*.." Yoane 17,20). Sisi waorthodoksi na msaada wa Mapokeo Takatifu tuko na umoja katika kanisa moja, maana tunaungana. Kila mkristu orthodoksi hafafanushe na akili yake Maandiko takatifu na kuifundisha wengine kama anavyotaka na kufanya kundi lingine la waaminifu wake. Hii zoezo ya fungula "makanisa mengine" ni Waprotestants weko nayo, kwa sababu wanakataa Mapokeo Takatifu, hivi leo hawana mu umoja kwa imani moja sababu ya kutengeneza makundi yao. Hawasikie ya kama weko mbali ya hii sala ya Bwana Yesu ambaye anaombea umoja wa Wakristu katika kundi moja. Wao wanasadiki ya kama wanakubali paka Mandiko Takatifu (Biblia) na ni paka hii Kitabu wanatumia. Lakini wanadanganyika. Tazama mufano : Agano Jipya (ku kitabu cha Matendo 6,3) inasema juu ya mashemasi saba, Mtume Paulo (mu barua yake ya kwanza kwa Timotheo 5,9) anasema juu ya wajane (wanawake wasiyo na wanaume). Mu barua yake ya kwanza kwa Wakorinto 11,3 anasema wanawake wanapaswa kusali na kichwa yenye kufunika. Tena Yesu Kristu aliosha miguu ya wanafunzi wake na aliwaagiza wafanye hivi (Yoane 13,14). Hii mazoezo na matendo

yote Waprotestants wanaifwata? Hapana, ni kweli hawaifwate. Juu ya nini wanaikataa? Kwa sisi, tuko na Mapokeo Takatifu yaliyo chemchem ya ufunuo kimungu ya pili na haitupatie mazoezo haya.

Maandiko Takatifu hayandike hata pa fasi moja ya kama Siku ya Mungu itakuwa siku bila kazi na kubwa kwa Ufufuo wa Kristu. Waprotestants wanakubali sawa sisi hii siku ya Mungu. Juu ya nini, kwa sababu hayandikwe hata pa fasi moja ndani ya Maandiko Takatifu? Nani alitengeneza mambo ya hii Siku ya Mungu?

Yesu Kristu alituma Mitume wake duniani kote na aliwaambia kubatiza watu kwa Jina la Utatu Mtakatifu. Hakuwaambia namna gani watafanya Ubatizo. Ni Mapokeo Takatifu inatwaambia namuna ya kuingiza ule mtu atabatiziwa ndani ya maji mara tatu. Kwa ile mara ya kwanza padri atasema: *Mutumishi wa Mungu... (jina lake fulani) anabatizwa kwa "jina la Baba"*, atamuingiza mara ya pili atasema: *"Na la Mwana"*, kwa mara ya tatu, atasema: "*na la Roho Mtakatifu. Amina"*.

Maandiko Takatifu yanatwaambia ya kama Mwana na Baba yake ni pamoja. Hivi : *"Mimi na Baba yangu ni mumoja"* (Yoane 10,30). Lakini hii umoja yao inatuonyesha nini? Ya kwamba wote wa wili hawakuzaliwa? Hapana. Mapokeo Takatifu na Mkutano Ikumeniki ya Kwanza yanatwaambia ya kama hii umoja inaonekana kwa asili nyuso zao. Mu luga ya kigreki ni "Omousios".

Waprotestants katika mikutano na mahubiri yao wanatenda matendo yale haina ndani ya Maandiko Takatifu. Nikusema wanatumia sala na vitabu vyasipo kutoka katika Maandiko Takatifu. Kwa mufano, wanafunga macho yao wakati wanaposali, wanatumia kitabu cha Biblia na kukifasiri, lakini wanasema ya kama wanapaswa kusoma Biblia paka na mandiko yake ya zamani.

Ushuhuda ya Maandiko Takatifu juu ya Mapokeo Takatifu ni mingi. Tutaandika kidogo : *„Kuna maneno Yesu, nayo yakiandikwa moja moja, ninazania hata dunia yote haiwezi kutosha kwa vitabu mengine mengi aliyoyafanya vyote vitakavyoandikwa"* (Yoane 21,25*)*. Na pa fasi ingine: "Yoane 20,30) na barua ya 2 Yoane 12 na barua ya 3 Yoane 13-14.). Hii Maandiko waliandika Waevangelizaji haiko ndio matendo na maneno yote ya Kristu. Matendo na maneno yake mengi hawakuyandika katika Agano Jipya. Kila kitu isiyoandikwa mu Biblia ni Mapokeo Takatifu ya Kanisa yetu.

Zaidi Mtume Paulo anawaambia wakristu wake kuchunga yale Mapokeo na mafundisho yeye aliwafundisha. Aliwaambia hivi : *"Mutu ye yote akiiwahubiri ninyi Habari Njema ya mbalimbali na ile muliyopokea, alaaniwe"* (Wagalatia 1,9). Tazama, namna gani anawashauria waaminifu kuchunga Mapokeo na mafundisho yake:

1) *"basi, ndugu, simameni kwa nguvu, mushike mafundisho muliyofundishwa, ama kwa maneno, ama kwa barua yetu"* (2 Watesalonika 2,15)".

2) *"Tunawaagiza ninyi, ndugu, katika jina la Bwana wetu yesu Kristu, mujitenge na kila ndugu anayetembea pasipo utaratibu, wala si kwa kufuata mafundisho muliyopokea kwetu*" (2 Watesalonika 3,6).

3) *"Ninawasifu ninyi kwa sababu munanikumbuka mimi katika maneno yote, na munashika mafundisho kama nilivyowaletea ninyi"* (1 Korinto 11,2).

4. *"Na maneno yanayobaki, nitayatengenaza wakati nitakapokuja"* (1 Korinto 11,34).

5. *"kwa sababu kwanza niliwapashwa ninyi habari za maneno niliyopokea vilevile* (1 Korinto 15,3".

6. *"Na maneno yale uliyoyasikia kwangu kwa washuhuda wengi, maneno haya uwekee watu waaminifu watakaofaa kufundisha wengine vile"* (2 Timotheo 2,2).

Kwa hii mustari ya mwisho inaonekana amri ya Mtume Paulo juu ya kujitoa kwa watu wengine.

7. "*Na kuweka wazee (mapadri) katika kila muji, kama nilivyokuagiza*" ( Tito 1,5).

8. “*Fanyeni maneno muliyojifundisha na kuyapokea na kuyasikia na kuyaona ndani yangu, na Mungu wa salama atakuwa pamoja nanyi*” (Wafilipi 4,9).

9. “*Kama zilizoelezwa kwetu na wale waliokuwa tangu mwanzo washuhuda na watumishi wa Habari Njema*” (Luka 1,2).

11. “*Kwa sababu ya maneno haya angalieni mukikumbuka ya kama kwa kadiri ya miaka mitatu, usiku na muchana, sikuacha kuonya kila mutu kwa machozi*” (Matendo 20,31). Mtume Paulo aliwaambia nini katika miaka mitatu? Na mu kitabu gani aliyaandika? Hata pa fasi moja . Lakini yaliandikwa ndani ya roho za wale watu waliyasikia na walifundisha na watu wengine.

Namna gani mafundisho ya Mapokeo Takatifu ni ya kweli na yasiyo haribika?

1. Kama haikombanishwe na mafundisho mengine ya Mapokeo ya Mitume na ya Maandiko Takatifu.

2. Kama inatokea kwa Mwokozi ao kwa Mitume waliyoongozwa na Roho Mtakatifu.

3. Inapaswa kuichunga imara katika Kanisa ya Mitume mpaka leo.

4.Inapaswa kuijuwa na kuitimiza ku Kanisa Orthodokse yote.

5. Inapaswa kufwata mafundisho ya mapadri na ya Waandishi wa Kanisa.

Kama Mapokeo haifwata kanuni hakuna namna ya kuwa mafundisho ya kweli na takatifu na kuyafwata kweli kwa waaminifu.

Tena tuko na ushuhuda mingi ya Mapadri wa zamani ambao walikuwa wanafunzi ya Mitume. Mwandishi wa habari, askofu wa Kesaria, jina lake Efsebios anaandika ya kama askofu wa Roma, Klimis, mtoto wa roho wa Mitume alikuwa, mbele ya macho yake, na mahubiri ya Mitume na Mapokeo Takatifu. Mt. Ignatio Mubebaji-Mungu anasema katika barua zake kwa waaminfu wa Efeso na Filadelfia ya kama Wakristu wanapaswa kuwa mu umoja, wajitenge mbali ya mafundisho ya uwongo ya wakosefu wa imani, muchungaji ni paka huyu wanamufwata kwa waaminifu sawa kondoo.

Mtakatifu Irineos (+202, kisha kuzaliwa kwa Kristu) na Klimis, askofu wa Aleksandria +215) wanasema : “*Wale wanafafanusha Maandiko Takatifu, bila msaada wa Mapokeo ya Kanisa wanaharabisha maana ya mafundisho ya kweli*”. Mt. Epifanios, askofu wa Kipro, anaandika hivi : “ Inapaswa kuweka imara Mapokeo takatifu, kwa sababu hakuna namna ya kupata mafundisho yote ndani ya Maandiko Takatifu. Mitume wa Kristu waliandika mafundisho kidogo, lakini mafundisho ingine waliifundisha kwa kinywa. Mt. Grigori, askofu wa muji Nisa (+394) aliandika hivi : “ *Tuko na Mapokeo yenye kutoka kwa Mapadri sawa uriti na ufwasi wa Mitume na inasambalishwa kwa Watakatifu*”. Mtakatifu Basile Mkubwa (+379) aliandika hivi *: “Katika mafundisho haya ya Kanisa, mengine yanatoka ku Mapokeo ya Mitume na ufwasi ya siri kwa kinywa chao na mafundisho haya iko na uwezo na nguvu na mafundisho ile iliandikwa*”. Tena huyu Mpadri mukubwa anasema: “*Kama tutakataa Mapokeo yasiyoandikwa tukizani ya kwamba tumekwisha kuyazombelea na ya kama mafaa yao ni kidogo, hivi tunakosa na tunakataa Habari Njema“.*

Ku mwisho tunasema ya kwamba Chemchem ya Ufunuo takatifu ni yote mbili pamoja : Maandiko Takatifu na Mapokeo Takatifu, yote mbili iko na mafaa moja, na utukufu moja. Moja inafafanusha na kutimiza ingine. Kama tutakataa moja, mara moja tutaanguka mu mafundisho ya uwongo na tutapoteza wokovu wa nafsi zetu.

## MAFUNDISHO JUU YA FUMBO YA UBATIZO

Neno “Fumbo” linatuonyesha tendo takatifu la kushuka kwa Neema takatifu ndani ya alama yenye kuonekana. Kwa mufano, Ku Fumbo ya Ubatizo inashuka kitu kisichoonekana, ni Neema ya Mungu, na inaingia ndani ya maji iliyo kitu chenye kuonekana, halafu namna gani anatakaswa zambi zake huyu anayebatizwa , hakuna namna ya mutu kuisikia na akili yake.

Kanisa yetu iko na Mafumbo saba yenye kutupatia Neema Takatifu. Hii Mafumbo ni: Ubatizo, Krisma (Uzabitisho, maana kupakaa Manukato yenye kutayarishwa na maua makumi ine), Kuungama, Komunyo takatifu, Upadirisho, Ndoa na Mafuta Takatifu. Mafumbo ine ya kwanza yanapaswa kila mutu kuyatimiza, lakini yale ingine tatu ya mwisho yanatimizika kwa mapenzi ya mutu. Fumbo kubwa kabisa ni kuja kwa Bwana Yesu Kristu duniani, hii Fumbo haisikilike na akili ya kimutu wala haiandikwe. Tena Fumbo inaitajwa katika mafundisho ya Evangelio (Waefeso 3,3). Na imani, kwa neno la Mtume Paulo : "*Na pasipo shaka, siri (fumbo) ya utawa ni* kubwa" (1 Timotheo 3,16). Tena yanaitwa mafumbo : Ufufuo wa Mwokozi wetu, ufufuo wa wafu wote, Kuja kwa Bwana Yesu Kristu mara ya pili duniani na ingine. Lakini, kama tunasema juu ya mafumbo ya Kanisa, tunasikia Ibada takatifu zenye kutoka kwa Bwana wetu Yesu Kristu na zenye kutupatia zawadi za Roho Mtakatifu kwa faida ya Mwili wa Kristu, nikusema Kanisa yake.

Mu Kanisa yetu Orthodokse Ubatizo ni Fumbo ambayo mutu mwenye kubatiziwa anashuka na anapanda mara tatu katika maji ya Ubatizo kwa Jina la Utatu Mutakatifu na anatakaswa zambi ya asili ya wazazi wetu wa kwanza Adamu na Eva, tena anatakaswa na zambi zake alitenda mbele ya kubatizwa. Kwa msaada wa neema ya Mungu, roho na mwili ya ule mutu anaingia mu maisha mupya zinatakaswa na anakuwa kiungo cha Mwili wa Kristu na Kanisa yake.

Musingi yenye kuimarisha Fumbo ya Ubatizo tunaiona katika Maandiko Takatifu na inasema hivi : " Bwana Yesu wakati alizungumuza na mwanafunzi wake wa siri Nikodemo alimufundisha juu ya kuzaliwa mara ya pili sababu ya kuingia mu Ufalme wake mbinguni. Akamwaambia hivi : "*Kweli, kweli, ninakwambia, Mutu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia mu ufalme wa Mungu*" (Yoane 3,5). Tena, Bwana Yesu aliwaambia wanafunzi wake : "*Kwendeni katika dunia yote, mukahubiri Habari Njema kwa kila mutu. Anayeamini na kubatizwa ataokolewa; asiyeamini atahukumiwa*". (Marko 16,15-16). Hi amri ya Kristu kwa Wanafunzi wake inapatikana vilevile katika Evangeli ya Matayo (Matayo 28,19-20).

Waprotestants wanakataa hii Fumbo ya Ubatizo. Wanasema ya kama haileta Neema takatifu kwa ule mutu anayebatizwa. Wao wanasema ya kwamba ni ibada moja ya bure, ni paka matendo yenye kuonekana inamusaidia mtu kuingia katika kanisa ya mbingu isiyoonekana. Na wanasadiki tena ya kama hii fumbo ya ubatizo haisafishe zambi ya asili ya wazazi wa kwanza, hailete haitakase roho na mwili ya mutu, maana haimutakase mutu. Kwa ile ubatizo wanafanya waprotestants wanasema ya kwamba wamekwisha kuokolewa kwa sababu wamekwisha kumuamani Kristu, na hii imani inenea juu ya wokovu wao. Wale watu wao walibatiza wanakataa kubatiza watoto wao tangu utoto wao. Kama wataokolewa paka kwa ya imani yao, mafaa gani inawapa ubatizo yao? Nikusema juu ya nini wanabatiziwa kama wataokolewa paka kwa imani yao? Maandiko takatifu yanasema juu ya tendo la Ubatizo ya watu katika maji mara tatu, lakini Waprotestants wanafwata zoezo ya Katholika.ya Roma. Wanafanya ubatizo yao kwa kumimia maji pa kichwa. Juu ya nini? Wanatwaambia ya kama hakukukuwe namna ya kubatiza watu elfu tatu siku moja ndani ya maji ile siku ya Pentikosti (Matendo 2,4). Hii wazo yao haiko ya kweli, kwa sababu katika Yerusalema kulikuwa chemchem mingi ya maji, sawa : Birika ya Siloamu (Yoane 5,7), Birika ya Kondoo (Yoane 5,2) na ingine ingine. Tena, hata kama hakukukuwe wakati wa kuwabatiza wale watu wote ile siku ya Pentikosti, kulikuwa namna ya kuendelesha kuwabatiza na siku ingine. Mtume Filippo hakumumimia maji ule mkubwa wa kuchunga mali zote za Kandake, malkia wa Ethiopia, lakini alimubatiza. Tazama, alisema nini ule mkubwa: "*Tazama, maji; neno gani linalonizuiza nisibatizwe*? (Matendo 8,36-38).

Sisi tunawajibu hivi: Ubatizo haina alama na kitu ya bure, lakini ni tendo lenye kutuletea Neema takatifu. Ile siku ya Pentikosti Mutume Petro alisema mbele ya watu wote waliyoamini mahubiri yake ya kwanza : "*Tubuni mukabatizwe kila mumoja kwa jina lake Yesu Kristu, mupate ondoleo la zambi zenu, nanyi mutapokea zawadi ya Roho Mutakatifu*" (Matendo 2,38). Wale watu walimuuliza: "tutafanya nini?" Walikuwa na imani, lakini maondoleo ya zambi zao itakuja wakati

wa Ubatizo yao. Kwa hivi, imani peke yayo haienee kwa wokovu wetu kama wanavyosema Waprotestants.

Mufano ingine : Ku kitabu cha Matendo 19,1-5 tunaona ya kama wale walibatizwa kwa Mtangulizi Yoane ubatizo ya toba walibatizwa mara ya pili kwa Mtume Paulo. Mtume Paulo aliawauliza: "*Mulipokea Roho Mtakatifu wakati mulipoamini*? Wakajibu: "*Hapana, hatukusikia ya kama Roho Mutakatifu yuko* ". Akawauliza: " *Mulibatizwa kwa Ubatizo gani*?" Wakasema: *"Kwa ubatizo wa Yoane...*"Hapa inaonekana ya kama ni paka Roho Mutakatifu analeta Ubatizo ya kweli. Haiko alama, lakini ni namna ya kuleta Neema Takatifu mu uzima ya mutu. Tusome kitabu cha Matendo ya Mitume tutasikia mzuri kabisa mafaa ya Ubatizo (Matendo 10,44-48). Wasikilizi wa Mtume Petro walimuamini Kristu na Roho Mutakatifu aliwashukia. Lakini, hawakusema ya kama ni bure kubatiziwa.

Mufano ingine: Mtume Paulo mu barua yake kwa Wagalatia (3,27) anatwaambia: "*Ninyi wote muliobatizwa na kuingizwa katika Kristu, mumevaa Kristu"*. Kama ubatizo ni alama hapana kitu cha kweli, basi na mavazi ya Kristu itakuwa tendo la bure, ni alama. Lakini mavazi ya Kristu ni ya kweli na ubatizo haiko tendo moja la bure sawa alama. Namna gani tunajua ya kama mavazi ya Kristu kwa ubatizo ni ya kweli? Mu kitabu cha Matendo 6,3-4 Mtume Paulo anaandika: „*Sisi sote tuliobatizwa katika Yesu Kristu, tulibatizwa katika kufa kwake*. *Tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika kufa"*. Hapa hii neno*: „kwa njia ya ubatizo"* haiko tendo la alama, lakini ni la kweli. Kama vile Kristu alivyoingia kaburini na kutokamo muzima, vilevile na sisi tunaingia na kutoka ndani ya maji sawa tunazaliwa mara ya pili. Kwa hivi, Ubatizo inatujaza na neema Takatifu, inatutakasa zambi zetu zote na inatustahilisha sisi kuwa watoto wapenzi wa Mungu na tunaweza kupata zawadi zake zote.

Tena Mtume Paulo mu barua yake kwa Waefeso (5,26) anasema ya kama Kristu alisafisha Kanisa ake "*kwa maji katika neno*". Hii neno lake linatuonyesha Ubatizo, kwa sababu kwa hii ubatizo tunapokea mu uzima yetu Neema ya Mungu. Namna gani mutu atazaliwa mara ya pili kama Ubatizo hailete Neema takatifu na iko paka alama na kitu cha bure?

Tena tuko na ushuhuda yenye kutoka kwa waandishi watakatifu wa Kanisa yetu ambao walifunza na kwandika mafundisho ya Agano Jipya juu ya Ubatizo.

Mtakatifu Irineos, askofu wa Lugduno (leo ni muji Lyon katika inchi ya France, aliyezaliwa ku mwaka 140 kisha kuzaliwa kwa Kristu, anasema ya kama Ubatizo ni mulango ya kuzaliwa mutu katika roho. Mtakatifu Tertilianos, aliyezaliwa mu mwaka 155 anasema ya kama Ubatizo ni njia ya mutu kupata maondoleo ya zambi zake. Mtakatifu Grigori wa Nazianzi aliyezaliwa mu mwaka 329 anaandika hivi : " *Ubatizo ni utukufu wa roho, ni ya kushusha tamaa za mwili, inaleta neema ya Roho Mtakatifu, inaharibu nguvu ya zambi, inaleta nuru, inafukuza giza, inavunja minyororo ya zambi, ni njia ya kweli ya mutu kupata nuru na zawadi zote za Mungu"*. Mtakatifu Bazile kwa mahubiri yake moja anaandika hivi : " *Ubatizo ni ukombozi wa watumwa, ni maondoleo ya zambi, ni lufu ya zambi, ni kuzaliwa kupya kwa roho, ni mavazi ya kwangaa, ni tendo lisilofanyika na mikono ya mutu, ni gari ya kwenda mbinguni ku ufalme wa milele, ni zawadi ya mutu kuwa mtoto wa Mungu"*. Mt. Grigori wa Nisa anaandika hivi : "*Ubatizo ni kusafisha zambi, ni maondoleo ya makosa sababu ya mutu kuzaliwa na kutakasa roho yake*". Mt. Yoane Krisostome anaandika hivi : " *Kama mutu mumoja eko mwenye zambi kwa uzini, hata kama ni mupagano, hata kama alitenda maovu yote, kama ataingia ndani ya maji ya hii Fumbo ya Ubatizo, atatokamo mwenye kutakaswa, atakuwa safi kabgisa kupita mwangaza ya jua"*.

Tunazani ya kama hii mifano yote tunaleta hapa juu inaene kwa sisi wote na waprotestants kujuwa ya kama Ubatizo haiko tendo moja sawa alama, lakini ni mulango ya kweli ya mutu kuingia mu Paradizo kisha kutoka mu hii uzima.

# MAFUNDISHO JUU YA UBATIZO YA WATOTO

Waprotestants wanatwaambia ya kama mtoto kidogo hataweza kuamini na utoto wake, kwa hivi hapashwe kubatizwa.

Sisi waorthodoksi tunawajibu hivi : Bwana Yesu, ile wakati alihubiri duniani, alipokea watoto wadogo na aliwabariki. Aliwaambia makutano : *"Mwache watoto wadogo waje kwangu; musiwakataze, sababu ufalme wa Mungu ni wa watu walio kama wao "* (Luka 18,16). Kwa sababu Kristu aliwapenda kabisa watoto wadogo, hivi aliwabariki na aliwapa Neema ya Roho Mtakatifu, juu ya nini Kanisa yake itakataa kuwapa watoto wadogo Neema ya Ubatizo, kwa sababu kwa hii ubatizo wanapokea maondoleo ya zambi ya wazazi wa kwanza. Tena kisha ubatizo yao wataweza kupewa Mwili na Damu ya Kristu. Juu ya nini wataishi bila Neema ya Komunyo Takatifu?

Bwana Yesu Kristu, wakati alizungumuza na mwanafunzi wake wa siri Nikodemu alimwaambia hivi : "*Kweli, kweli ninakwambia, mutu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho Mtakatifu, hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu*" (Yoane 3,5). Hapa haseme paka juu ya watu wakubwa, lakini anasema juu ya kila mutu, nikusema wa kila umri. Ni kweli anasema na ya watoto wadogo, kama hawabatizwe hawataokolewa.

Mtume Paulo mu barua yake ya 1 Wakorinto 1,16 anaandika hivi : " *Vilevile nilibatiza watu wa nyumba ya Stefano…*" na ku Matendo 16,33 anasema : "*Akawakaribisha saa ile ile ya usiku, akawaosha mapigo yao, akabatizwa, yeye na wote wa nyumba yake. Kisha aliwalete nyumbani mwake, akawapa chakula, akafurahi sana yeye na nyumba yake yote, kwa sababu wamekwisha kuamini Mungu".* Sisi tunauliza : Katika hii nyumba wale watu walibatizwa, hamukukukuwe watoto wadogo? Ile wakati wa Agano la Kale, kwa amri ya Mungu, watoto wanaume wote, kisha siku mnane ya kuzaliwa kwa, walitarihiwa. Hii tendo lilikuwa alama ya Ubatizo, mu wakati wa Agano Jipya lilikombola kwa Tohara. Juu ya nini, basi, sasa mu wakati wa Agano Jipya haipashwe kubatiza watoto wadogo?

Ni kweli, watoto wadogo sababu ya umri yao hawasikie kitu kwa hii Fumbo. Lakini sisi tunauliza Waprotestants ambao wao ni watu wakubwa mu kipimo yao, wanasikia namna gani inatumika hii Fumbo ya maondoleo ya zambi zetu? Namna gani roho inazaa uzima yetu? Namna gani sisi tunapokea zawadi za Roho Mtakatifu? Watoto hawahukumiwe kwa sababu wanapokea Neema takatifu mu kipimo yao kidogo, lakini wanahukumiwa ni wale wanakataa hii Fumbo. Maandiko Takatifu hayaseme hivi? „*Anayeamini na kubatizwa ataokolewa*" (Marko 16,16). Neema takatifu haitakosa kumushukia mtoto kidogo sababu ya utoto wake.

Zambi ya wazazi wa kwanza inaingia kwa kila mtoto bila yeye kujuwa kitu. Haiko vile? Juu ya nini zambi ya asili inaondolewa paka kwa Ubatizo?

Pa hii mambo ya ubatizo ya watoto wadogo, sababu ya utoto yao, Kanisa yetu iliweka zoezo ya wasimamizi. Hawa ni mapadri wa roho ya wale watoto, wanahakikisha imani pa fasi ya watoto na wanawapokelea kisha Ubatizo yao juu ya kufwata uzima mupya katika Roho Mtakatifu. Maandiko Takatifu yanatwaambia waziwazi mambo ya hii zoezo tuko nayo : Bwana Yesu anasema : " *Lakini kama hasikii, chukua pamoja nawe tena mutu mumoja ao wawili ili kwa vinywa vya washuhuda wawili ao watatu kila neno lihakikishwe*" (Matayo 18,16 na 1 Timotheo 5,19). Tena Bwana Yesu alikamata mtoto mumoja pa mikono yake, alimusimamisha katikati ya wasikilizaji wake na alisema: „*Na kila mutu anayepokea mutoto mudogo mumoja kama huyu kwa jina langu ananipokea mimi" (Matayo 18,5).* Kwa hivi, ubatizo ya watoto wadogo inafanyika kwa imani ya wazazi na ya washuhuda kwa uwezo wa padri.

Waprotestants wanatuuliza: Imani ya Musimamizi inaweza kumuokoa mtoto?

Sisi tunawajibu: Ndiyo. Tazama hii ushuhuda : "Kwa imani yake ule Akida wa Waroma Bwana Yesu Kristu aliponyesha mutumishi wake. (Matayo 8,13). Watu ine walimuletea Kristu mtu mumoja mwenye kupooza :. " Wakaleta mutu mumoja mwenye kupooza aliyebebwa na watu wane....Yesu alipoona imani yao akamwaambia mutu mwenye kupooza : "*Mwana zambi zako*

*zinasamehewa"* (Marko 2,3-5). Basi, imani ya wale watu ine, hapana ya ule mugonjwa mwenye kupooza, ilimuponyesha katika mwili na roho. Tena Bwana Yesu sababu ya imani ya Yairo, aliponyesha binti yake (Matayo 9,18). Tena aliponyesha mugonjwa mumoja mwenye pepo muchafu na bubu mumoja (Matayo 9,32). Tena kwa imani ya ule mwanamuke Mukanana Bwana Yesu aliponyesha binti yake aliyeteswa na pepo muchafu. (Matayo 15,21). Kwa imani ya baba Bwana Yesu aliponyesha mtoto yake alikuwa na ugonjwa wa kifafa (Matayo 17,14). Mtume Paulo anasema : " Kwa sababu mume asiyeamini, anatakaswa na muke wake, na muke asiyeamini anatakaswa na mume wake: kama sivyo, kama watoto wenu wangekuwa si safi; lakini sasa ni watakatifu"(1 Wakorinto 7,14).

Waprotestante wanatwaambia: Juu ya nini Yesu Kristu alibatizwa mu kipimo yake miaka 30? Na sisi ahpaswe kubatizwa paka na hii kipimo Yake?

Sisi tunawajibu hivi: "Hii Ubatizo aliibeba Kristu ya Yoane ilikuwa ubatizo katika maji, lakini ubatizo ile inatokea ya imani kwa Yesu Kristu ni ubatizo katika maji na Roho Mtakatifu. Kristu asibatizwe juu ya kutubu na kusafishwa na zambi zake, kwa sababu alikuwa bila zambi. Lakini alifata hii desturi juu ya kutimiza sheria ya Waebrania (Matayo 3,14) na kwa kutupatia sisi mufano juu ya kubatiziwa na sisi kwa kusafisha ma tamaa na zambi zetu. Mt. Yoane Krisostomo anasema ya kama Yoane alimubatiza Kristu juu ya kumuonyesha duniani. "Tazama mwana-kondoo wa Mungu anayechukua zambi ya ulimwengu" (Yoane 1,29-30). Lakini na Mungu Baba alimuonyesha katika onekano ya Roho Mtakatifu, nikusema onekano ya Utatu Mtakatifu muzima.

Kristu haseme kwa umri gani tunapashwa kubatiziwa. Waprotestants wanaobatizwa hawabatizwe kwa umri wa miaka 30, lakini wanafwata mapenzi yao.

Katika Kanisa yetu Orthodokse Ubatizo inafanyika paka mara moja kwa Jina la Utatu Mutakatifu. Na Mtume Paulo anasema vile : *"Bwana mumoja, imani moja, ubatizo mumoja"* (Waefeso 4,5). Paka wale walibatizwa ku kanisa ingine isiyo na imani sisi tunawabatiza mara ingine. Katika makundi ya Waprotestants haikataziwe kubatiziwa mara mbili ao tatu, kwa sababu hawasadiki Fumbo Takatifu ya Kanisa yetu.

Watu wote weko na lazima ya Ubatizo juu ya kusafisha zambi zao zote. Lakini sikitiko mnene! Waprotestants milioni na milioni wanabaki bila kubatiziwa, hivi wanajiweka wao wenyewe inje ya Ufalme wa mbinguni.

Tena Waprotestants wanatwaambia ya kama watoto wadogo ni watakatifu na wanaweza kuokolewa bila kubatiziwa. Wanatwaambia maandiko ya Mtume Paulo: " *Kwa sababu mume asiyeamini, anatakaswa na muke wake, na muke asiyeamini anatakaswa na mume wake: kama sivyo, kama watoto wenu wangekuwa si safi; lakini sasa ni watakatifu"*(1 Wakorinto 7,14). Wao wanasema ya kwamba wazazi weko watakatifu, nikusema wamekwisha kubatizwa, hivi na watoto wao ni watakatifu. Sisi tunawajibu : Hii wazo yao haiko ya kweli, kwa sababu : " *kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho*" (Yoane 3,6). Kwa hivi, watoto wasiyobatizwa ni paka mwili, hapana roho, kwa sababu hawajazaliwa bado kwa maji na kwa Roho Mtakatifu. Kosa ya Wazazi wa kwanza iko kwa watu wote na inakuwa sawa ugonjwa katika vizazi vyote vya watu. " *Basi kwa njia ya mutu mumoja zambi iliingia katika dunia, na zambi hii ilileta mauti...*" (Waroma 5,12). Wale wanabatizwa kwa umri yote wanavaa kweli Kristu.

Watoto weko wenye zambi sawa vile watu wote walikuja duniani, na ni lazima kuwatakasa na Fumbo ya Ubatizo. Tazama ushuhuda ingine: " Yoane 3,6; Waroma 3,10; 1 Yoane 1,8; Isaya 48,8; Zaburi 50,5 na ingine.

## MAFUNDISHO YA KUPAKAA MARASI TAKATIFU (Khrisma)

Fumbo ya Khrisma ao Marasi Takatifu ni Ibada iliyotoka kwa Bwana Yesu Kristu. Kwa hii Fumbo padri anapakaa pa viungo malimbali vya mwili wa ule mutu alibatizwa na anasema hii sala: "*Alama ya zawadi ya Roho Mtakatifu. Amina*". Huyu anapakaliwa Marasi takatifu anaingia mu uzima wa Kristu na kwa hii Khrisma anapokea Neema kamili na kisha anatakaswa kwa Fumbo ya Komunyo Takatifu. Ubatizo inaondoa zambi, lakini Khrisma inazidisha zawadi takatifu juu ya kukaa imara katika uzima ya roho.

Waprotestants wanakataa Khrisma kuwa Fumbo takatifu, wala ibada ya neema. Wanaandika katika vitabu vyao ya kama "*hawana na ushuhuda wa hii Fumbo ndani ya Evangelio, wala mafundisho machache ya hii Fumbo".*

Sisi tunawajibu hivi : Mu Kitabu cha Matendo ya Mitume tunapata ushuhuda mbili pahali panaonekana ya kwamba kisha ubatizo Mitume walitmiza tena ibada ingine, Fumbo ingine takatifu, hivi mutu alipokea zawadi za Roho Mtakatifu. Mtume Luka anaandika hivi : "*Nao Mitume waliokuwa Yerusalema, wakatuma Petro na Yoane waende kwao. Wakashuka, wakawaombea wapokee Roho Mtakatifu. Kwa maana Roho Mtakatifu hajawashukia bado hata mumoja wao, wamebatizwa tu katika jina lake Bwana Yesu. Wakaweka mikono juu yao, nao wakapokea Roho Mutakatifu"* (Matendo 8,14-17). Pa hii mistari tunapata mafundisho ya kwamba ubatizo ni kitu kingine na kushuka kwa Roho Mutakatifu ni kitu kingine cha Mitume kuwekea *mikono pa vichwa vya wale walibatizwa. Tena ku Matendo 19,5-6) tunapata hii ushuhuda : "Waliposikia maneno haya wakabatizwa katika jina la Bwana Yesu. Na wakati Paulo alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mutakatifu akawashukia, wakaanza kusema kwa lugha nyingine na kutabiri*" . Na hapa tunaona mafumbo mbili mbalimbali : Ya Ubatizo na ya Khrisma. Mtume Paulo anatuhakikishia ya kama hii Fumbo ya krisma ilifwata Ubatizo. "*Wala musihuzunishe Roho Mutakatifu wa Mungu, ndani yake mulitiwa muhuri hata siku ya ukombozi*" (Waefeso 4,30).

Hii Fumbo, tangu wakati ya Mitume, ilikuwako na ilitimizwa kwa kupakaa marasi takatifu. Hii inatuonyesha ya kwamba Wakristu walikuwa wengi, lakini Mitume walikuwa kidogo na hakuna namna ya kuweka mikono yao juu ya kichwa cha kila mumoja wa wale watu wote walibatizwa sababu ya kupokea Roho Mutakatifu. Kwa hivi, Mitume walibariki hii Marasi Takatifu na kisha mapadri walitimiza hii Fumbo mu maparokia yao. Barua ya 2 Wakorinto 1,21-22 na barua ya 1 Yoane 2,20 na 27 wanatufundisha juu ya "Khrisma" na "ya kupakaa". Fundisho ya nguvu ndani ya hii mafundisho ni ya kwamma katika hii Fumbo Neema ya Roho Mutakatifu inatushukia, lakini tendo la kupakaa ni tendo la pili. Hii Fumbo ya Khrisma inatimizika paka mara moja tu kwa ule mutu anabatizwa. Tena inafanyika mara ya pili paka kwa wale watu walianguka kwa imani na kisha walipenda kurudia mu imani ya Kanisa ya Kristu.

Inje ya Maandiko Takatifu tuko na ushuhuda inatoka kwa Mapadri watakatifu wa Kanisa yetu. Sawa:

1. Mtakatifu Theofilo, askofu wa Antiokhia (169-180), anaandika hivi : „ *Kwa hii mambo na sisi tunaitwa Wakristu kwa sababu tunapakaliwa mafuta takatifu"*.

2. Mwandishi mkubwa wa Kanisa yetu, jina lake Tertilianos (155-240) anaandika hivi : "*Kama tunatoka mu maji ya Ubatizo, mara moja tunapakaliwa Khrisma kufwatana na desturi ya zamani. Khrisma inapakaliwa pa mwili yetu,….kisha padri anaipakaa na mukono yake pa kichwa, anaomba kwa Mungu na Roho Mutakatifu anashukia huyu anabatizwa"*.

3. Mukutano wa muji Kalkidona mwaka 258 ulikusanya askofu Mtakatifu Kiprianos na maaskofu wengine 84 ilikamata hii mpango : " *Inapashwa kupakaa marasi huyu mutu atabatizwa sababu ya kupokea Kristu. Wenye kukosa imani hawawezi kupakaliwa Marasi takatifu"*.

4. MtakatifuYoane Krizostome anasema: "Sisi wote tulistahiliwa kupakaliwa Khrisma na tulipewa Komunyo takatifu, tunapaswa kuchunga hii heshima na hii utukufu".

Ku mwisho tunaweza kusema ya kwamba Fumbo ya Khrisma inatoka kwa Mitume. Ku mwanzo ilifanyika kwa kuwekea mikono ya Mitume juu ya vichwa vya wale watu walibatizwa, kisha Mitume waliweka desturi ya kupakaa Marasi takatifu na mafuta takatifu yenye kutayarishwa na marasi makumi ine. Leo, Hii marasi inatayarishwa ku Patriarkha ya Konstantinopoli kila mangaribi ya mu Kazi tatu mkubwa ya Juma Takatifu na kisha wanaigawanya mu makanisa yote. Wanaitayarisha na marasi makumi ine yenye kuonyesha wingi wa zawadi za Roho Mtakatifu.

## MAFUNDISHO JUU YA FUMBO YA KOMUNYO TAKATIFU

Ushukuru kimungu ao Komunyo Takatifu ni Fumbo ambayo kwa uwezo wa Roho Mutakatifu mukate na vinyo tunayomutolea Mungu inageuka kuwa Mwili na Damu ya Bwana Yesu Kristu kwa uzima wa milele.

Waprotestants wanakataa neema ya Mungu katika hii Fumbo na wanasema ya kwamba haiko Fumbo, ni paka mufano, ni makumbusho ya Karamu ya Siri ile alifanya Kristu mangaribi ya mu Kazi ine kubwa. Sisi tunawaambia hivi hawa Waprotestants : " Sisi tunapatana kwa siri na Bwana Yesu Kristu mwenye kukaa kwa imani yetu ndani ya roho yetu. Kwa hivi, Fumbo ya Komunyo takatifu ni ya lazima sana. Kwa mawazo yao, wanakataa mafumbo ya Bwana Yesu Kristu.

Sisi Waorthodoksi tunawajibu hivi : Komunyo Takatifu haiko mufano, lakini ni sadaka ya kweli damu. Hii Sadaka ilifanyika mara ya kwanza juu ya Musalaba kwa ajili ya wokovu Wa watu. Hii sadaka inafanyika mara ingine ku Meza Takatifu ya Kanisa Orthodokse wakati inafanyika Fumbo ya Komunyo. Bwana Yesu anatwaambia mara mbili juu ya hii Fumbo. Anatwaambia ya kama hii Fumbo inasaidia wakristu kwa wokovu wao. Tazama hii mustari : *"Kweli, kweli ninawaambia ninyi, kama hamukuli mwili wa Mwana wa watu, na kunywa damu yake, hamuna uzima ndani yenu. Yeye anayekula mwili wangu, na kunywa damu yangu ana uzima wa milele ;…kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli, na damu yangu ni kinywaji cha kweli. Yeye mwenye kula mwili wangu na kunywa damu yangu anakaa ndani yangu na mimi ndani yake* ».(Yoane 6,53-57).

Hapa tunaona ya kama Bwana Yesu anatuonyesha mara ingine juu ya Mwili na Damu yake. Waprotestants wengi kama wanassoma hii mustari «*änayekula mwili wangu*» wanaifafanusha hivi ya kama *"wanapatana na Kristu katika kiroho na hivi weko na uzima wa milele"*. kama hawakule mwili wake na hawakunywe damu yake, hawatapatana na Kristu na hawakuwa na uzima wa milele.

Sisi tunawajibu : «Kama Bwana Yesu alipenda kuwafundisha wasikilizi wake juu ya mapatano katika roho, juu ya nini Wanafunzi wake wengine walikimbia wakisema : *« Neno hili ni gumu, nani anayeweza kulisikia ?* (Yoane 6,60). Wayuda walishangaa kwa hii maneno ya Kristu na wakaanza kubishana sana kati yao, wakisema : *« Namuna gani mutu huyu anaweza kutupa sisi mwili wake tuule ?* (Yoane 6,52), lakini Yesu Kristu aliwakikisha bila shaka ya kama wanakataa kula Mwili wake na kunywa damu yake hawatapata uzima wa milele. Wanafunzi wake wengi « *wakarudi nyuma, wala hawakutembea tena pamoja naye* » (Yoane 6,66). Akawaambia kama wanataka kwenda waende (Mustari 67). Hii mufano ya Kristu inatuonyesha ya kama hawafundishe kwa siri, lakini anawaambia waziwazi ya kwamba kweli huu ni Mwili wake na hii ni Damu yake.

Mara ya pili Bwana Yesu alitoa Mwili wake na Damu yake ku Karamu ya Siri mu Kazi Ine kubwa. Aliwaambia Wanafunzi wake : " *Twaeni mule ; huu ni mwili wangu…Kunyweni, ninyi wote, kwa maana hii ni damu yangu ya Agano inayomwangika kwa ajili ya wengi kwa maondoleo ya zambi* "(Matayo 26, 26-27). Hapa tunaona anasema juu ya sadaka, hakuna kitu cha alama, kwani ku mwisho anasema : " *kwa maondoleo ya zambi* ". Tena kuna tafauti safi kati ya mwili wake na damu yake.

Waprotestants wanaleta hii mistari : Luka 22,19 na 1 Wakoronto 11,24 na wanasema ya kama Karamu ya Siri ilikuwa Karamu ya makumbusho katikati yao, ilikuwa meza ya urafiki.

Sisi tunawajibu : Yesu Kristu hakusema : Kuleni kwa sababu ni mufano ya Mwili wangu, lakini alisema : «*Twaeni mule ; huu ni mwili wangu* » na "*hii ni damu yangu* »(Luka 22,19). Sasa tuangalie hii mustari ya pili ya Luka. Bwana anasema : *Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu inayomwangika kwa ajili yenu »(Luka 22,20).* Haseme << hii Kikombe ni ukumbusho wa Agano Jipya...>> Hapa anasema safi ya kama Hii iliyo ndani ya Kikombe ni Damu yake. Pa mustari 19 haseme hii ni mufamo wa mwili wangu, lakini ni mwili wangu. Tena anatwaambia sababu gani Yeye Kristu anatupatia mwili wake na damu yake « *Inayomwangika kwa ajili yenu »,* na Mtakatifu Matayo anasema *: « kwa maondoleo ya zambi »* (26,27). Kisha Luka anasema : "*Fanyeni hivi kwa kunikumbuka* "(22,19). Hii maneno inasikitisha Waprotestants. Wanaitosha pa ile fasi yake na wanasema, munaona? Karamu ya Siri ni ibada ya ukumbusho. Lakini sisi tunawajibu hivi : Komunyo Takatifu ni sadaka ya kweli, kwa sababu Kristu yeye mwenyewe anasema ya kama huu ni Mwili wake na hii ni Damu yake. Tena ni ya makumbusho kwa sababu ni mukate na vinyo na kwa ajili ya vile vitu tunakumbuka sisi Sadaka ya kule Kalvario iliyofanyika paka mara moja tu. Pa meza ya mahekalu Orthodokse inatolewa hii sadaka pasipo damu lakini na mukate na vinyo na itaendelea kutolewa hivi mpaka atapokuja Yesu Kristu mara ya pili duniani. (Luka 22,19 na 1 Wakoro\into 11,25).

Katika Maandiko matakatifu tuko na mistari inasema juu ya sadaka na zabihu ya wakristu. Mtume Paulo mu barua yake kwa Waebrania (13,10) anasema : " *Tuna mazabahu, nao wanaotumikia katika hema hawana ruhusa kula vitu vyake"* Kwa sababu tuko na zabihu, inapaswa kuwa na mapadri na sadaka. Waprotestants wanakataa na wanasema ya kwamba zabihu haina Meza takatifu ya kanisa, lakini ni Kalvario. Tena hii neno: *kula vitu vyake*" maana yake haiko kula, lakini ni kuamini. Kama tutaitika hii ufafanusho ya waprotestants tunapaswa kusema hivi : Maana ya zabihu, katika akili yao, ni Kalvario. Kula maana yake ni kuamini, na wale wanaotumika katika hema ni Waisraeli. Kwa hivi, maana ya hii maneno yote ni hii : "Tuko na Kalvario, lakini haiko haki ya Waisraeli kuamini! Ni kweli, Kristu hakupokea Waisraeli kwa imani? Mtume Paulo alikuwa muisraeli na alifanyika kuwa mukristu.

Kwa maana na barua ya Mtume Paulo (Waebrania 10,12-14) waprotestants wanasema ya kama sadaka alitoa Kristu ilikuwa mbili, ile muko nayo ninyi, nikusema moja pa Kalvario na moja pa Meza Takatifu. Sisi tunawajibu hivi : Sadaka pa Kalvario na pa meza takatifu ni paka moja tu. Ilianza ku Kalvario na inaendelea ku Meza Takatifu. Ni paka moja tu. Nikusema Kristu peke yake anajitoa na ku Kalvario na ku Meza Takatifu, lakini sadaka ya kwanza ilikuwa ya kumwanga damu, ile ya ku meza takatifu ni yasipokumwanga damu. Ile sadaka ya ku Kalvario ni toleo ya watu wote, lakini ile ya Meza takatifu ni ya wale watu wanaitaka. Sadaka ya ku Meza takatifu inatokea ku sadaka ya ku Kalvario. Sadaka ya ku meza ya makanisa yetu ni sadaka ya kweli ya ku kalvario. Kwa sababu inaonekana mukate na vinyo. Tena ni Mwili kweli na Damu kweli ya Kristu, hivi alitwaambia Bwana Yesu Kristu..

Mkubwa ya Waprotestents, Martin Luther, hakusadiki ya kama katika hii Fumbo kunafanyika muujiza mumoja. Alikataa ya kwamba mukate na vinyo yanageuka kwa uwezo wa Roho Mtakatifu kuwa Mwili na Damu ya Kristu. Wale waliandika uzima yake waliandika ya kwamba mazungumuzo juu ya hii Fumbo yalimusikitisha sana, kwa sababu hakusadiki. Hivi afya ya misipa yake iliharibika, na polepole alikufa.

Leo, Waprotestants wenye kuchunga hii Fumbo sawa mufano wanajivuna bure kwa sababu hawana na Meza takatifu, wala chetezo na ubani, wala Ibada, wala manguo Takatifu, wala Fumbo ya kuungama, wala kitu kingine kitakatifu sawa vile sisi waorthodoksi tuko nayo. Wanaendelea kusadiki ya kama paka kama watakula mukate na kunywa vinyo watapokea Roho Mtakatifu. Tunawauliza, kuiko namna paka na mukate na vinyo mutu mumoja anaweza kupatana na kuwa mu umoja pamoja na Kristu ?

Tangu zamani Mapokeo yetu takatifu inatufundisha mafundisho mengi juu ya hii Fumbo. Mtakatifu Ignatio, askofu wa Antiokhia, aliyeishi ku mwaka 107 kisha kuzaliwa kwa Kristu aliandika hivi ndani ya barua yake moja kwa wakristu wa muji Smirni ya Azia Kidogo : « *Wale wakosefu wa imani, jina lao Dokite, wanaepuka hii Fumbo ya Komunyo, kwa maana wanakataa kuamini ya kama hii mukate ni mwili wa Mwokozi wetu aliyeteswa kwa ajili ya wokovu wetu…*

« Mtakatifu Yustino, aliyezaliwa ku mwaka 100, anaandika hivi : « Tunatoa kwa jina lake ile sadaka Yesu Kristu aliamuru tufanye kwa Karamu ya Siri katika mwili na vinyo.

Mtakatifu Kirilli, askofu wa Yerusalema, aliyezaliwa mu mwaka 312 kisha kuzaliwa kwa Kristu, anaandika hivi : *« ni mukate, lakini haiko mukate, hata vile tunaisikia ndani ya kinywa chetu, lakini ni Mwili wa Kristu; na hii inaonekana sawa vinyo, hata kama ndani ya kinywa chetu iko hivi, ni Hii inaonekana damu ya Kristu »*.

Mtakatifu Basile katika Liturgia yake anaandika hivi : *" Zawadi hii tunakutolea sawa mukate ni mwili wa Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu; na Kikombe hiki ni Damu ya Bwana Mungu na Mwokozi wetu »*

Mtakatifu. Yoane Krisostome anandika hivi ndani ya Liturgia yake : « Fanya hii mukate kuwa mwili samani wa Kristu wako na hii vinyo ya kikombe uifanye kuwa damu ya Kristu wako kwa ushirika wa Roho wako Mutakatifu ».

Kwa hivi, tangu mwanzo mpaka karne ya tano Maandiko takatifu na Mapokeo takatifu yanatuonyesha juu ya hii Fumbo ya Komonyo.

Waprotestants wanatuuliza : Namna gani padri yeye ni mwenye zambi ataweza kufanya hii muujiza ya kugeuza mukate na vinyo kuwa mwili na damu ya Kristu ?

Sisi tunawajibu hivi : « padri eko mwenye zambi sawa watu wote, lakini haiko padri anafanya hii muujiza. Yeye anamuomba Mungu na Mungu anatuma Roho wake Mtakatifu. Paka yeye eko na hii zawadi ya upadirisho tangu ile siku askofu alimupa hii cheo na anaweza kutimiza hii tendo takatifu na mafumbo mengine yote ya Kanisa yetu.

Kwa sisi kusaidia waaminifu wetu juu ya kukaribia ku Kikombe takatifu juu ya kupokea Mwili na Damu ya Kristu, wanapaswa kutayarisha roho zao kwa hivi :

1. Kuungama zambi zote. Bila kuungama hakuna namna kwa mwaminifu mumoja kupokea Komunyo. Paka watoto mpaka umri wa miaka saba wataweza kukomunika bila kuungama.
2. Kuwa mu umoja na watu wote. Kama kuiko makokotano kati yao watapatana kwa haraka, kwa maana bila mapendo Komunyo takatifu ni moto ya kuunguza roho, hapana moto ya zambi zetu.
3. Kuepuka zambi zote, kabisa ya zambi za mwili, kwa sababu tamaa za mwili zinaharibu na mwili na roho ya mutu. Tena ni lazima kuchunga chakula na kinywaji.
4. Tena ule mwaminifu atakomunika atasoma tangu jana ao asubui sala ya Komunyo takatifu. Ao anapaswa kukumbuka zambi zake na ataanza kulia na kutubu.

## MAFUNDISHO YA KUTUBU (KUUNGAMA)

Kutubu ao Kuungama ni Fumbo moja takatifu. Kwa hii, Mungu anasamehe zambi za mkristu. Katika padri zambi za wale wakristu wanatubu kweli na kuungama mbele yake zinasamehewa.

Katika mafundisho ya Mtakatifu Yoane Damaskinos, kutubu ni kurudi kwa mtu toka zambi kwenda mu uzima ya Mungu, kwacha shetani na kwenda mu uzima ya roho.

Fumbo ya Kutubu iko na vipande ine :

1.Kutubu.

2.Kumwambia padri wa roho mawazo na zambi zote zilitendeka.

3. Kutimiza ile malipizi mpadri atamupa mukristu.
4. Kusamehewa zambi zake.

Padri mumoja hawezi kusamehe zambi za mukristu pembeni ya padri wake wa roho

Waprotestants wanakataa hii maungamo na toba kuwa Fumbo takatifu. Wanasema kama vile watu wanasema mumoja kwa mwingine mambo yao, na makosa na zambi zao, na kama wanajuwa ya kama walifanya kosa, wanaombana huruma kati yao na hivi wanasikilizana. Ni vile na mu uzima yao katika Kristu, kama wanasikia uzito ndani ya roho yao wanaomba huruma kwa Mungu na wanaipokea bila kuwa katikati yao mtu mwingine, maana padri. Wanasema ya kama Kuungama na kutubu yaliwekwa duniani mu karne ya tano.

Tena Waprotestants wanasema hivi : " Kanisa haijuwe maungamo ingine juu ya maondoleo ya zambi, paka ile inafanyika kwa Mungu, kama tunataja zambi zetu mbele yake. Kwa hivi, tunapaswa kuungama paka kwake, kwa sababu ni Yeye peke yake anayeweza kusamahe zambi. Hii maungamo inaweza kufanyika kwa siri mbele ya Mungu ao mbele ya waaminifu wengine. Wanaongeza wakisema : tena mwaminifu anaweza kuungama hata mbele ya pasteur yake mkubwa ao mbele ya mukristu mwingine, lakini maungamo mbele ya waaminifu wengi ni kwa mapenzi ya ule mutu mwenye kuungama.

Na kwa hii mafundisho waprotestants walianguka inje ya kanisa kwa kujikaza kwao sababu ya kukombanisha makosa ya Kanisa ya pape na zaidi mafundisho yake ya Kartasi ya kusamehe zambi za watu. Ni kwa hivi Waprotestants walifika kwa kukataa Fumbo ya kuungama, bila kutafuta hii mafundisho ilikuwa ndani ya Agano Jipya. Tena wanakataa hii Fumbo, kwa sababu wanakataa unyenyekevu. Ni kweli, hakuna unyenyekevu kwa watu wenye kukosa imani.

Waprotestants wanasema ya kama si lazima kuungama, kwani, wanasema wao weko karibu ya Kristu na hawatende zambi. Wanaleta mistari hizi : " *Kila mutu anayekaa ndani yake hatendi zambi*" ( 1 Yoane 3,6) Mu mustari wa 9 wa hii barua Mwandishi Yoane nasema : „*Kila mutu aliyezaliwa na Mungu hatendi zambi......wala hawezi kutenda zambi*". Pa fasi ingine *(*5,18) ya hii barua anasema Mtakatifu Yoane anasema : „*Tunajua ya kuwa kila mutu aliyezaliwa na Mungu hatendi zambi...*"nikusema huyu anayezaliwa na anabaki karibu ya Kristu asifanye zambi.

Sisi tunajibu Waprotestans hivi : Maandiko takatifu fasi mingi mbalimbali yanasema ya kwamba sisi wote tuko watu wenye zambi na kila siku tunamukosea Mungu. Mtume Yakobo mu barua yake ( Yakobo 3,1) anasema: „*Ndugu zangu musiwe walimu wengi, mukijua ya kuwa tutapata hukumu kubwa zaidi. Maana tunajikwaa sisi sote pia katika mambo mengi*". Katika ile sala Bwana Yesu alitupatia anasema : „*Utusamehe deni zetu kama sisi vilevile tunawasamehe walio na deni zetu…*". Mwenye deni ni huyu mwenye zambi, na deni ni zambi zake. Tena Mwevangelizaji Yoane mu barua yake ya kwanza (1 Yoane 1,8) anaandika hivi *:* „*Kama tukisema kwamba hatuna zambi, tunajidanganya sisi wenyewe, wala kweli si ndani yetu. Tukikiri zambi zetu yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee zambi zetu na kusafisha na uzalimu wote. Kama tukisema kwamba hatukutenda zambi, tunamufanya yeye kuwa muwongo, wala neno lake si ndani yetu. Watoto wangu wadogo, ninawaandikia ninyi maneno haya ili musitende zambi. Na kama mutu akitenda zambi tuna Mwombezi kwa Baba Yesu Kristu mwenye haki".*

Waprotestantees wanatuuliza : Namna gani inafafanushwa mustari ya barua ya kwanza ya Yoane ( 1Yoane 5,18) ya kwamba : " *Kila mutu aliyezaliwa na Mungu hatendi zambi*?...Sisi tunawajibu hivi: Tunaitika hii mistari ya juu ya kwamba sisi tuko wenye zambi na siku zote tunakosa, hata uzima yetu ni paka ya siku moja duniani. Lakini tutasema tena na hii neno : na wale watu weko kweli watoto wa Mungu weko na zambi, lakini wanafanya zambi kidogo, halafu wengine walio viungo vya kanisa ya Kristu, na wao ni watu wa kufa katika uzima yao wa kiroho wanafanya zambi bila haya na heshima. Wale wa kwanza wanakosa kwa sababu nguvu ya roho yao ni kidogo, lakini wale wa pili wanakosa kwa sababui ya tamaa mbaya. Mu mustari ya barua ya kwanza ya (1 Yoane 2,1) inasema hivi : " *Na kama mutu akitenda zambi tuna Mwombezi kwa Baba, ni Yesu Kristu mwenye haki*", anasikia wale watu wanakosa kidogo sababu ya nguvu yao

kidogo. Nikusema hawatendi zambi ya kuendelea. Lakini, wakati Yoane anasema *: Kila mutu aliyezaliwa na Mungu hatendi zambi...“*anasikia ya kama hafanye zambi ya kuendelea. Kama tutakubali ya kama hafanye zambi hata kidogo, tunakombanisha mustari ya barua ya kwanza (1 Yoane 5,18).

Waprotestants wanazania ya kama hakuna habari katika Maandiko takatifu juu ya hii Fumbo ya Kuungama. Kwa hivi, wanasema ya kwamba inaenea kupatana na Mungu katika sala na mazungumuzo waaminifu wengine.

Sisi tunawajibu hivi : Kristu anaweza kutusamehe hata kama tunakimbilia mara moja kwake, lakini, ni Yeye alituamuru kwa namna ingine, katika mapenzi yake, kutupa sisi usamehe wa zambi zetu. Tazama anatwaambia nini : “ *Mupokee Roho Mutakatifu, wo wote mukiwasamehe zambi, zinasamehewa kwao, na wo wote mukiwafungia zambi, zinafungwa kwao*” (Yoane 20,22-23). Na mbele ya kusulubiwa kwake paka na hii maana anasema maneno haya : “ *Kweli ninawaambia ninyi, vitu vyo vyote munavyofunga duniani vitafungwa mbinguni; na vitu vyo vyote munavyofungua duniani vitafunguliwa mbinguni“* (Matayo 18,18). Hii mistari yanatwaambia ya kama Bwana Yesu aliwapa Mitume wake na wafwasi wao uwezo wa kusamehe zambi za wale watu watatubu kweli. Basi, kila mwenye zambi anayesikia uzito wa zambi zake na anataka ziondolewe anapashwa kutii hii amri ya Kristu. Ni majivuno na uzarau kubwa kama sisi tunapenda kutafuta namna ingine ya usamahe wa zambi zetu, hivi tunazarau amri ya Bwana Yesu.

Kweli, maondoleo ya zambi ilitokea kwa Damu ya Mwokozi wetu Yesu Kristu aliyomwanga juu ya Musalaba wake. Hii maondoleo ni ya watu wote na watu wote weko na haki ya kuipokea, lakini namna gani? Pale ni chemchem lakini namna gani tutashota maji ya uzima?

Waprotestants wanatwaambia ya kama paka na imani kwa Kristu tutapata usamehe wa zambi zetu. Wanaleta hii mustari: “ *Pasipo upendeleo kati yetu sisi nao, akisafisha mioyo yao kwa imani”* (Matendo 15,9). Nikusema, kama tutasadiki, tutasamehewa zambi zetu.

Lakini, katika Maandiko takatifu tuko na namna ingine ya usamehe wa zambi zetu. Kwa mufano : Mu sala ya Bwana Yesu tunasema: „*Utusamehe deni zetu kama sisi vilevile tunawasamehe walio na deni zetu...“*. Mu Matendo 2,38 Mtume Petros anawaambia wale Waebrania walikusanyika ile siku ya Pentikosti : „*Tubuni mukabatizwe kila mumoja kwa jina lake Yesu Kristu, mupate maondoleo ya zambi zenu...“*. Tena ku mustari ya Marko 16,16 ): „*Aneamini na kubatizwa ataokolewa*“ Na ku mkustari Waefeso 5,26 : „*Apate kulitakasa, akiwa amelisafisha kwa maji katika neno“*. Mistari hizi zinatwaambia ya kama tunapokea maondoleo ya zambi zetu katika Ubatizo. Mustari ya Luka 11,41 : „*Lakini toeni sadaka za vitu vilivyo ndani, na tazama, vitu vyote ni safi kwenu“* na mustari ya Matayo 6,4 : „*Hata sadaka zako ziwe kwa siri, na Baba yako anayeona kwa siri atakupa zawabu“* yanatuonyesha namuna ya maondoleo ya zambi, katika huruma. Mu mustari ya Yakobo 5,16 tunasoma hivi : „*Kirini zambi ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mupate kuponyeshwa. Kuomba kwa mwenye haki kuna faida sana, kama akiomba kwa bidii“*. Hapa Mtume Yakobo anasema ya kama tutaponyeshwa katika roho, kama tunaungama mumoja kwa mwingine. Sawa vile tuliona juu, Mutume Yoane anasema sababu ya hii Fumbo ya Kuungama : „Mupokee Roho Mutakatifu, wo wote mukiwasamehe zambi, zitasamehewa kwao, na wo wote mukiwafungia zambi, zinafungwa kwao“( Yoane 20,23).

Hii sura zote zinatwaambia namna nyingi za usamehe wa zambi zetu. Waprotestants wanasimamia paka pa namna moja, nikusema *kwa imani*, na hawapendi kuona namna zingine. Tena wanakataa kufafanusha hii sura zote. Wanamutii mkubwa yao martin Luther, kwa sababu ni vile wanataka kuishi katika majivuno yao.

Kwa sisi waortodoksi hii mambo haiko kidogo. Hatuwezi kukubali sura fulani za Maandiko Takatifu na kuzarau zingine, kwa sababu tunasadiki ya kama Maandiko Takatifu iliandikwa katika maongozi ya Roho Mutakatifu.

Imani na Ubatizo ni namna za usamehe wa zambi zetu zile tulifanya mbele ya kuamini na ya kubatizwa. Lakini kila mukristu, kisha kubatizwa kwake atafanya zambi mara ingine. Sisi tubatizwa paka mara moja, kufwatana na hii maandiko : "*Bwana mumoja, imani moja, ubatizo mumoja"* (Waefeso 4,5), tuko na Fumbo ya kuungama sababu ya ile zambi tunafanya kisha ubatizo. Halafu tulisema juu ya usamehe wa zambi, sawa katika sala, huruma, masikilizano na watu hii yote ni namna ya kuleta rohoni mwetu hali ya kutubu na ya kuongoza roho yetu kuwa tayari Kuungama. Kristu aliwaambia Mitume yake : " „Mupokee Roho Mutakatifu, wo wote mukiosamehe zambi, zinasamehewa kwao, na wo wote mukiwafungia zambi, zinafungwa kwao"(Yoane 20,23). Kwa hivi anatupatia Fumbo ya kuungama. Kwa uwezo wa Roho Mtakatifu Mitume wataweza kufunga na kufungua zambi za watu.

Waprotestants wanatwaambia ya kwamba Yesu Kristu aliwapa Mitume wake Roho Mtakaitfu paka mara moja na hapana mara tatu. Paka ile siku ya Pentikosti, namna gani hapa aliamuru fumbo ya Kuungama kisha Ufufuo wake kufatana na mustari ya Yoane 20,23?

Sisi tunawajibu hivi: Ile siku ya Ufufuo wake hakutume Roho Mutakatifu, lakini aliwahidi ya kama atawatumia. Mbele ya siku kidogo alitayarisha roho zao ya kama atawatumia Roho Mutakatifu. Tena aliwashauria wasiondoke mbali ya Yerusalema mpaka watapokea uwezo toka juu mbinguni. Ni vile tena alifanya juu ya Fumbo ya Komunyo Takatifu. Mwaka moja,mbele ya Mateso yake alifundisha wanafunzi wake na watu hii Fumbo. Hakuwapa kitu, lakini alitayarisha roho yao juu ya kuipokea, kufwatana na mustari wa Yoane 6,52-67. Mitume walianza kufanya mafumbo yote. Tangu ile wakati Yesu Kristu aliondoka kati yao na walikuwa wamekwisha kupokea uwezo wa Roho Mutakatidu ile siku ya Pentikosti.

Mustari ya Yoane 20,23 inasema hivi : "*Mupokee Roho Mutakatifu*…". Alitayarisha roho zao. Tena aliwapa mamlaka, lakini bado kuwapa neema yake juu ya kufunga na kufungua zambi za watu.

Wakati Kristu aliwaambia Mitume : "*Mupokee Roho Mutakatifu*…" Mtume Thoma hakuwako pamoja na Mitume wengine, tutasema jee, ya kama Mtume Thoma hakupokea mamlaka na Neema ya hii Fumbo Takatifu? Alipokea Roho Mutakatifu ile siku ya Pentikosti, wakati alikuwa pamoja na wenzake na alipokea ahadi yote pamoja na Mitume wengine.

Waprotestants wanatwaambia ya kwamba hakuna mustari moja ndani ya Agano Jipya yenye kutuonyesha ya kama Waaminifu walikwenda kwa Mitume na waliungama.

Sisi tunawajibu hivi : " Iko vile na sababu ni tatu : Ya kwanza, ile wakati watu walikuwa paka wapagano. Zambi zao zilisamehewa kwa Ubatizo tu, na Maungamo haikukuweko, lakini katika mapenzi yao. Fumbo ya Maungamo ilipewa kwa Mitume sababu ya ile zambi watu watafanya kisha Ubatizo yao. Ya pili : Lufu ya ule mukristu Anania na bibi yake Safira (Matendo 5,1-10) na matendo mengine ya ajabu Mitume walifanya yaliwaogopesha waaminifu na kuwachunga nguvu na uzima safi na waliogopa nguvu ya Mitume, kwani walizani ya kama na wao itaweza kuwafikia ile mambo sawa Anania na Safira. Na ya tatu : Katika Maandiko takatifu hakuna namna kuyandika mafundisho yote kama anavyosema Mtume Yoane ( Yoane 21,25). Ni kwa hii sababu hatuna na ushuhuda wa Maungamo ya waaminifu ile wakati ya kwanza. Lakini amri ya Kristu katika Evangeli ya Yoane 20,23 iko wazi, haina na shaka ya kama ni lazima kuungama zambi zetu kwa wafwasi wa Mitume : maaskofu na mapadri.

Waprotestants wanatuuliza hivi : Sababu gani Mtume Paulo hakumwaambia mulozi Simoni :" kuja uungame ", lakini alimwaambia : "*basi geuza nia yako toka ubaya huu na umwombe Bwana ili akusamehe kwa kufikiri mawazo ya namna hii* (Matendo 8,22).

Sisi tunawajibu hivi : Hii Fumbo inasamehe ile zambi ilitendeka kisha ubatizo. Mulozi Simoni alikuwa bado kuamini kweli wala kubatizwa. Lakini mulozi Simoni katika maneno yake haya : "*Muniombee kwa Bwana kusudi lisinipate hata neno moja kati ya mambo haya muliyosema"* (Matendo 8,24), anajuwa ya kama Mitume Yoane na Petro weko na uwezo juu yake na wanaweza kumuondolea mutu zambi zake kwa Jina la Mungu.

Tena Waprotestants wanauliza juu ya nini leo hii Fumbo ya Kuungama inafanyika paka kwa siri na hapana mbele ya watu wengi kama ilivyokuwa zamani, sisi tunawajibu, kwa kutosha Kanisa yetu ku machukizo na taabu ya wale watu walikosa na kupoteza kitumaini yao na wanaweza kuharibu uzima yao : Sawa na Mafumbo ingine, hii Fumbo ya Kuungama hakuna namna padri kuzuia neema ya Mungu kuwafikia waaminifu. Kwa sababu padri hafanye Fumbo wala Neema haitoke kwake. Padri eko na uwezo mbele ya Mungu paka ya zambi zake, lakini sawa padri anawakabulia wakristu zawadi za Roho Mtakatifu hata kama mikono yake haistahili. Basi, Neema ya Mungu inakubali kuingia na kukaa ndani ya *vyombo vya udongo*" (2 Wakorinto 4,7).

Hapana paka Agano Jipya inatwaambia mambo mengi juu ya hii Fumbo, lakini na Watakatifu wa Kanisa yetu. Sasa tutakumbusha ushuhuda wa wale waliishi zamani kabisa juu ya sisi wote kujua ya kama hii Fumbo ilitokea kwa Bwana Yesu Kristu.

Mtakatifu Ignatio, askofu wa muji wa Antiokhia (30-107) aliandika mu barua yake kwa waaminifu ya muji Filadelfia : "*Bwana Yesu anasamehe wale wenye kutubu na wenye kumukiri Kristu na ndani ya kundi yao muko askofu*". Nikusema wale watatubu wanapashwa kutubu mbele ya Kanisa, kwani kanisa ni kusanyiko la mapadri na waaminifu na mkubwa yao ni askofu.

Tertilianos (145-220) anaandika hivi : " *Basi, kuungama ni fundisho ya roho ya mtu mwenye anapaswa kupiga magoti mbele ya Mungu na kujinyenyekeza. Tena anapaswa kuweka pa kichwa chake mufuko na juu yake maivi juu* ya *kuonyesha toba yake. Na anapaswa kupiga magoti na mbele ya mapadri.*

Mtakatifu Hipoliti, askofu wa muji Roma (170-236), ndani ya kitabu chake kinachoitwa "*Amri ya Misri*" muko sala moja ya upadirisho ya skofu inasema *: "Ee Bwana, kwa amri yako, katika cheo chake cha askofu, eko na uwezo wa kusamehe zambi na wa kufunga zambi, kwa hii mamlaka uliwapa Mitume wako"*. Hii ushuhuda ni ya mafaa sana kwa sababu ni ya tangu mwaka 230 na aliandikwa na mwandishi mumoja mkubwa wa Kanisa yetu.

Mtakatifu Kiprianos, askofu wa muji Karkhidona ya Afrika ya kaskazini anasema hivi : *Wandugu zangu, ninawaambia ya kama kila mtu anapaswa kuungama zambi zake, hii wakati kuiko namna Mungu kupokea toba yake na Kuungama kwake kutamufurahisha Mungu, na mukristu ataondolewa zambi zake ku mikono ya padri.*

Ili Kutubu iwe ya kweli inafai iwe hivi :

1. Inapaswa kuwa yote muzima, bila kuficha zambi hata moja. Mkristu atasema zambi zake toka maungamo yake ya mwisho mpaka ile siku, bila kuficha zambi zake fulani.
2. Inapaswa Maungamo ifanyike na roho safi na mapendo ya ule mkristu, hapana kama wanamutuma kwa baba yake ao kwa mama yake.
3. Inapaswa ifanyike kwa siri. Zamani Maungamo ilifanyika mbele ya waaminifu wote, lakini hii zoezo ilikataziwa tangu wakati wa Mitume.

4. Maungamo inapaswa kufanyika na unyenyekevu na roho yenye kuvunjika. Haifai kuifanya bila toba na mawazo mbaya juu ya jirani yake. Kazi kubwa mu uzima ya mukristu ni kwacha kufanya zambi. Vile ataendelea mu uzima ya roho na atapata fazila za Kristu.

Sasa ku mwisho tunaweza kusema ya kama wenye uwezo na wakubwa wa kusamehe zambi za waaminifu ni paka maaskofu, mapadri na mashemasi. Kristu, mbele ya kupanda mbinguni aliwaambia Mitume wake: „*Mimi ni pamoja nanyi siku zote hata mwisho wa dunia*" (Matayo 28,20). Mitume walikufa, hii kazi yao ilibaki ku mikono ya watoto wao wa roho na mpaka sasa wanaendelea hii kazi. Kristu eko pamoja nao na tena pamoja na wafwasi wao mpaka mwisho wa milele. Kwa hivi, basi, paka hawa weko na mamlaka ya kufunga na kufungua zambi za waaminifu, na hapana Waprotestants ambao walionekana mara ya kwanza duniani mu mwaka 1535. Hata ku mbele Kristu hatakuwa pamoja na Waprotestants, kwa sababu Kristu anabariki na anakaa ndani ya Kanisa Yake ile aliacha duniani, tangu ile siku alikuja karibu yetu. Hii Kanisa leo inaitwa Orthodokse na hii itabakia milele Chombo cha wokovu cha kila mutu mwenye kutaka kuokolewa.

# MAFUNDISHO YA FUMBO YA NDOA

Ndoa ni Fumbo moja katika Mafumbo saba ya Kanisa yetu. Kwa hii Fumbo mume na muke wanasikilizana kuishi pamoja, mumoja karibu ya mwingine na baraka ya Mungu juu ya kufanya jamaa yao, kuzaa na kukomesha watoto wao na kuwapa maendeleo mu uzima ya kiroho. Juu ya kutimiza hii agano yao, wanapokea baraka ya kanisa katika padri orthodokse ambaye kwa jina la Kristu anawapa Neema takatifu.

Waprotestants wanakataa hii Fumbo kuwa ibada ya kanisa. Basi, wanasadiki nini juu ya hii Fumbo? Wanasema hivi :" *Ndoa ni kuungana kwa mume na muke mbele ya washuhuda katika sheria ya hii fasi wanaishi. Ndoa iko ya kweli kama inafanyika mbele ya wakubwa ya muji yao"*. Hii haiko ndoa ya kanisa, ni ndoa mbele ya mkubwa ya muji (mariage civile), haina na baraka ya kanisa na ya Mungu.

Jibu gani Kanisa yetu Orthodokse inawapa : " Ndoa ni Fumbo kubwa. Mbele ya kuowana kwao, hawa watu wawili, mume na muke walikuwa watu wasipo kujuana katikati yao. Sasa, katika Ndoa ya kanisa wanapokea baraka ya Mungu bila wao wawili kusikia ya kwamba wanakuwa moja. Hii muungano ya watu wawili haiko paka katika mwili, lakini tena katika roho. Ndio maana Mungu alisema : " *Kwa sababu hii mume ataacha baba yake na mama yake na atauungana na muke wake; na watakuwa mwili mumoja*" (Mwanzo 2,24). Wao wawili katika kanisa, kisha ndoa yao wanabaki miili mbili, lakini Mungu anawaita hapa mwili mumoja. Basi, hapa inaonekana maana ya hii Fumbo, maana yake inapita akili ya mutu.

Mungu alifanya mara ya kwanza hii Fumbo mu Agano la Kale. Katika kitabu cha Mwanzo 2,18 tunasoma hivi : " *Si vema mutu awe peke yake; nitamufanyia musaidizi anayefaa kwake*" (Mwanzo 2,18) . Na mara moja Mungu aliumba Adamu, na toka ubavu wake aliumba muke, Eva (Mwanzo 2,21-24). Wakati aliwaumba, aliwaambia: "*Muzidi na kuongezeka na mujaze tena inchi na kuitisha*" Mwanzo 1,28*)*.

Mtume Paulo anafananisha umoja wa mume na muke na umoja wa Kristu na Kanisa. Mu barua yake kwa Waefeso 5,22-23 anasema : " *Ninyi wake, mutii waume wenu, kama kutii Bwana. Kwa maana mume ni kichwa cha muke, kama Kristu vilevile ni kichwa cha Kanisa, naye ni Mwokozi wa mwili*". Ku mustari ingine chini (5,29-30) anasema : " *Maana hakuna mutu aliyechukia mwili wake mwenyewe wakati wowote; lakini anaukulisha na kuuchunga, kama Kristu vilevile anavyotenda kanisa"*. Basi, kufwatana na Evangelio, katika ndoa mwanamuke ni mwili wa mume wake na mume ni kichwa chake. Hii umoja kati ya wanaume na wanawake, tena na kati ya Kristu na Kanisa yake ni Fumbo kubwa. Lakini, kwa akili yetu, namna gani Kristu aliacha Baba yake wa mbinguni, alikuja duniani na aliowa Kanisa na viungo vyake ni sisi watu wote wenye zambi ambao mbele ya kufika Kristu tulikuwa wageni na adui katikati yetu?

Mtume Paulo, anasema ya kama ndoa haiko Fumbo ndogo, lakini ni Fumbo kubwa : *" Hii Siri (Fumbo) ni kubwa; lakini ninasema habari za Kristu na kanisa"* (Waefeso 5,32). Kwa kusema hivi Mt. Paulo anasema juu ya Ndoa katika jina la Kristu, hapana juu ya ndoa yoyote, kwa sababu Waprotestants wanasema juu ya ndoa, ndoa yoyote, hata ile ilifanyika mbele ya kuzaliwa kwa Kristu, ao ile ndoa inafanyika bila jina la Kristu. Tena hii barua yake Mtume Paulo anaituma kwa wakristu, hapana kwa wapagano wa muji wa Efeso.

Waprotestants wanakataa kusadiki ya kama katika hii Fumbo ya ndoa inashuka Neema ya Roho Mtakatifu. Lakini sisi tunawaambia hivi : " Mtume Paulo anawaambia wale vijana wataowa waishi katika mapendo na utii, sawa vile Kristu anaishi na Bibi-Arusi yake, nikusema Kanisa yake.*"Lakini kama vile Kanisa linavyotii Kristu, hivi vilevile wake watii waume wao katika kila kitu"* (Waefeso 5,24), mapendo ya Kristu kwa Kanisa yake na utii ya Kanisa yake kwake haiko kitu cha bure, lakini ni kitu takatifu na ya kimungu. Hii umoja iko kati ya Kristu na Kanisa yake inapaswa kuwa vilevile kati ya mume na muke wake. Halafu, tunauliza Waprotestants : Bila

nguvu kimungu na Neema ya Roho Mtakatifu kuiko namna ya hawa watu wawili kuishi mu umoja kati yao, kwa sababu na wao ni watu wenye zambi sawa sisi wote? Hapana. Hawa ni watu na watapata mateso, taabu na machukizo mengi mu uzima yao. Lakini namna gani watavumulia hii mateso yote bila msaada na Neema ya Roho Mtakatifu? Ni lazima iwafikie Neema kimungu juu ya kuwapa nguvu kimungu.

Sawa vile zamani ndoa ilikuwa mu Agano la Kale : " *Kwa sababu hii mume ataacha baba yake na mama yake na atafungana na muke wake...* " (Mwanzo 2,24) mufano na sura ya ndoa ya Kristu na Kanisa yake. Vilevile mu Agano Jipya ndoa ni mufano wa ndoa ya Kristu na Kanisa yake. Kwa hivi ndoa ya Agano la kale na ndoa ya Agano Jipya ni mufano wa ndoa ya Kristu na Kanisa yake, kwani ndoa ya Kristu ni mufano muzuri wa uzima ya wakristu. Ili ndoa iwe kamilifu sawa ile ya Kristu na Kanisa yake, ni lazima kuwe neema na nguvu ya Mungu, kufwatana na barua kwa Waefeso (5,22-25). Kwa hii mambo ndoa kati ya mume na muke inaitwa Fumbo kubwa kwa Mtume Paulo, kwa sababu matendo yake ni ya kufwatanisha mufano wa ndoa ya Kristu na Kanisa yake.

Mtume Paulo anatwaambia juu ya ndoa ya mume na muke : " *Ndoa iheshimiwe na watu wote, na kitanda kisiwe na uchafu: kwa sababu Mungu atahukumu waasherati na wazini*" (Waebrania 13,4). Walevi na wsharati wanaleta mu maisha yao kasirani ya Mungu (1 Petro 4,3-6). Kama mumoja kati ya wale waliunga ndoa atakufa, mwingine anaweza kuunga ndoa mara ingine, hii haiko zambi (Waroma 7,2-8). Lakini kama mume mumoja anaishi na muke wake bila ibada ya Ndoa, huyu anaishi bila baraka ya Mungu na ya Kanisa na eko muzini (1 Wakorinto 6,16-20). *Wanaume wanapaswa kupenda wake wao, vilevile wanawake wanapaswa kuogopa waume wao na watawatii sawa wanatii kwa Kristu* (Waefeso 5,22-33).

Makundi ingine ya Waprotestants wanasema ya kama wanafanya Ndoa ya Kanisa. Lakini, namna gani wanafanya ndoa mu Kanisa kama wao wanakataa hii Fumbo takatifu. Hata, kama "Pasteur yao mkubwa" atawasomea sala mingi, hakuna namna ya wao kupata baraka ya kanisa, kwa sababu kila "pasteur" yao ni laiki hakupokea Fumbo ya upadirisho. Maana, bila upadirisho hakuna namna mutu mumoja kufanya ibada ndani ya kanisa ya Mungu. Mu Kanisa Orthodokse hakuna namna kufanya ibada ao Fumbo fulani bila kutumia baraka ya Musalaba. Kama waprotestants wanakataa Musalaba ya Kristu, namna gani wataweza kuleta baraka ya Kristu mu uzima ya waaminifu wao?

Ule mkubwa yao Martin Luther hakukatae paka hii Fumbo, lakini alisema tena ya kama ndoa ni sawa na mapatano ya wanyama katika miili, kwa Martin Luther mawazo yako ni ya kuongeza hesabu ya watu katika hii dunia. Nikusema katika ndoa Martin Luther haone kuwa kitu kitakatifu, ni paka ya kufurahisha mapenzi ya watu. Alikataa tena na kanuni za Kanisa zenye kukataza kuoana kati ya wandugu wa jamaa moja. Nikusema, Martin Luther aliamuru kuoana kati ya wandugu : waviala, muyomba na mwipwa yake mwanamuke, na ingine ingine... Lakini, kisha miaka fulani wafwasi wake waliheshimia kanuni za kanisa, maana walikataza watu wa jamaa moja kuoana, sawa muyomba na mwipwa yake mwanamuke, na ingine...

Kwa mutu mumoja kuunga ndoa yake katika Kanisa Orthodokse, kufwatana na kanuni ya Kanisa yetu, hapashwe kuifanya wakati wa Mafungo ine, nikusema Kwarezima : Mafungo ya Kuzaliwa kwa Kristu, Mafungo ya Mzazi-Mungu, Mwanzo ya Augusti na Kifunga, mu juma moja kisha siku ya Pentikosti mpaka siku Kuu ya Mitume Petro na Paulo.. Tena hawezi kuunga ndoa siku ya Kukata Kichwa cha Yoane Mtangulizi (29 Augusti). Tena hapana kuunga ndoa mu Juma Mkubwa na Takatifu, ao siku ya yenga ya Matawi.

Tuko na ushuhuda ya zamani :

Mtakatifu Ignatios, askofu wa Antioki anamwandikia hivi askofu Polikarpo wa Smirni :

"*Inapaswa hawa watu wanapenda kuoana wapokee baraka kwa askofu yao, juu ndoa yao inapaswa kuwa katika Kristu na hapana katika mapenzi yao*". Naye Tertilianos +24) kisha

kuzaliwa kwa Kristu anaandika hivi *: " Ndoa ya Kanisa ni ya lazima, baraka inawapa chapa, malaika wanaitangaza. Baba wa mbinguni anabariki*".

Mtakatifu Ambroise askofu wa Mediolana kule inchi ya Italia (397 kisha kuzaliwa kwa Kristu, anaandika hivi : " *Ndoa inapaswa kutakaswa na baraka ya padri ndani ya Kanisa..."*

Basi, kwa maneno ya Mtume Paulo Ndoa ni Fumbo kubwa. Inaleta neema takatifu mu uzima ya wale wanaowana. Hii Fumbo ni kitu chenye kuonekana, ni baraka ya Kanisa na mapenzi ya wale wanaowana. Tena ni kitu kisichoonekana, nikusema ni Neema ya Roho Mutakatifu. Wale watu wanaenda kwa mukubwa ya muji juu ya kuunga ndoa yao (mariage civi), hii ndoa ni zambi ya uzini. Wanakataa Kanisa ya Kristu, pahali wazazi waliwabatiza, waliwakomesha na ku mwisho ni paka katika Kanisa mapadri watasoma na sala ya lufu yao.

## MAFUNDISHO JUU YA UPADIRISHO

Yesu Kristu hakukaa zaidi duniani. Alipanda kwenda mbinguni na anakaa kuume kwa Baba yake. Lakini ilikuwa lazima, mbele ya kuondoka kwake, aweke watu wazuri kwa kuendelesha kazi yake, nikusema kutangaza Habari Njema na kuwahubiri watu, kuwabatiza, kufunga na kufungua zambi zao watu. Hawa watu wanaitwa Mapadri, weko na daraja tatu: askofu, padri na shemasi. Kwa sababu Kanisa ya Kristu iko katika inchi yetu, inapaswa hawa watu watokee mu hii inchi sababu ya kuendelesha hii kazi Bwana Yesu Kristu aliwapa.

Waprotestants hakuna namna ya kusadiki ya kama ni cheo ya Upadirisho. Tena, wanasema ya kama hii cheo ilitokea kwa shetani. Wanahubiri na kasirani na kukombanisha mapadri wetu. Hii chuki yao ilianza toka mkubwa yao Martin Luther aliyechukia mapadri ya kanisa ya papa na kukombanisha Fumbo ya Upadirisho. Nikusema haseme : " Inje mapadri wasiyostahili ", lakini alisema na " Inje na mbali Fumbo ya Upadirisho ".Tena, juu ya kuhakikisha na yeye ya kama anaitikia hii maneno yake, alikataa upadirisho yake sababu ya kufurahisha uzima yake sawa laike.

Tazama, wanasema nini: " Hakuna daraja ya mapadri, kwa sababu kufwatana na Evangelio, sisi wote tuko mapadri. Na wanatuonyesha hii mistari : " *lakini ninyi taifa chaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu walio mali ya Mungu mwenyewe, mupate kutangaza uzuri wake aliyewatia ninyi toka giza mwingie katika nuru yake ya ajabu*" (1 Petro 2,9) na „*Ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanatawala juu ya dunia*" (Ufunuo 5,10), na " *na kutufanya kuwa ufalme wa makuhani kwa Mungu na baba yake*..." (Ufunuo 1,6).

Sisi tunawajibu hivi : Mu Agano la Kale (Kutoka 19,6 na 23,22) mustari „*Ukuhani wa kifalme"* maana yake ni taifa la Israeli, muchanguliwa wa Mungu. kulikuwa na kabila la Walawi ambao walikuwa mapadri wa dini ya Waebrania. Tunauliza hivi Waprotestants : Juu ya nini wanaitika mu Agano la Kale hii " Ukuhani ya Kifalme", nikusema taifa la Mungu na upadirisho ya wale walikuwa wa kabila ya Walawi, lakini mu Agano Jipya wanaitika upadirsho ya watu wote na wanakataa upadirisho ya mapadri? Wanatafuta kuonyesha ya kama ni Upadirisho ya mapadri wa Agano Jipya? Sisi tunawajibu ya kwamba : Wakati Kristu aliweka Fumbo ya Komunyo Takatifu, aliwaambia Wanafunzi wake : " *Twaeni, kuleni, huu ni mwili wangu, uliovunjika kwa ajili yenu, fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi*" (1 Wakorinto 11,24-25). Juu ya hii mustari sisi tunapaswa kuitika ya kama Mitume walikuwa mapadri. Mtume Paulo anawaambia wale Wakorintho : " *Kikombe cha baraka tunachobariki, si ushirika wa damu ya Kristu; Mukate tunaovunja, si ushirika wa mwili wa Kristu* " (1 Wakorinto 10,16). Namna gani Mtume Paulo anasema : " *tunachobariki*" na "*tunaovunja*" kama huyu hakuwa padri wa Kristu? Kama tunaitika, sawa vile wanasema Waprotestants, paka upadirisho wa wakristu wote, juu ya nini Kristu hakuwaambia watu wote hii maneno : " *Mwendeni basi mukafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mukiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu*" (Matayo 28,19) lakini aliwaambia paka wale alichagua, nikusema wanafunzi Wake? Juu ya nini alilaka kuwatumia Roho

Mtakatifu paka Mitume juu ya kufunga na kufungua zambi za watu na hapana kwa watu yote? (Yoane 20,22,23). Kweli, kwa sababu alichagua katikati ya watu wanaume fulani na aliwapa mzigo ya hii kazi ya kuchunga na kufungua zambi za watu na kutimiza Mafumbo yote. Hii mamlaka Kristu aliipatia hapana paka kwa Mitume, lakini na kwa Kanisa yake, na Kanisa, katika milele yote anatafuta watu wazuri na anawapa muzigo ya kuwa mapadri wa taifa la Mungu.\

Tena, hata ile wakati wa Mitume kulikuwa daraja tatu za upadirisho. Mashemasi saba walikuwa mu daraja ya kwanza. Wengine katikati yao walikuwa mapadri ao maaskofu. Mtakatifu Luka, mwandishi wa kitabu cha Matendo ya Mitume, anatwaambia ya kama Mtume Paulo alipadirisha mapadri na shemasi katika maparokia yeye alifungula (Mdo 14,23). Huyu Mtume Paulo aliweka Tito, mtoto yake wa roho, kuwa askofu kule Kisanga ya Kreti. Ku muji Efeso aliweka mtoto yake wa roho Timotheo; aliwashauria waongeze moto ya mapendo pa hii zawadi ya upadirisho ile walipokea ku mikono yake (2 Timotheo 1,6). Hakuna shaka ya kwamba hii amri aliipatia na kwa maskofu wengine, juu ya kuleta neema ya upadirisho kwa vijana waaminifu, hivi, hii zawadi inaendelea katika milele kwa utakaso wa wakristu.

Basi, ni upadirisho ya kundi moja, nikusema ya mapadri, na hawa ni wachungaji wa taifa la Mungu. Ni Mungu anachagua hawa mapadri, hapana watu sawa vile inafanyika kwa Waprotestants ambao wanachagua "pasteur" yao. Mtume Paulo anamwaambia mtoto yake wa roho Timotheo : " *Usiache kutumia zawadi iliyo ndani yako uliyopewa kwa unabii na kwa kuwekewa mikono ya wazee*" (2 Timotheo 4,14). Fasi ingine (1 Timotheo1,6) anamwaambia: "*Kwa sababu hii ninakukumbusha, uamshe zawadi ya Mungu iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu*"; na fasi ingine (1 Timot.5,22): "*Usiwekee mutu mikono kwa haraka, wala usishiriki kwa zambi za watu wengine"*. Hapa Mtume Paulo anataka kusema nini? Ya kwamba upadirisho ni zawadi ya Mungu, inakuja kwa watu katika ibada ya Upadirisho na hii ibada ni maaskofu wanaifanya, ndio Fumbo ya Upadirisho.

Ni kweli, makundi mbalimbali ya waprotestants wanaita wapasteurs yao maaskofu, mapadri na mashemasi. Lakini, musizanie ya kama hawa wapasteurs weko na zawadi ya upadirisho na ya fumbo ya ibada ya Upadirisho, hapana, kwa sababu « makanisa » yao haina na ufwasi ya Mitume. Wanafanya paka hivi kazi ya administration pa ile fasi waaminifu wao waliwachagua na kuwapa hii kazi. Hakikisho ya kwamba wapasteurs yao hawana na daraja ya upadirisho inaonekena wazi : hawafanye hii kazi yao mu uzima yao yote, kwa sababu wanasimamishwa kisha wakati fulani, na waaminifu wao wanachagua watu wengine.

Mu inchi ya Ingreza ni « kanisa » moja tu iko na daraja tatu za Upadirisho. Sawa vile waongozi wao wanajikaza kusema ya kama askofu yao mkubwa wa kwanza alikuwa na upadirisho ya kweli na ilitoka kwa Mitume wa Kristu, kwa hivi wanasema, mafumbo yao ni ya kweli 9. Lakini wanachoka bure, kwa sababu Kanisa ya Kristu haikwanze mu karne ya kumi na sita mule ilianza kanisa yao, lakini Kanisa ya Kristu ilianza mu karne ya kwanza.

Tena mambo ingine ya ajabu na ya taabu nyingi ni hii : Kanisa « Anglicane » mu Amerika ilikamata mpango ya kuingiza wanawake mu daraja ya upadirisho. Tena kwa hii wakati wanapadirisha maaskofu wanawake, lakini mtume Paulo anakataa wanawake kuhubiri mu Kanisa ao kufanya ibada fulani (1 Timotheo 2,12).

Kundi ya Waprotestants yenye kuitwa "Kanisa ya wanafunzi wa Kristu" iliweka kuwa pasteur wao binti moja wa umri wa miaka 19. Huyu binti kwa mahubiri yake ya kwanza alihubiri juu ya mavazi ya binti na vijana wanawake. Alisema wanapaswa kuvaa mavazi mifupi, kukata nywele zao, kupakaa nyuso zao rangi mbalimbali , kucheza, kunywa na kufurahi katika hii dunia. Ma "kanisa yao" kule ku Ulaya weko na wapasteusr wanawake. Hii matendo yanatuonyesha ya kama waprotestants walijitumbukiza katika fujo na katika mafundisho mubaya mbalimbali. Walianguka mu hii fujo kwa sababu wanafwata majivuno yao na wanakataa kufwata Mapokeo takatifu na mafundisho ya Kanisa ya Kristu, Kanisa Orthodokse.

Waprotestants mingi wanatuchukia wanasema ya kama mapadri wetu ni watu wenye zambi. Sisi tunawajibu hivi : Kanisa ya Kristu ni takatifu na safi haina na uchafu na hakuna namna kuchafuka sababu ya zambi zetu. Tena, na Kristu alikuja duniani sababu ya kuongoza watu watubu. Mafumbo haiharibike kama ule padri mwenye zambi anafanya Fumbo fulani, kwa sababu Fumbo ni tendo takatifu na ni Neema ya Mungu, hapana uzima ya ule padri itazuia kuja kwa Neema Takatifu. Wafarisayo walikuwa wadanganyifu na wenye zambi kabisa kuliko watu wengine. Yesu Kristu aliwahamakia, lakini hakuwahukumu wale watu waliwafwata. Paka aliwaambia hivi : « *Basi maneno yote wanayowaambia ninyi kutenda, muyashike na kuyatenda; lakini musitende kwa mufano wa matendo yao*“ (Matayo 23,3). Nikusema, mufanye ile wanawambia ninyi kufanya lakini musifwate matendo yao. Hii jibu ya Kristu tunaweza kuwapayo na wale watu wenye kuhukumu mapadri wetu juu ya zambi zao fulani. Tena haipaswe kusahau ya kama ndani ya jicho lao muko boriti, kama anavyosema Kristu : *« Kwa nini unaona kitakataka ndani ya jisho la ndugu yako, lakini hufikili boriti iliyo ndani ya jisho lako mwenyewe »* (Matayo 7,3-4).

Katika Liturgia moja kunawezekana kufanyika upadirisho tatu, moja ya shemasi, moja ya padri na moja ya askofu, lakini hakuna namna kufanyika upadirisho mbili na cheo moja katikadani ya Liturgia moja. Wakristu wengine wadanganyifu na wenye kukosa imani wanachukia mavazi ya mapadri na ya maskofu wetu. Sisi tunaweza kuwaambia hivi : Kwa wakati wake Yesu Kristu alihukumu kundi la Wafarisayo na Wandishi wa Sheria juu ya matendo yao, hapana juu ya mavazi yao mazuri, kwa sababu yale mavazi yalikuwako tangu wakati wa Agano la Kale (Hesabu 15,38), lakini aliwahukumu sababu ya udanganyifu yao, kwa sababu walivaa hii mavazi na majivuno bila heshima. Kwa hivi na padri moja wa sasa hapashwe kujivuna sababu ya manguo yake ile Kanisa alimupa, anapashwa kuishi na kutembea na unyenyekevu mingi na kumwogopa Mungu katikati ya waaminifu wake. Manguo marefu ya mapadri wetu yanatukumbusha mavazi marefu ya Bwana Yesu, ile inaitwa kanzu (Yoane 19,23). Mapadri wanavaa kofya na maaskofu kofya ingine yenye kuitwa „Mitra“ kama wanafanya Liturgia yao. Hii wanafanya ni sawa mufano ya makuhani ya Agano la Kale (Hesabu 6). Mtume Paulo naye alifwata desturi ya Nazairei (Matendo 18,18 na 21,20-24). Kufwatana na mapokeo yao wale walifwata hii Kundi ya Nazirei hawakukate nywele na ndevu yao. Katika Kitabu cha Agano la kale, kinachoitwa Walawi tunaona ya kama Mungu anaamuru makuhani wasikate nywele zao na ndevu yao (Walawi 21,5). Na manabii wote, Wapatriarchi, Mitume na Bwana Yesu Kristu wote walivaa mavazi marefu mbalimbali na walichunga ndevu yao na nywele zao.

Katika kitabu na uzima ya Mtakatifu Pagratios, askofu wa Tabromenia, aliyeishi mu karne ya kwanza, tunasoma hivi : „Wakati mtawala wa inchi, jina lake Bonifatio alienda kumukuta askofu Pagratios, alimukuta mwenye kuvaa manguo ya ukuhani wake na mwenye kukaa pa kiti kimoja kirefu. Mbele yake kulikuwa picha ya Kristu na Musalaba. Wakati alimuangalia, alianguka na aliinamisha uso wake chini juu ya kumusujudu. Alishangaa kwa ile mwangaza ilimuzunguka ku uso wake na hakuweze kutazama na macho yake. Mtakatifu alimuamusha, alimubusu, na ule mkubwa alimwaambia: “Mungu wa Wakristu ni Mkubwa. Ninakuamin,i ee Mungu wangu Yesu Kristu, Mungu wa kweli kamili!

Mtakatifu alimubariki na alimuamuru akae karibu yake. Ule mtawala alimujibu : “namna gani nitakukaribia, kwa sababu ninaona moto yenye kuwaka pembeni yako? Mt. Pagratios alisikia ya kama hii moto ilikuwa Neema ya Roho Mtakatifu ile ilitokea ku mavazi yake. Wakati alitosha manguo yake matakatifu hii nuru haikuonekana tena.

Mavazi ya utukufu ya askofu na padri ndani ya Kanisa wakati wanafanya ibada ya Liturgia, haiwezi kutuchukiza, kwani hii maneno inasema hivi : « *Mapadri wakubwa wa Kanisa yetu wanasema ya kama Zabihu ya hii dunia ni mufano na alama ya Zabihu ya mbingu. Na askofu, anayevaa manguo yake takatifu eko pa fasi na pa kazi ya Bwana Yesu Kristu* ». Kwa hivi mufano ya padri ao askofu inatupatia mufano ya utukufu wa zabihu ya mbingu. Tunaona utukufu

ya Kristu, ni sababu ya hii utukufu wake wanavaa na watumishi wake mavazi mazuri na ya utukufu mingi. Mt. Bazile, wakati alivaa manguo yake, aliwaza ya kama anaivaa pa fasi ya Bwana Yesu Kristu. Kwa hivi alisema : "Sasa Bazile anavaa Kristu". Nikusema anavaa utukufu wa Kristu katika manguo yake matakatifu.

Tena watu wengine wanachukia mapadri wetu kwa sababu wanapokea mushahara. Sisi tunasema ya kama mapadri wetu wanalipwa hapana juu ya zawadi yao, lakini sababu ya muchoko kwa kazi yao. Mtume Luka anasema (10,7) : „*Kwa maana mutenda kazi anastahili kupewa mushahara wake*" tena na Matayo 10,9-14. Mtume Paulo anatwaambia mu barua yake (1 Wakorinto 9,13-14. „*hamujui ya kwamba wale wanaofanya kazi ya hekalu wanakula sehemu ya vitu vya hekalu, na wale wanaotumikia kwa mazabahu wanashirikiana vitu vya mazabahu*?" tena mu barua yake 1 Timotheo 5,17 *: „Wazee(mapadri) wanaotawala vema wahesabiwe kustahili heshima mara mbili zaidi wale wenye kujitaabisha sana kwa neno na kwa mafundisho"....Usifunge kinywa cha ngombe wakati anapokanyanga ngano".*

Lakini kuna mapadri wengine sababu ya tabia yao mbaya walianguka na wakawa wapenda feza na wadanganyifu, sisi hatupashwe kuhukumu sheria, wala kuchukizwa kwa tabia yao, kwa sababu amri ya Kristu ni safi : „*Musihukumu ili mkusihukumiwe"* (Matayo 7,1-5). Neno lingine la nguvu kabisa; linasema ya kwamba : « *Neema ya Mungu haitakosa kuja sababu ya mikono isiyostahili ya padri mumoja. Inashuka na inatakasa waaminifu. Mambo ya hatari itakuwa paka kwa padri, atasema nini kwa Mungu wakati atasimama kuleta jibu ya matendo yake,* sawa vile na sisi wote.

## MAFUNDISHO JUU YA FUMBO YA KUPAKAA MAFUTA TAKATIFU

Na hii Fumbo Waprotestants wanaikataa na wanasema ya kama ni ibada moja ya kufanya kama mtu mumoja ni mugonjwa, lakini hakuna namna ya kuwa Fumbo, kwa sababu, hivi wanasema, Neema ya Mungu haikuje kwa mugopnjwa..

Juu ya hii Fumbo tunasoma barua ya Mtume Yakobo (5,14-16) : „*Mutu wa kwenu amekuwa mgonjwa? Aite wazee (mapadri) wa kanisa; nao waombe juu yake, na kumupakaa mafuta kwa jina la Bwana. Na kule kuomba kwa imani kutaokoa mugonjwa yule, na Bwana atamusimamisha; na kama amefanya zambi, atasamehewa"* Hapa Mtume anatushauria ya kwamba kama mutu mumoja ni mugonjwa tunapaswa kuita mapadri wa Kanisa. Hawa wataomba kwa Mungu, watamupakaa mafuta na hii sala yao ya imani itamuponyesha ule mugonjwa. Tena, kama alitenda zambi atasamehewa.

Vile vitu vinaonekana pa hii Fumbo ni mafuta na sala ya mapadri. Waprotestants wanasema ya kama mafuta haiko kitu cha kuonekana na cha lazima, tangu zamani mafuta haiwezi kuponyesha watu ku magonjwa yao fulani. Lakini, sisi tunawajibu ya kama hapa Mtume Yakobo anasema paka mapadri watamupakaa ule mugonjwa mafuta, hapana watu wengine, ndugu, marafiki ao jirani zake, paka padri.

Mafuta iko na nguvu ya kuponyesha magonjwa fulani, lakini hapana magonjwa yote. Sala, katika imani, ni hii inasaidia mugonjwa kupona, na kupakaa mafuta inaonyesha hii ponyesho.

Mafuta haiko kitu cha bure, lakini ni ya lazima pamoja na sala ya imani. Ile neema inakuja kwa mugonjwa inamuponyesha katika mwili na roho yake. Lakini waprotestants wanasema ya kama hawaone miujiza kisha hii Fumbo. Sisi tunawajibu hivi : Paka Mungu anaweza kufanya miujiza, ni Yeye atakamata mpango ya kuponyesha mgonjwa ao hapana, kwa sababu paka Yeye anajua mafaa ya wokovu ya ule mutu. Lakini ya kweli ule mugonjwa anapokea neema kimungu na katika mapenzi ya Mungu anasamehewa zambi zake. Hatuwezi kukataa hii baraka ya Neema takatifu, kwani Roho Mutakatifu haseme uwongo, wakati Mtume anasema: *Na kule kuomba kwa*

*imani kutaokoa mugonjwa yule, na Bwana atamusimamisha*. Hapa tunaona kupona kwa mugonjwa.

Waprotesrtants wengine wanasema ya kama hapa Mtume Yakobo anasema juu ya zawadi ya kufanya miujiza, ile walikuwa nayo Mitume kufwatana na mustari ya Marko 6,13: „*Wakapakaa na mafuta watu wengi waliokuwa wagonjwa, wakawaponyesha*“. Sisi tunawajibu: zawadi ya kuponyesha wagonjwa Mungu alileta kwa watu mbalimbali kwa wakati kidogo. Nikusema hawakuwa siku zote ndani ya kanisa. Lakini hapa Mtume Yakobo anatwaambia juu ya kukimbilia ku maponyesho ya magonjwa fulani kwa mapadri wa kanisa. Hii kazi ni mapadri wanaweza kuifanya kila mara, wao weko na uwezo ya Mungu siku zote katika Kanisa ya Kristu. Tena zawadi ya miujiza ilibakia kidogo mu wakati yetu, lakini hii Fumbo iko ya magonjwa siku zote.

Ni kweli, hii Fumbo haiponyeshe kila ugonjwa kwa sababu ni hivi Mungu Yesu Kristu anapenda. Kama itaponyesha kila ugonjwa, inapashwa kufunga ma hopitali yote na kuondoa masomo na kazi ya waganga, lakini hii uganga ni Mungu anatupatiayo.

Hata, kama mugonjwa hataponyeshwa katika mwili wake ataponyeshwa katika roho yake, kufwatana na mustari ya Yakobo: „*Na kama amefanya zambi, atasamehewa*“. Hii mustari haipingane na mistari ingine yanayosema juu ya Fumbo ya Kuungama, lakini inatengeneza hivi: Sisi wote tuko wenye zambi na kama anavyosema Mtume Yakobo : „*Maana tunajikwaa sisi sote pia katika mambo mengi*“ (3,2) Lakini namna gani inasema mustari: „*Na kama amefanya zambi*, a*tasamehewa*“? Hii neno linaleta kweli shaka ya kama sisi wote tuko wenye zambi? Na kwa hii neno : „*kama amefanya*...“anataka kusema juu ya ile zambi ilileta ugonjwa kwa ule mugonjwa. Kwa mufano : Wakati Kristu alimuponyesha ule mtu mwenye kupooza (Yoane 5,14) kisha alimushauria hivi : „*Usifanye zambi tena, neno mbaya zaidi lisikushike*“. Na Mtume Paulo anatwaambia hivi : „*Na kwa sababu hii wengi kati yenu ni wagonjwa na wazaifu, na wengi wamekufa*“ (1 Wakorinto 11,30). Kwa hivi, hii Fumbo kama haiponyeshe mwili wa mugonjwa inamuponyesha katika roho.

Ni amri ya Kristu ile aliwapa Mitume wake juu ya maungamo ya zambi zetu. Lakini zambi ngapi tunafanya bila mioyo, bila kusopoka, bila kujua na bila kuongojea? Zambi ngapi zinaharibu macho ya roho yetu? Na nani anaweza kutwaambia ya kama hii zambi inaleta ugonjwa kwa ule mugonjwa? Basi, zambi hizi kidogokidogo zinasamehewa na hii fumbo ya Kupakaa mafuta takatifu. Hii Fumbo inasaidia na inatimiza Fumbo ingine kubwa ya kuungama. Mwaaminifu kwa Fumbo ya kuungama atasema zambi zake kubwa anazokumbuka muzuri, lakini zambi zake kidogokidogo zinasamehewa kwa Fumbo ya Kupakaa mafuta. Na zamani, ilikuwa zoezo, Fumbo ya Kupakaa mafuta ilifanyika kisha Fumbo ya Kuungama, na mwisho Fumbo ya Komunyo takatifu.

Ushuhuda ingine tangu zamani juu ya hii Fumbo tutaipata ndani ya vitabu vya askofu wa Roma, Hipoliti, aliyezaliwa ku mwaka 150 kisha kuzaliwa kwa Kristu. Mu Kitabu chake kimoja kinachoitwa *Amri kwa Mitume*, anaandika hivi : “ *Ee Mungu, takasa hii mafuta juu ya kuleta afya kwa wale weko nayo lazima. Sawa vile kwa hii Mafuta walipakaliwa wafalme, manabii na mapadri, vilevile, ee Mungu, na kwa wale wanapokea hii Mafuta, uwape afya”*.

Théologien mkubwa wa Kanisa yetu anayeitwa Origenis aliyezaliwa mu mwaka 185 kisha kuzaliwa kwa Kristu anaandika : „Sikia, basi, maondoleo ngapi iko ndani ya Evangelio ya Kristu. Ya kwanza ni ile wakati tunabatizwa kwa maondoleo ya zambi…Kisha ni ile neno anasema Mtume Yakobo: “*mutu wa kwenu amekuwa ugonjwa? Aite wazee (wapadri) wa kanisa; nao waombe juu yake, na kumupakaa mafuta kwa jina la Bwana. Na kule kuomba kwa imani kutaokoa mugonjwa yule, na Bwana atamusimamisha; na kama amefanya zambi, atasamehewa*“. Kwa hivi Origenis anaandika ya kama hii Fumbo ya Kupakaa mafuta inaondoa zambi.

Askofu Serapion wa muji Thimueo, aliyezaliwa mu mwaka 300, kisha kuzaliwa kwa Kristu, aliandika kitabu cha sala mbalimbali (Efkhologion),. Ndani ya hii kitabu muko sala mbili zinatitwa : *Sala ya kupakaa wagonjwa mafuta, ao kwa mukate ao kwa maji..”*

Mtakatifu Yoane Krisostome, aliyezaliwa ku mwaka 345 anasema: “Hapana paka Ubatizo inaleta usamehe wa zambi, lakini na mafumbo mengine yale yanaifwata, sawa anasema vilevile na Mtume Yakobo”. Hapa Mt. Yoane anasema ya kama na Fumbo ya Kupakaa mafuta inaleta usamehe wa zambi.

Ku mwisho tunaweza kusema ya kama hii ni Fumbo Takatifu. Inaleta uponyesho wa mwili na usamehe wa zambi kwa ushuhuda wa Mtume Yakobo.

## MAFUNDISHO JUU YA UBIKIRA WA MARIA MZAZI-MUNGU

Kanisa ya papa inamutukuza kabisa na zaidi Mzazi-Mungu Mtakatifu Kamili mpaka kushusha utukufu wa Mwana wake Bwana Yesu Kristu. Mkubwa ya Waprotestants, Martin Luther, sababu alitaka hii kushusha masifu ya Mzazi-Mungu alifika mbali ya hii mambo, alikataa ubikira wake, kwani alifafanusha namna ingine mistari ya Maandiko Takatifu. Tena Waprotestants wanakataa usujudu wake, maombezi yake, miujiza yake, picha yake na jina lake “Theotokos” nikusema Mzazi –Mungu ao Mama wa Mungu.

Makundi ya waprotestants wote wanakataa ubikira ya Mzazi-Mungu na wanasadiki ya kama kisha kuzaa Kristu Maria alizaa watoto wengine na mume wake Yosefu. Wanatwaambia mistari yanasema “*ndugu*” za Kristu. Tazama ni hii mistari : Matayo 12,46:” *Wakati alipokuwa akisema na makutano, tazama, mama yake na ndugu zake wakasimama inje, wakitaka kusemezana naye”*. Tena: “Marko 6,3-7 na Matendo 1,14.

Sisi tunawajibu hivi: Neno “ndugu” iko na maana kubwa katika Maandiko Takatifu. Maana yake haina paka “ndugu”, lakini iko na mwipwa na muviala. Kwa mufano Loti anaitwa ndugu ya Abrahamu, lakini huyu ni mwipwa yake (Mwanzo 14,14). Yakobo anaitwa ndugu, lakini ni mwipwa, muyomba yake ni Labani (mwanzo 27,43 na 29,15). Watoto ya Kisi wanaitwa wa ndugu, lakini ni waviala ya watoto wanawake wa Eleazari (1 Mambo ya Siku 23,21-22). Hapa ni umoja wao katika kizazi kimoja. Hii neno “*ndugu*” kwa sababu mu lugha ya kiebrania na lugha ya kiaramaika hakuna neno “ *muviala* “. Na majina ingine ya muviala wanaisema hivi : *mwana wa muyumba*, ao *mwana wa ndugu ya mama*”. Lakini *muviala* ni ndugu. Basi, paka na maneno ingine pembeni tutaweza kujua kama huyu mutu ni muviala ao mwana ao ndugu ya mutu mwingine.

Kwa hii mambo ya „ *ndugu*“ za Kristu tunasema hivi : Hii neno „*ndugu*“ iko na maana mingi. Kwa sababu, kama walikuwa wandugu ya Yesu katika mwili, sababu gani hawakuandikiwa ya kama ni wana wa Mzazi-Mungu, lakini anandikiwa paka Yesu Kristu? Mtume Marko anasema (6,3): „Huyu si seramala mwana wa Maria, na ndugu ya Yakobo na Yose, na Yuda na Simoni? Juu ya nini hawa hawakuitwa ndugu za Yesu na watoto wa Mzazi-Mungu, ila tu Yesu?

Askofu wa Roma jina lake Igisipos, aliyeishi katika miaka 110-180 anatupatia ushuhuda juu ya ndugu za Kristu : « *Kisha kufa kwa Yakobo, askofu wa kwanza wa Yerusalema, kulifwata Simeoni mwana wa Klopa, aliyekuwa mwipwa wa pili wa Kristu* ». Hapa tunapata ushuhuda tangu mwanzo ya karne ya mbili ya kama Simeoni, Yakobo na wengine „*wandugu* „ wa Kristu walikuwa watoto wa Klopas, ndugu ya Yosefu, mulinzi wa Bikira Maria. Nikusema hawa wandugu wa Kristu walikuwa wepwa wa Kristu na watoto wa Kleopa. Kwa hivi, Yakobo, Simeoni, Yuda na Yose walikuwa waviala wa Kristu, hapana „ *ndugu*“ zake watoto wa mama yake Maria.

Tena tuko na ushuhuda ingine ile inatoka kwa askofu wa Roma, jina lake Igisipos, aliyeishi mu mwaka 110-180. Huyu anaandika hivi : « *Kisha kufa kwa Yakobo na mateso mengi, askofu wa kwanza wa Yerusalema, Simeoni alimupiana, mwipwa wa Yesu Kristu na mtoto wa Kleopa, ndugu ya Yosefu.* » Hapa Igisipos anasema ya kama wale wanaitwa ndugu za Kristu walikuwa waviala yake, kwa sababu walikuwa watoto ya Kleopas, ndugu ya Yosefu.

Tena askofu wa Aleksandria, jina lake Klimis (150-211) anasema neno lingine. Mtume Yuda anaanza hivi barua yake, ile iko ndani ya Agano Jipya : "*Yuda, mutumishi wa Yesu Kristu, ndugu wa Yakobo…*". Kama huyu alikuwa ndugu wa Kristu na mama moja na baba moja, juu ya nini anaandika kwa ajili yake mwenye : « *mutumishi wa Yesu Kristu*? »

Ushuhuda ingine tuko nayo inatoka kwa mwandishi mkubwa na théologien wa kanisa yetu, jina lake Origenis. Huyu aliishi mu miaka 185-250 kisha kuzaliwa kwa Kristu. Huyu anaandika ya kama Yosefu alikuwa amekwisha kuzaa watoto wake na muke wake aliyekufa mbele ya kuishi na Bikira Maria. Hakuunga ndoa na Bikira Maria, kwani alikuwa mulinzi wake. Mama Maria alikuwa Bikira mu uzima yake yote. Tazama ushuhuda yenyi kutoka kwa mapadri watakatifu wa zamani wa Kanisa yetu:

Mtakatifu Athanasios 295-402 patriarchi mkubwa wa Aleksandria anaandika hivi : "*Na huyu Maria alikuwa Mzazi wa Mungu na Bikira daima*".

Mtakatifu Epifanios, askofu wa Kisanga Kipro (313-402) anaandika hivi : *"Hakupatana naye katika mwili, hata mbele ya kuzaa Kristu, hata kisha kuzaa Kriostu, lakini alibaki mtakatifu na safi kamili"*.

Mtakatifu Grigori askofu wa Nisa (335-394) anaandika hivi : „*Sawa vile karatasi ni safi na yasipo kuandikiwa, vilevile na Huyu alikuwa Bikira, mtakatifu, bila kupatana na mwanaume...*"

Mtakatifu Augustino (354-430) anaandika hivi: "Alipata mimba na alikuwa Bikira, alizaa na alikuwa Bikira, na kisha mu uzima yake alikuwa bikira..."

Mtakatifu Basile mkubwa (330-379) aliandika hivi : "*Waaminifu wetu hakuna namna ya kusikia ya kama Mzazi-Mungu alikuwa Bikira...*"

Mtakatifu Yoane Damaskino (645-750) anaandika hivi : " Basi, alibaki Bikira na kisha kuzaa kwake Huyu aliye Bikira daima, na hakupakana na mume mpaka mwisho ya uzima yake.."

Kwa hivi, sisi waortodokse tunapaswa, bila shaka, kufwata hii ushuhuda ya Mapokeo yetu Takatifu na kusadiki ya kama Mama Maria alikuwa Bikira mu uzima yake yote.

Agano Jipya paka mara moja inataja Maria bibi ya Yosefu mu mustari wa Matayo 1,20 mbele ya kuzaliwa Yesu. Ile wakati Yosefu, kwa sababu alikuwa mutu wa haki na hakutaka kumupatisha Bikira Maria haya mele ya watu, akakusudia kumwacha kwa siri. Lakini malaika wa Mungu akamutokea kwa ndoto na kumwambia amuchukue Maria nyumbani mwake kuwa muke wake , kwa sababu alipata mimba ile kwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Lakini, pa fasi ingine, mara makumi mbili na tisa, anaitwa „Mama wa mtoto", hivi Waevangelizaji wote wanatuonyesha ya kama Bikira Maria hakuwa muke wa Yosefu, wala mbele, wala kisha kuzaa Kristu.

Mbele ya kutoa uzima yake juu ya Musalaba, Kristu aliita *mwanafunzi wake Yoane juu ya kumuchukua nyumbani mwake Mama yake yake. Alimwambia hivi : „Mwanamuke, tazama mwana wako! Halafu akamwambia yule mwanafunzi: Tazama mama yako. Na kutoka saa ile mwanafunzi yule alimupeleka kwake*". (Yoane 19,27). Sisi tunauliza Waprotestants : Kama Mzazi-Mungu alikuwa na watoto wengine, juu ya nini Kristu hakumuache kwa ndugu zake wengine, lakini alimuacha kwa mwanafunzi wake?

Wakati Malaika Gabrieli alimutokea ku muji wa Nazareti juu ya kumuletea habari njema, alimwambia: "*Salamu, Mujaliwa neema…Mubarikiwa katika wanawake*" (Luka 1,28). Maria alishituka kwa maneno ya Malaika, hata kama hajue mume, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu atazaa Mwana wa Mungu (Luka 1,29-35). Huyu, basi, Isaya alimuita Bikira*: "Tazama bikira atapata mimba naye atazaa mutoto mwanaume, na ataita jina lake Emanueli*" (Isaya 7,14). Nabii Daudi alimuita *Mama Bikira Mufalme anayesimama kuume kwa Bwana* (Zaburi 44,9). Ezekieli anamuita *Mulango ya kufungwa* (Ezek.44,1-3), Musa anamuita *Mungazi ya Yakobo* na yeye Mungu anashuka duniani. Halafu, namna gani aliharibu ubikira yake? Huyu alijua ya kama alizaa

Mungu na kwa hivi alikuwa Mama wa Mungu, namna gani ataitika kupana na mwenye haki muzee Yosefu?

Kufwatana na Maandiko Takatifu (Mwanzo 2,23) tunajua ya kama Eva aliumbwa toka mwili wa Adamu, bila Adamu kupatana na mwanamuke. Basi, kama Mungu aliumba Eva bikira na kumuita mwanamuke, namna gani Waprotestants wanasadiki ya kuwa Maria aliolewa, kwa sababu aliitwa mara moja muke wa Yosefu? Malaika Gabrieli alimwita na maneno haya: "*Mubarikiwa katika wanawake"*, nikusema alimwita *mwanamuke*, sisi tunapashwa kujua ya kama neno "*mwanamuke*" maana yake haiko paka ule anaolewa, lakini ni asili ya wanawake wote. Na sawa vile Adamu, bila kupatana na mwanamuke mumoja, alizaa mwanamuke kwa ubikira wa mwili wake, vilevile na Bikira Maria, bila kupatana na mume alizaa kwa uwezo wa Roho Mutakatifu Adamu mupya, Mwokozi wa dunia. Unabii juu ya ubikira wa Mzazi-Mungu iko ndani ya kitabu cha Mwanzo 3,15, kule tunasoma : *"na nitatia uadui katikati yako na mwanamuke, na katikati ya uzao wako na uzao wake"*. Hapa Mungu anasema ya kama ataweka uadui katikati ya shetani na mwanamuke, Maria Mzazi-Mungu, na katikati ya shetani na Yesu. Kisha, Yesu atavunja kichwa cha shetani, lakini shetani atamupiga chini ya muguu yake, nikusema ni lufu ya Kristu pa Musalaba. Mapadri wetu watakatifu wanasema ya kama Kristu aliitwa „*uzao wa mwanamuke*" (Mwanzo 3,15), kwa sababu hakuzaliwa toka mbego ya mwanaume, lakini toka uwezo wa Roho Mutakatifu na tumbo la Mzazi-Mungu Bikira Maria.

Waprotestants wanasadiki ya kama Mama Bikira Maria, alipatana katika mwili na mwenye haki muzee Yosefu kisha kuzaliwa kwa Kristu. Hii mawazo yao haiko ya kweli, kwa sababu wakati Malaika Gabrieli alimutokea na kumupasha habari ya kama atazaa mtoto, binti Maria alishituka na alimuuliza Malaika : " *Neno hili litakuwa namna gani, kwani mimi ni bikira*? (Luka 1,34). Tena mu Luka 1,27" tunasoma: „*Kwa bikira mumoja aliyekuwa muchumba wa mutu aliyeitwa Yosefu, wa uzao wa Daudi. Na jina la yule bikira lilikuwa Maria*" Hapa si tunaona ya kama Maria alikuwa bikira na muchumba, hapana bibi ya Yosefu. Tena nabii Isaya alisema unabii moja juu ya Bikira Maria: " *Tazama bikira atapata mimba naye atazaa mutoto mwanaume, na ataita jina lake Emanueli" (I*saya 7,14). Ile wakati kama mwanamuke mumoja anapata mimba ya bwana mwingine, bwana yake anapashwa kumufukuza inje ya nyumba yake na watu wengine watamuuwa katikati ya muji yao. Yosefu, wakati aliona ya kama Maria alikuwa na mimba, bila kujua ya kama aliipata kwa uwezo wa Roho Mutakatifu, aliwaza namuna ya kumutosha kwa siri inje ya nyumba yake. Alikuwa mtu mwenye haki na hakupenda kumupatisha haya na atendewe vibaya. Wakati malaika alimwaambia ya kama huyu mtoto atazaliwa kwa uwezo wa Roho Mutakatifu, namna gani Yosefu ataweza kupatana na Maria wakati yeye alijua ya kama huyu Maria atazaa Mwokozi wa dunia na atakuwa mama wa Mungu wake? Mama Maria alikuwa bikira mbele ya kuzaa, wakati alikuwa na mimba, na kisha kuzaa. Ndio maana anaitwa „*mujaliwa neema*" (Luka 1,28) na *"mubarikiwa katika wanawake"* (Luka 1,28) *na mwenye heri katika vizazi vyote* (Luka 1,48). Elisabeti wakati alikutana na Maria Mzazi-Mungu alimwaambia: „*Wewe umebarikiwa kuliko wanawake wengune, na mutoto wa tumbo lako amebarikiwa. Mimi ni nani, hata mama wa Bwana wangu aje kwangu kunitembelea?* (Luka 1,42-43). Sisi Waorthodoksi tunamutukuza Mzazi-Mungu sawa vile alimusalimia na kumutukuza Malaika Gabrieli wakati alimuleta habari ya kuzaliwa kwa Mwana wa Mungu (Luka 1,28-29).

Waprotestants wanasema ya kama Bwana Yesu alimuzarau mama yake. Wanasema ya kama ku ndoa ku muji wa Kana alimufokea mama yake na maneno haya: *„Mwanamuke, nina nini nawe? Saa yangu haijakuja bado"* (Yoane 2,4).

Sisi tunawajibu hivi : "Kama Bwana Yesu alimufokea mama yake, huyu hakuweza kuwaambia watumishi : "*Fanyeni lo lote atakalowaambiai*…"(Yoane 2,5). Kama kweli mwana wake alimuzarau, Mama yake alipashwa kufunga kinywa chake na hakupashwe kuwaambia watumishi wa ile nyumba wafanye vile Yesu atasema. Mambo ya ajabu ni hii : Mwana wake anatimiza mapenzi yake na anageuza maji kuwa vinyo. Mzazi-Mungu alijua ya kama Mwana

wake anaweza kufanya miujiza, ni kwa hii mambo alimwaambia na unyenyekevu na heshima: "*Hawana vinyo tena* ". Yesu alipenda kuonyesha mbele ya watu wote umungu wake na uwezo wake ya kama ataanza kufanya miujiza na alama zingine za ajabu duniani sababu ya kutukuza Baba yake wa mbinguni, ndio maana alimwaambia mama yake : "„*Mwanamuke, nina nini nawe?"* Nikusema : Kitu gani iko katikati yetu, kwani tangu sasa mimi nitatumika na uwezo wa Baba yangu wa mbinguni. Saa yangu ya kufanya miujiza haijafika bado na kuonekana mbele ya watu sawa Mwokozi wao. Yesu alisema : "*Saa yangu haijakuja bado*". Tangu ile saa alianza kufanya miujiza. Lakini hakupenda Mama yake amuonyeshe afanye miujiza, kwani aliongojea amri toka kwa Baba yake wa mbinguni.

Hii maneno alimwambia mama yake haionyeshe ya kama Yesu alimuzarau mama yake. Alimutukuza, alimutii na alifanya miujiza tokea ile ndoa. Hivi, Kristu alionyesha ya kama alimutukuza na kumuheshimu mama yake.

Waprotestants" wanashangaa kwa sababu sisi Waorthodoksi tunamuita Mama Maria "**Mtakatifu kamili**". Mtume Paulo anasema: "*Kama tukiteswa pamoja naye, ili tutukuzwe pamoja naye vilevile".* (Waroma 8,17). Lakini nani aliteswa kuliko watu wote, ni paka Maria Mzazi-Mungu, wakati alisimama karibu ya Musalaba na alimuona mtoto yake akiteswa kabisa? Mtakatifu Simeoni mubebaji-Kristu alimwambia Mzazi-Mungu : "*Ndiyo, upanga utakuchoma roho yako mwenyewe ili mawazo ya mioyo mingi yafunuliwe"* (Luka 2,35). Hapa inaonekana uchungu wake mingi alisikia pakuona Mwana wake Yesu Kristu Musalabani. Basi, kama Maria aliteswa kabisa na alipenda watu wa dunia yote na alibaki bikira na Safi kabisa na tumbo lake lilikuwa nyumba ya Mungu, namna gani hatatukuzwa mbinguni karibu ya Mwana wake na namna gani atakuwa chini ya utukufu ya watakatifu wengine?

Tena Waprotestants wanakataa maombezi ya Mzazi-Mungu na wanaleta hii mustari: " *Kwa sababu Mungu ni mumoja tu, na mupatanishi kati ya Mungu na watu ni mumoja, yule mutu, Kristu Yesu"* ( 1 Timotheo 2,5). Kwa wao wanasema ya kama paka Yesu ndiye mupatanishi kati ya Mungu na watu, kwa hivi maombezi ya Mzazi-Mungu haina ya lazima.

Hii mustari inasema juu ya Mupatanishi kati ya Mungu na watu, hapana kati ya Yesu na watu. Ni kweli, hakuna Mupatanishi kati ya watu na Baba ila Bwana Yesu Kristu. Paka Yeye peke yake alitoa mwili wake kuwa sadaka ya wokovu wa dunia. Wakati sisi tunamuomba Mzazi-Mungu, tunamuomba atuombee kwa Mwana wake sawa Mama yake juu ya kutusaidia na kutuokoa. Kwa hivi Mzazi-Mungu tunamutumia sawa mupatanishi kati ya Yesu Kristu na watu na hapana kati ya Mungu na watu, kwa sababu pa hii fasi Mupatanishi ni paka moja tu, nikusema Mwokozi wa watu, Bwana Yesu Kristu. Kwa hivi, maombi yetu kwa Mzazi-Mungu ni hii: "*Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu Maria, utuokoe*". Nikusema: *Ee Mzazi-Mungu wetu umuombe Mwana wako wa pekee atuokoe.* Mu lugha la kigreki neno *Kuokoa* iko na maana mengi. Sawa ninaokolewa toka majaribu, toka mateso fulani, toka sikitiko. "*Utuokoe*" si kusema "*Utusamehe zambi zetu*", lakini maana yake ni hii: "*Utuombee kwa Mwana wako atuokoe*".

Heshima yetu kwa Mzazi-Mungu haipite ile heshima tunaheshimu nayoYesu Kristu, Mwana wake, kwa sababu huyu Yesu alimutakasa, alimutukuza na alimufanya kuwa mama yake. Mzazi-Mungu haokoe. Hivi anasema huyu pa mustari ya Luka 1,46-47 : "*Moyo wangu unamusifu Bwana, na roho yangu inamufurahia Mungu, Mwokozi wangu".* Kwa hivi Mama Maria anasema ya kama Bwana Yesu Kristu, mwana wake, ni Mwokozi yake.

Waprotestants wanakataa kumwita Mama Maria Mzazi-Mungu, kwa sababu wanasema ya kwamba hii neno halipatikane ndani ya Maandiko Takatifu.

Ni kweli neno ***Mzazi-Mungu*** ao mu kigreki **Theotokos** halipatikane ndani ya Biblia. Lakini iko ndani ya Mapokeo Takatifu na ndani ya vitabu vya wmpadri wetu tangu karne ya ine. Sisi tunajua toka Maandiko Takatifu ya kama Kristu, hakukuwe paka Mungu ao paka mutu, lakini alikuwa **Mungu** na **mutu** pamoja. Sisi waorthodoksi kama tunasema ya kama Maria ni Theotokos (Mzazi-Mungu) hatuwaze ya kama huyu Mama ni chemchem ya uzima wa Mwana wake. Hii

itakuwa matusi na kumuzarau Kristu. Mama Maria anaitwa Theotokos (Mzazi-Mungu), kwa sababu alizaa Kristu aliye Mungu na Mutu. Huyu Kristu mojamoja anawaambia Waebrania: „*Kweli, kweli ninawaambia ninyi, mbele Abrahamu hajaliwa, mimi nilikuwako*“ (Yoane 8,58). Kristu, sawa mutu ile wakati alikuwa na umri wa miaka 30, lakini Abrahamu aliishi mbele ya miaka elfu mbili. Hii maneno ya Kristu, inataka kutuonyesha asili yake ya umungu.

Mukutano Ikumeniki ya tatu ku mwaka 430, kwa sababu ilikua na ushuhuda mingi ya Watakatifu wa zamani, ilijua ya kama Mama Maria eko kweli Theotokos (Mzazi-Mungu) ilikamata mpango ikamupa hii jina **Theotokos**, kwa sababu alizaa Yesu Kristu, Mungu na Mutu pamoja.

## MAFUNDISHO JUU YA MAOMBEZI YA WATAKATIFU

Waprotestants wanakataa MAombezi na saidio ya sala ya Watakatifu. Tena wanakataa kusujudu mbele yao. Waprotestants waanandika katika vitabu vyao ya kama hawaombe kwa Watakatifu, hawatumainie Watakatifu, hawala na ma fêtes ya Watakatifu. Tena wanasema hivi : Zamani wakati wa Mitume watu pamoja na jamaa zao na watoto wao waliitwa ***watakatifu.*** Na hii wakati wa sasa wale watu wanaishi na toba na wanamuamini Kristu sawa Mwokozi wao ni ***watakatifu***. Wale watu wa zamani waliokolewa kwa saidio ya Kristu, na hawa wanaokolewa kila siku na wale wataokolewa mpaka mwisho ya dunia, hawa wote wanaitwa ***watakatifu***“

Paka kwa hii maneno yao tunawatambua ya kama hawafanye tafauti juu ya watakatifu. Wao kwa imani yao wanasadiki ya kama wataokolewa paka kwa imani. Wanasema hivi : *“ Paka imani inamupatanisha mutu kwa Mungu, ni ile inaleta utakaso”*. Tena, wanasema ya kama watakatifu hawana na haki ya kutuombea sisi kwa Mungu. Tena, wanaongeza kusema : *„Sisi tunaweza kuelekeza sala yetu paka kwa Mungu bila kupitia kwa watakatifu Fulani”*. Tena wanaongeza hii neno lingine tunajua : “ Kwa sababu Mungu ni mumoja tu, na mupatanishi kati ya Mungu na watu ni mumoja, yule mutu Kristu Yesu“ (1 Timotheo 2,5).

Sawa vile kuna umbalimbali kati ya nyota kufwatana na barua ya 1 Wakorinto 15,41: “*Kuna utukufu mumoja wa jua, na utukufu mwingine wa mwezi, na utukufu mwingine wa nyota; kwa sababu nyota moja ina utukufu mbalimbali na nyota nyingine*”, Vilevile kuna makundi mbalimbali na makao mbalimbali ya wenye haki kufwatana na mustari hili : *“Katika nyumba ya Baba yangu kuna makao mengi”* (Yoane 14,2).

Neno “**mtakatifu**” liko na maana : safi, kimungu, muheshimiwa, mwenye kuishi mbali ya dunia na kujitoa kwa kazi ya Mungu. Tena Maandiko Takatifu inaita **watakatifu** wale watu walifufuka toka makaburi kisha Kusulubiwa kwa Kristu: *“Makaburi yakafunguliwa, na miili mingi ya watakatifu waliokwisha kulala ilifufuliwa”* (Matayo 27,52). Tena watakatifu ni wale wanawake walitii waume wao, sawa Sara (1 Petro 3,5), tena na wale Wakristu walikuwa mu muji Roma (Waroma 1,7) na mu muji wa Korinto (1 Wakorinto 1,2), mu muji Efeso, Filippi na fasi ingine.

Kwa sauti ya Mtume Paulo, anaitwa **mtakatifu** ni ule mutu anayependa kupendezwa kwa Kristu. (barua ya kwanza kwa Wakorinto 7,32-34). Nikusema huyu mtu anayeishi uzima yake yote paka na usafi wa roho na wa mwili, na matendo ya mapendo, na sadaka kwa Kristu.

Tena hii jina “**Mtakatifu**” ulipewa na kwa mashahidi wa Kristu, kwa sababu shahidi wa kwanza na wa kweli ni Yesu Kristu (Ufufuo 1,5), aliyekufa na mateso mengi wakati wa Pontio Pilato kama anavyosema Mtume Paulo kwa Timotheo ( 1 Timotheo 6,13). Kwa hivi, shahidi ni mwanafunzi wa Kristu, aliyetoa uzima yake sawa sadaka kwa kuimarisha imani ya Kristu.

Waprotestants, wanasema ya kama Watakatifu hawana na haki ya kutuombea saidio na wokovu . Sisi tunawajibu hivi: “Watakatifu wakati waliishi waliomba kwa Mungu juu ya watu wengine. Abrahamu aliombea Abimeleki, mufalme ya Gerari na Mungu alimuponyesha yeye na bibi yake na wajakazi wake (Mwanzo 20,7 na 17). Ku Kitabu cha Kutoka 8,17-18) Mufalme ya

Misri Farao anamuomba Musa afanye sala juu ya kuuwa chawa. Watu wa Israeli wanafanya ngombe ya zahabu na wanamuomba ngombe sawa mungu wao. Mungu anasirika na anataka kuwaua. Anakuja katikati Nabi9 Musa na katika sala yake alischusha kasirani ya Mungu (Kutoka 32,1-14). Mu Kitabu Matendo ya Mitume (12,5) tunasoma: „Basi Petro alilindwa katika kifungo; lakini kanisa walimwombea kwa Mungu pasipo kuchoka“ Wakristiani ya Yerusalema walijua ya kama Petro alikuwa na uwezo katika sala yake, lakini sasa, wakati alikuw andani ya kifungo wanaombea kwa Mungu juu ya wokovu wake. Mtume Pauloa naandika hivi kwa Timotheo (barua ya kwanza 2,1-2): „basi ninaonya mbele ya maneno yote, kuomba, na kusihi, na kuombea, na kushukuru kufanyike kwa ajili ya watu wote; kwa wafalme, na kwa wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya kimya na salama, katika utawa wote na upole“ Kisha anaongeza: „kwa sababu hili ni zuri, na la kukubaliwa mbele ya Mungu Mwokozi wetu“. Hii fundisho safi ya Agani Jipya inaharabisha mawazo ya Waprotestante na inatushauria sisi wote tufanye mapaswa yetu ya kuombea kwa watu wengine na wengine kwa sisi, kwa sababu „Kuomba kwake ,mwenye haki kuna faida sana, kama akiomba kwa bidii“. (Yakobo 5,16).

*Tena tutaongeza na mustari ingine ya barua ya Mtume Paulo kwa Waroma ya (15,30-32): "Na ninawasihi ninyi, ndugu, kwa Bwana wetu Yesu Kristu, na kwa mapendo ya Roho, mudumu pamoja nami kwa maombi yenu kwa Mungu kwa ajili yangu, niokolewe kwa watu wasioamini katika Yudea; na utumishi wangu nilio nao katika Yerusalema ukubaliwe kwa watakatifu; nipate kuja kwenu kwa furaha, kwa mapenzi ya Mungu, nipate kupumzika pamoja nanyi*". Hapa Mtume Paulo anawaambia wakristu wafanye sala juu ya kumusaidia kwa hii kazi yake, nikusema: Ku mwanzo juu ya kuokolewa ku mikono ya Waebrania, ya pili juu ya kukubalisha hii mafundisho yeye anawafundisha wakristu wa Yerusalema, na ya tatu sababu Mungu amusaidie kusudi atembelee wakristu wa Roma na kupata kupumzika karibu yao.

Wakristu walijuwa ya kama walikuwa mapashwa ya kumuomba Mungu juu ya watu wengine na juu ya Mitume. Musome hii mistari : "Matendo 12,5-12, Waefeso 6,18-20, Filimoni 22, 2 Watesalonika 3,1-2 na ingine mingi.

Wakati wa mateso yake, Bwana Yesu Kristu alimuomba Mungu Baba yake juu ya kumupa nguvu. Tazama inasema nini Maandiko Takatifu : *„Malaika toka mbinguni alimutokea, akamupa nguvu"* (Luka 22,43). Kama Kristu alikuwa na lazima ya sala, sala ngapi na saidio ngapi ya watakatifu sisi tuko nayo lazima kwa Bwana Yesu Kristu, kwani Huyu anatupa sisi mufano juu ya maombezi?

Waprotestants wanatujibu ya kama na wao wanaombea watu wengine, Watakatifu wamekwisha kufa na kupotea milele.

Hii jibu na mafundisho yao ni matukano, kwa sababu *"Mungu si Mungu wa wafu, lakini wa walio hai*" (Matayo 22,32) Na Marko 12,26-27 na Luka 22,37-39).

Bwana Yesu pa fasi ingine (Yoane 5,24) anasema: "*Kweli, kweli, ninawaambia ninyi, yeye anayesikia neno langu na kumwamini yeye aliyenituma ana uzima wa milele; hafiki kwa hukumu, lakini amepita kutoka mauti kuingia uzima*". Na pa fasi ingine (Yoane 11,26): "*Na kila mutu mwenye uzima na kuniamini mimi hatakufa hata milele"*. Basi, ni lazima kujua na Waprotestants wote ya kama wale wanaamini Mungu hawatakufa milele na hawatapita kwa hukumu yake, lakini wataishi milele.

Kwa sababu wao ni wa milele, wale watu walimufurahisha Kristu kwa uzima yao na walipata utukufu wa milele, kizuio gani weko nayo ya kumuomba Mungu juu yetu sisi tulio tena duniani? Mtume Paulo, wakati alikuwa tena pa dunia alipiga magoti, aliombea sana Wakristu (Waroma 1,8-10). Waefeso 3,14-16-17. Waefeso 1,15). Sasa Watakatifu waliingia mu Paradizo, wanakaa kimya. Halafu, namna gani hawataomba kwa Mungu? Kazi ya kuombea watu wengine kwa Mungu ilisimama? Ao mapendo yao kwa jirani zao yao iliisha. Hakuna mapendo ingine ndani ya roho yao? Ao Mungu ni mbali yao na hakuna namna kusikia maombi yao ao Mungu anakataa maombi yao? Hapana, haina vile. Kweli, Mtume Paulo na watakatiofu wote

wanamuomba Mungu juu ya dunia yote. Tazama ushuhuda ingine (Ufunuo 5,8): "*Hata alipotwaa kile kitabu, wale nyama wane na wale wazee makumi mbili na wane, wakaanguka mbele ya mwana-Kondoo, kila mumoja wao ana kinubi na machupa ya zahabu yaliyojaa uvumba ndiyo ni maombi ya watakatifu*". Hapa tunapata ushuhuda ya kama wale weko mbinguni wanayuombea sisi tuko hapa duniani. Mustari ingine ya Ufunuo 6,9-10) inatuonyesha hivi? *: "Na wakati alipofungua muhuri wa tano, nikanona chini ya mazabahu nafsi zao waliouawa kwa ajili ya Neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao. Wakalia kwa sauti kubwa, wakisema: Ee Bwana, Mutakatifu, mwenye kweli, hata wakati gani hukumu, wala kupatia haki damu yetu kwao wanaokaa juu ya dunia"?* Hapa anaonyesha roho zilichinjwa kwa ushuhuuda wa Kondoo (Kristu) wanaomba kwa Mungu juu ya kuhukumu wale watu wa hii dunia walikimbia mbali yake. Lakini mu mustari ingine (Ufunuo 8,3-4) tunasoma ya kama maombi ya watakatifu, hapana paka yanafanyika, lakini yanamufikia Mungu katika Malaika zake.

Waprotestants hawawezi kutujibu, lakini na upumbafu mingi wanasema ya kama Watakatifu hawajue kazi gani inafanyika hapa duniani, wala hawasikie maombi yetu. Lakin, sisi tunawajibu na mistari ya Maandiko Takatifu ya kama Watakatifu wanaona mafaa mingi vitu vyote vinafanyika hapa duniani. Bwana Yesu anatuhakikishia ya kwamba Abrahamu alitamani kuona ile siku ya Kufika Kristu duniani na anaongeza katika mustari ya Yoane 8,56): "*Akaiona, akafurahi*". Nikusema toka ile fasi alikuwa aliona ya kama Kristu alikuja duniani na alifurahi. Tena mu Mufano ya feza iliyopotea Kristu alitufundisha *: "Kuna furaha katikati ya Malaika za Mungu juu ya mwenye zambi mumoja anayetubu"* (Luka 15,7-10). Ku Mufano ya Mutajiri na maskini Lazaro Abrahamu alimwambia mutajiri:; "*Mwana, kumbuka ya kuwa ulipokea vitu vizuri katika maisha yako, kama vile Lazaro alivyopokea vitu vibaya"* (Luka 16,25). Hapa tunaona ya kama Abrahamu bila kuwa pa ile fasi, alijua uzima hapa duniani ya ule mutajiri na ya maskini Lazaro. Tena ku mustari ya Matendo 5, 1-11 inaandikwa ya kama Anania na bibi yake Safira walikamata mpango ya kuuzisha shamba yao, kisha wakasema uwongo kwa Mtume Petro ya kama waliiuzisha ku bei fulani , lakini wakaficha feza ingine juu ya maisha yao ya kuonekana mbele ya wakristu ya kama wao ni waaminifu wa kweli. Lakini Mtume Petro, bila kuwa pamoja nao wakati waliuzisha lile shamba, paka na mwangaza ya Roho Mutakatifu, alijuwa ubaya yao, aliwahamakia, aliwafinga na kisha wote wa wili walikufa.

Wazo lingine la ovyo la Waprotestants ni hili: "Wanasema ya kama maombezi ya Watakatifu juu ya wokovu wetu haina lazima kwa sababu Mungu ni Mwenyezi na anaweza kutusaidia na kutuokoa, bila saidio ya wengine". Sisi tunawajibu hivi: Ni kweli Mungu anaweza kutusaidia bila saidio ya wengine, ni kwa sababu ya hii maana kunakuwa na hii neno : "*Na mupatanishi katikati ya Mungu na watu ni mumoja, yule mutu Kristo Yesu*" (1 Timoth.2,5). Lakini maombi ya Watakatifu haiharabishe maombi na saidio ya Kristu. Mwenye kuokoa ni Kristu, lakini Watakatifu wanamuomba Kristu kwa ajili ya wokovu wetu bila hii wokovu kutoka kwa watakatifu. Kwa hivi na sisi Waorthodoksi hatuabudu watakatifu na malaika sawa Mungu. Tunawasujudu sawa ndugu zetu wakubwa na rafiki za Mungu. Tena Mungu tunamwabudu kwani yeye ni Mungu wetu na Muumba wetu .

Ni kweli, Kristu ni Mwokozi wa watu wote, lakini, juu ya kuleta wokovu kwa watu anatumia watu fulani sawa wasaidizi. Kwa mufano, sisi hapa duniani tunapata saidio ya wokovu wetu kwa watu wengine wale waliuawa juu ya Habari Njema ya Kristu. Yesu anasikia maombezi yao na kwa ajili yao, anatualika na sisi mu njia ya ukweli na ya wokovu.

Kwa hivi, Kristu ni Mupatanishi wa pekee kwa wokovu wetu na waombezi ni watakatifu wote. Bila upatanisho wa Kristu, hakuna na maombezi ya Watakatifu. Maombi ya watakatifu iko na nguvu kabisa mbinguni kwa Mungu, kwa sababu weko na uwezo mbele yake, kwa mateso na mahangahiko wanapata hapa duniani kwa mapendo ya Kristu.

## MAFUNDISHO JUU YA KUSUJUDU PICHA ( Ikona) ZA WATAKATIFU NA MUSALABA WA KTISTU

Waprotestants wanasema ya kama sisi waorthodoksi tunaabudu picha za Watakatifu wetu na Mifupa yao. Halafu, sisi tunawajibu ya kama hatuwaabudu, lakini tunawasujudu, tunaabudu paka Mungu. Uabudu ni paka Kwake.

Waprotestants wanaleta mustari ya kitabu cha Kutoka 20,4-5 *: « Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala kitu kilicho mbinguni juu, wala duniani chini, wala ndani ya maji chini ya dunia; usijiname mbele yao kuzitumikia; kwa kuwa mimi Bwana Mungu wako ni Mungu mwenye wivu; nikipatiliza wana uovu wa baba zao, hata kizazi cha tatu ao cha ine cha wale wanaonichukia* ». Hapa Nabii Musa haseme juu ya picha, lakini anasema juu ya sanamu, nikusema ya vitu vyasipo na uzima, bila kuishi, bila kuonekana. Lakini picha ni vitu vya watu waliyoishi na walionekana. Basi, hapa sheria ya Musa inakataza sanamu, hapana picha ya Kristu, ya Mzazi-Mungu na ya Watakatifu wetu. Maana ya mu mustari : " *kwa kuwa mimi Bwana Mungu wako*" nikusema ile wakati taifa ya Waebrania iliishi katikati ya mataifa ya wapagano. Mungu alitaka kuchunga taifa yake juu ya kumuabudu paka Yeye peke yake. Kwa hivi aliwakataza kuabudu miungu ya mataifa ingine, kwani yalikuwa miungu ya uwongo. Miungu na sanamu ni mashetani. Nabii Daudi anasema ya kama : „ *Maana miungu yote ya watu ni sanamu; lakini Bwana aliumba mbingu"* (Zaburi (95) 96,5).

Tunasema ya kama Mungu anakataza kuabudu sanamu, lakini anaruhusu Waebrania kufanya malaika, nyuso, na kiti za zahabu ndani ya hema ya kumuabudu Mungu. Kwa hivi, kwa amri ya Mungu, ndani ya hekalu waebrania walifanya malaika Makherubi wawili ya zahabu na mabawa yao yakifunika kiti cha rehema, maana Meza Takatifu (Kutoka 25,17-19). Malaika Makherubi wengine wawili waliwekwa juu ya Vitakatifu ya Watakatifu ya Hekalu ya Solomono (Kutoka 25,23-28). Hivi vitu haviko vya kuabudu wala kuvisujudu. Lakini vinakumbusha kitu kizuri cha Mungu wa kweli.

Kwa sababu mutu hana paka na roho, eko na akili na mwili, ni lazima amukumbuke Mungu na vitu vya hii dunia. Kwa sababu Yesu Kristu alichukuwa mwili sawa sisi, bila zambi, tunaweza kufanya picha. Ile wakati ya Agano la Kale Mungu hakutwae mwili, haikuwezekana kuona uso wake. Lakini, tunafanya wa Yesu Kristu kwa sababu alichukua mwili na alikuwa na uso sawa wetu sisi. Kwa hivi, picha inaonyesha hali kimutu ya Yesu, ao ya Watakatifu wetu. Utukufu ya picha inatokea sababu ya ile mafundisho ya kwamba Yesu Kristu alikuwa Mungu kweli na mutu kweli na alikuja duniani na uso sawa mutu. Tena heshima yetu kwa picha ya mtakatifu fulani hatuilete ku muti ao ku rangi mbalimbali ya picha, lakini inaelekea ile uso yake. Ni vile tunafanya wakati tunabusu picha ya ndugu yetu mupendwa. Tunabusu picha ya wazazi wetu, lakini hii heshima inaelekea uso yao wazazi wetu, hapana rangi ao kartasi ya picha yao. Tunabusu picha ya watakatifu ao ya wandugu wetu kwa heshima na mapendo na sifa, hapana kartasi ao rangi. Hatusadiki ya kama hii picha iko takatifu itatuokoa ao ni Yesu Kristu. Mawazo ya hii namuna ni zambi na matusi kwa Kristu. Tunabusu uso wa mtakatifu fulani, mawazo yetu inapanda yulu tunamuwaza vile eko ndani ya Paradizo. Kwa hivi mtakatifu Basile anasema ya kama „ *Picha ni vitabu vya waaminifu* ". Ku mwaka 783, kisha kuzaliwa Kristu kulifanyika Mukutano kubwa ku Konstantinopoli, na hii Mukutano iliondoa hii ugomvi ya kusujudu picha na iliteswa Kanisa ya Kristu karibu miaka 130. Tazama mpango walikamata walikamata wale maaskofu juu ya Picha za Watakatifu : „ Kama waaminifu wanaona nyuso za Watakatifu pa picha zao, mapendo na heshima yao inaongezeka katika uzima yao, na mawazo yao inaelekea kwa ule mtakatifu. Tena tunabusu picha zao juu ya heshima, utukufu na mapendo, hapana juu ya kuwaabudu, kwani tunaabudu paka Mungu, Muumba wetu.. Huyu anayebusu picha ya Mtakatifu fulani hii usujudu inaelekea ule Mtakatifu aliye katika Paradizo, hapana ile lubao ao rangi".

Sababu tu ya kubusu picha za Watakatifu, Waprotestants wanatukombanisha kwa sababu sisi Waorthodoksi tunabusu na kuheshimu Musalaba wa samani wa Bwana Yesu Kristu. Wanasema Musalaba ni kitu kingine, na Kusulubiwa ni mambo ingine. Wanasema Musalaba ni kitu cha laana, kwa sababu juu yake palisulubiwa watu wabaya na wanyanganyi.

Sisi tunawajibu hivi : "Maandiko Takatifu inatwaambia hivi: "N*a mutu akiwa ametenda zambi inayopasa mauti, naye anauawa, nawe utamutundika juu ya muti"* (Kumbukumbu la Torati 21,22). Tena na mu mustari ya Wagalatia 3,13 tunasoma; "*Kristu alitukomboa kwa laana ya torati, akiwa alifanywa laana kwa ajili yetu, kama ilivyoandikwa*". Halafu, tunawauliza : Kweli Kristu ni ***laana*** kwa ajili yetu? Hakuna namna. Hapana! Maana ya hii maneno ni hii : "*Alifanywa laana kwa ajili yetu*" nikusema ***Kristu alichukua laana yetu na aliibadilisha kuwa baraka***. Kwa hivi, kama Kristu alifanywa kuwa ***laana*** kwa ajili ya wokovu wetu na alibadilisha hii laana kuwa baraka, juu ya nini Musalaba wake itabaki yenyi kulaaniwa na haitabadilishwa kuwa baraka? Kwa sababu Damu ya samani ya Kristu ilimwangika yulu yake, namuna gani Musalaba itabaki muti ya laana? Kama vitambaa na nguo za Mtume Paulo vilifanya miujiza (Matendo 19,12) juu ya nini Musalaba wa Bwana Yesu haina na Neema yake juu ya kufanya miujiza?

Alama ya Musalaba inaonekana hata katika Agano la Kale : kunyanyua kwa nyoka ya shaba jangwani kwa Musa katika muti mbele ya Waisraeli ( Hesabu 21,8) Tunajua ya kama katika safari yao ya kwenda katika inchi ya Palestina Waebrania wakati moja walikufaka kwa sababu waliwaumiza kwa nyoka ya sumu. Kwa amri ya Mungu, Musa aliweka katikati yao nyoka ya shaba juu ya muti. Wale watu waliumizwa kwa nyoka, wakati waliangalia ule nyoka ya shaba juu ya muti mara moja walipona. Huyu nyoka alikuwa alama ya ushindi ya Agano Jipya, lakini na alama ingine, Musalaba ya Kristu. Kwa hivi na Yesu Kristu mwenyewe anatwaambia: "***Na kama Musa alivyonyanyua nyoka jangwani, vivyo hivyo sharti Mwana wa watu anyanyuliwe, ili kila mutu akimwamini asipotee, lakini awe na uzima wa milele***" (Yoane 3,14-15).

Kwa hivi, Musalaba haina sasa alama ya haya na mafigo (laana), lakini ni chemchem ya uzima ya milele. Hakuna onyesho mnene ya Kristu ya mapendo Yake mbele yadunia ku Musalaba Yake, kwa sababu pa Musalaba yake alifufua dunia wa zamani kwa zambi na aliunganisha mutu na Muumba yake, Mungu. Huyu Yesu Kristu mumoja anatwaambia ya kama inakuja saa ya kutukuzwa Mwana wa mutu (Kristu) na alisema juu ya kunyanyua Kwake pa Musalaba (Yoane 12,23). Tena, alituwaambia ya kama, kama atanyanyuliwa ku inchi, atakokota wa\ote kwa maugu Yake. Alipenda kusema namna gani atakufa (Yoane 12,31-32).

Musalaba ni alama ya Kristu Musulubiwa, inaleta neema yake kwa Mateso yake. Kwa hivi, sisi waortodoksi tunafanya alama ya Musalaba pa kilari yetu juu ya kukumbuka hii tendo la Kusulubiwa kwa Kristu juu ya Msalaba, na ya pili juu ya kutukuza hii Muti takatifu.

Tena Musalaba ni alama yenye kutangulia ibafa ya Mafumbo yote ya Kanisa yetu, kwa sababu kwa ajili ya hii mafumbo inatimizika wokovu wetu. Musalaba haiko kitu kimoja sawa ulozi, lakini ni kitu kitakatifu na inaleta neema ya Yesu Kristu mu uzima yetu. Hii Neema haitoke ku muti wa Musalaba, lakini inatoka kwa Bwana Yesu Kristu kwa imani yetu. Ni vile waliponyeshwa na wale Waebrania jangwani wakati waliangalia ule nyoka ya shaba. Matunzo na wokovu yao ilitokea hapana kwa nyoka ya shaba, lakini kwa imani yao kwa ulinzi na uwezo wa Mungu. Vilevile, Musalaba ni alama ya ushindi na ya utukufu ya kukombanisha nayo shetani na matendo yake mbaya. Ku mwisho ya hii dunia, wokovu itakuwa paka kwa wale watu wanafanya alama ya Musalaba mu uzima yao.

Maana ingine ya Musalaba ni juu ya sisi kusulubisha tamaa na matendo yetu mbaya sababu ya kupokea Neema ya Mungu, hivi tutaweza kuishi katika maisha yetu na uzima mupya katika Kristu. (Angalia Marko 8,34 na Matayo 10,38).

# MAFUNDISHO JUU YA KUBUSU NA KUSUJUDU MIFUPA YA WATAKATIFU

Kwa sababu Waprotestants wanakataa Watakatifu na picha zao, kunafwata na mambo ingine : wanakataa kuheshimu Mifupa takatifu ya Watakatifu yenye kutosha harufu nzuri ya manukato na ingine yanafanya miujiza ya ajabu kwa wale waaminifu wanaikimbilia na imani na wanaibusu na heshima na utukufu.

Neema ya Kristu inatakasa hapana paka roho, lakini na miili ya waaminifu waorthodoksi. Kwa hivi tunaona mpaka sasa Miili ya Watakatifu fulani iko paka muzima, haioze ao kuharibika, lakini inatosha harufu nzuri ya marasi na manukato. Mtume Paulo anatwaambia hivi : "*Hamujui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mutakatifu aliye ndani yenu, muliyepewa na Mungu?* (1 Wakorinto 6,19). Huyu Roho Mtakatifu anafanya miujiza katika Watakatifu kama alikuwa mu uzima yao ya hapa duniani, atakuwa tena mu uzima yao ya milele. Maandiko Takatifu yanatwaambia miujiza ya miili yaliyokwisha kufa kwa wafu wengine : Mu Kitabu cha 2 Wafalme 13,20-21) tunasoma ya kama : "*Elisa akakufa, nao wakamuzika. Basi vikosi vya Wamoabu wakaingia katika inchi mwanzo wa mwaka. Na ilikuwa wakati walipokuwa wakizika mutu, tazama, waliona kikosi; wakatupa yule mutu katika kaburi la Elisa; na wakati yule maiti alipogusa mifupa ya Elisa, alifufuka, akasimama kwa miguu*". Hapa tunaona ya kama walitupa kijana moja wa kabila ya Moabu ndani ya kaburi ya Elisa na wakati aligusa mifupa yake, alifufuka. Tena na mu Agano Jipya tunaona hii mambo : "*Wakamusihi waweze kugusa pindo la vazi lake tu; na wote waliogusa wakaponyeshwa"* (Matayo 14,36). Hapana paka pindo ya vazi yao ilikuwa na nguvu ya kutunza, lakini na vitambaa vyenye vilikugusa mwili wa Mtume Paulo. Tazama :"*Mungu alifanya kwa mikono ya Paulo maajabu zaidi, hata watu walitwaa vitambaa na nguo zilizogusa mwili wake wakaziletea wagonjwa, na magonjwa yao yaliwaondoka, pepo wachafu wakawatoka. Lakini Wayuda wengine, wenye kutangatanga, nao ni wafumu wa pepo, wakajaribu kutaja jina la Bwana Yesu juu yao waliokuwa na pepo wachafu, wakisema: Tunawaapiza ninyi kwa Yesu yule anayehubiriwa na Paulo"* (Matendo 19,12-13). Hapana tunaona paka nyoka ya shaba na Mifupa ya Elisa mu Agano la Kale, lakini na Vitambaa vya Paulo vilifanya miujiza na kivuli cha Petro; katika hii mustari tunaona : "*Hata walibeba wagonjwa inje katika njia, wakawaweka juu ya mikeka na vitanda, ili Petro akikuja, kivuli chake kiwafikie wachache wao"* (Matendo 5,15-16).

Mtakatifu Grigori Palama anasema : *Tunasujudu Mifupa takatifu, kwa sababu uwezo ya utakaso bado kutoka ndani yao, sawa vile ilikuwa Mwili ya Kristu, kisha kufa kwake katika siku tatu.* Hii nguvu ya utakaso yao ni tunda la umoja wa Watakatifu wetu na Kristu, walimuvaa sawa nguo, kwa ubatizo yao (Wagalatia 3,27) na waliichunga safi mpaka mwisho ya uzima yao (1 Watesalonika 5,23).

Mtakatifu Simeoni Mthéologien anasema hivi : "Roho iliyostahiliwa kupata Neema Takatifu inaleta utakaso na ku mwili yake, kwani inaikaa ndani yake". Kwa hivi, sawa vile Neema Takatifu inakaa ndani ya roho, vilevile inaingia na inakaa ndani ya mwili. Mwili inabaki na hii neema hata pasipo roho na inaungana na hali kimungu, nikusema Neema Takatifu, uwezo kimungu na miujiza zinaonekana kwa watu . Kisha kufa kwa mwili, hakuna umoja kati ya mwili na roho, lakini yote mbili iko na neema takatifu ile vilichukua wakati vilikuwa pamoja katika hii dunia mbele ya kufa kwa mwili.

Kanisa yetu inaheshimu na kutukuza Mifupa takatifu ya watakatifu wetu tangu karne ya kwanza. Ilijenga mahekalu pa hii fasi walifia na mateso mengi na iliamuru kuweka kipande kidogo cha mufupa ya mtakatifu fulani ndani ya tundu yulu ya Meza Takatifu.

## MAFUNDISHO JUU YA MAKUMBUSHO YA WAFU

Waprotestants waliuhukumu makosa ya Katholika ya Roma, kwa mufano : moto ya kutakasa (Purgatori), maondoleo ya zambi na kartasi ya kuhurumia zambi, waliondoa kabisa sala na makumbusho yote ya wale waliyokufa.

Kanisa yetu Orthodokse haisadiki ya kama Kanisa ya Katholika ya Roma, kwa sala zake, haiwezi kusamehe zambi kubwa za watu, wala kuombea wokovu wale wasiyo na imani. anaomba Kanisa yetu Orthodoksi inaomba kwa Mungu maondoleo ya zambi za wale watu waliishi na utawa na imani na anamuomba vilevile Mungu usamehe wa makosa yao kidogokidogo yale hawajaugama bado.

Wafu waovu hawawezi kusaidia mwili yao, kwa sababu mu gehena hamuna toba. Hii kazi ni Kanisa inaifanya wakati padri anakumbuka majina yao ku Matayarisho (Proskomidi) ya Liturgia Kimungu.

Ushuhuda ya Makumbusho ya wafu tuko nayo mu Agano la Kale katika kitabu cha 2 Makabeo (12,40-45). Hapa tunasoma ya kama Yuda Makabeo alituma ku Yerusalema feza juu ya kutoa sadaka kwa usamehe wa zambi za waaskari yake mingi walikufa ku vita kwa sababu alisadiki ufufuo wa wafu. Tena, ndani ya mifuko ya mavazii yao walipatamo sanamu kidogo zile waliiba ku vita, sanamu hizi zilikataziwa toka sheria ya Mungu. Kisha Yuda Makabeo alifanya sala juu Mungu asamehe hii makosa yao.

Tunaona tena ya kama mu Agano la Kale Waebrania walifunga chakula juu ya waaksari wafu wao. Tena, kisha maziko yao walikabula kipande kimoja cha mukate sawa vile inafanyika leo mu Kanisa yetu orthodokse kwa ibada ya makumbusho ya wafu. Waebrania walizani ya kama ni kuzarau wafu wao kama wanakataa kukabula kipande cha mukate ku maziko ya ndugu yao. Yeremia anaandika hivi: "*Wala watu hawatagawia mukate kwa ajili yao, wakati wa kuomboleza, ili kuwatuliza, kwa ajili yao waliokufa*" (Yeremia 16,7). Katika Kitabu cha Nehemia inaandikwa ya kama wana wa Israeli kisha kifunga chakula waliungama kwa Mungu sababu ya kupokea maondoleo ya zambi, hapana paka ya zambi zao, lakini na zambi za ndugu zao waliokufa zamani. "*Basi kwa siku ya makumi mbili na ine ya mwezi huu wana wa Israeli walikuwa wamekusanyika wakifunga chakula, na wakivaa gunia, na kujitia udongo vichwani…na sehemu moja ya ine nyingine wakakiri zambi na kuabudu Bwana Mungu wao*" (Nehemia 9,1-3).

Mafundisho ingine juu ya makumbusho ya wafu iko katika Agano Jipya mu barua yake ya pili kwa Timotheo (2 Timotheo1,18). Kule Mtume Paulo anamwandikia mupendwa wake Timotheo juu ya Onesiforo : "*Bwana amujalie rehema kwa Siku ile!Unajua vizuri sana vilevile kazi zote alizonitendea katika Efeso*".

Tuko na mifano mingi katika vitabu vya Watakatifu wetu juu ya makumbusho ya wafu Karne ya kwanza na ku mbele.

Tertilianos, ku mwaka 200, kisha kuzaliwa kwa Kristu anasema: " **Tunafanya maombezi na kutoa sadaka kwa ajili ya mapumziko ya wafu, zaidi siku ya kuzaliwa kwao**" (Siku ya kuzaliwa kwao ni ile siku walikufa katika mwili na waliingia mu uzima ya milele).

Origenis, théologien mkubwa, aliyeishi ku mwaka 250, kisha kuzaliwa kwa Kristu anaandika hivi : "***Ni haki na ya mafaa sisi kufanya makumbusho na sala juu ya wale walilala milele".***

Mtakatifu Augustino (354-430) anaandika hivi : " **Ilikuwa zoezo ya Kanisa yetu tangu mwanzo wa Kristianisme kutoa sadaka kwa ajili ya wafu wake na kuwakumbuka**".

Mtakatifu Athanasi, patriarche mkubwa wa Aleksandria mu karne ya ine anaandika hivi : "Hata kama mwaaminifu alikufa na pepo ao na namna ingine, wewe toa mishumaa na mafuta, kwani Mungu anayakubali hii sadaka. Sadaka ya Mwili wa Kristu inaleta usamehe ya zambi zao na sadaka ya vitu mbalimbali kwa maskini inaleta faida ya roho ".

Kwa kifupi, Kanisa yetu Orthodokse anasadiki ya kama sala zetu juu ya ndugu zetu waliyokufa zinapaswa kutolewa na mapendo na imani. Tunapashwa kuwakumbuka wafu, hawa ndugu zetu walikuwa na imani; na sisi kwa imani na mapendo tunamuomba Mungu asaidie roho zao, ni saidio kubwa toka kwa Mungu, ni tunda la imani yetu.

Sala ya makumbusho inasaidia hapana paka wafu, lakini na wazima. Inawasaidia kuishi na mapendo, na kwa wale walisafiri kwa uzima ingine (wafu) wanasikia ya kama weko mu umoja na ndugu zao. Hivi wanasikia ya kama Kanisa ni moja, na Kichwa chake ni Bwana Yesu Kristu.

## MAFUNDISHO JUU YA KUFUNGA (KWAREZIMA)

Kwa ushuhuda wa Mtakatifu Basile kufunga chakula ni amri ya zamani kabisa, kwani Mungu aliwaambia wazazi wa kwanza hivi: “*Lakini wa muti wa kujua uzuri na ubaya usile kwa maana siku unapokula, hakika utakufa”* (Mwanzo 2,17)

Kufunga ni kuacha kula chakula mbalimbali wakati fulani. Tena kufunga ni kuacha kutenda zambi zote juu mukristu apate fazila na Neema ya Kristu katika maombi, sala na ushirika wa Kanisa na Mafumbo yake. Kufunga ni namna ya mutu kupata fazila na kuacha tamaa zake. Haiuwe mwili, lakini inaua zambi na tamaa mbaya. Inasaidia mwili juu ya kusafisha roho, hivi, akili na roho yake zitapanda mbinguni na zitapata utakaso.

Ni Bwana Yesu Kristu mwenyewe alitupatia mufano ya kufunga, alifunga katika siku makumi ine. Tena Yeye alitufundisha ya kama mashetani wanafukuzwa kwa njia ya sala na kufunga (Matayo 17,21).

Mitume Watakatifu walifanya kazi yao kimungu na kufunga : “*Nao walipokuwa wakitumikia Bwana na kufunga,…”* (Matendo 13,1-4). Mtume Paulo, hata kama aliteswa na mahangaiko katika safari yake, alifunga : “ *katika mapigo, katika vifungo, katika fitina, katika taabu, katika kulinda, katika kufunga chakula, katika usafi, katika elimu, katika uvumilivu, katika kutendea vema, Katika Roho Mutakatifu, katika mapendo pasipo udanganyifu*…” (2 Wakorinto 6,5).

Waprotestants waliharibisha mafungo yote na wanashitaki Kanisa Orthodokse ya kama inakosa kwa sababu inakataa kutumia chakula mbalimbali. Tena wanaleta hii mustari ya Mtume Paulo : (1 Timotheo 4,3) *: “Wakikataza watu kuoana, na wakiagiza watu wakatae vyakula Mungu alivyoumba, kupokea na ushukuru na walio na imani na kujua kweli*”.Hapa Mtume Paulo anasema juu ya wale watu wanazania ya kama chakula ingine iko na uchafu na imekwisha kukataziwa. Kanisa yetu inaturuhusu sisi kula chakula yote, kwani haina na uchafu, lakini tunafunga chakula ingine kwa wakati fulani katika mwaka juu ya maneno ya dini na ya roho.

Waprotestants wengine wanakubali kufunga, lakini kwa mapenzi ya kila mutu. Wanakataa kufunga kila mu kazi tatu na kila mu kazi tano, lakini hii Kufunga ya masiku hizi mbili iliandikwa mu Kitabu cha Mafundisho ya Mitume (Mapokeo ya Mitume ao Les Saintes Traditions, iliandikwa tangu mwaka 100-160, kisha kuzaliwa Kristu. Tena Klimis wa Aleksandria anaandika ya kama mu Kanisa yetu ni lazima waaminifu kuchunga hii kufunga ya mu kazi tatu na mu Kazi Tano. Lakini Kufunga kwa masiku makumi ine ilitengezwa ku Mukutano Ikumeni ya kwanza ku mwaka 325, kisha kuzaliwa Kristu.

Ku mwisho tunasema ya kama Kufunga chakula ilitokea kwa Mungu na inapatikana katika Maandiko Takatifu na Mapokeo Takatifu. Ni namna ya utakaso na inafanyika kwa kila mwaminifu wa kweli kwa baraka ya padri wake wa roho.

**xxxxxxxxxxxxxxoOoxxxxxxxxxxxxx**